# Nipashe

Jumatano Machi 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579876

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Shahidi kesi ya Malinzi amwaga chozi kortini

UKURASA 3




UKURASA 13

# Njia hujuma mapato U/Taifa hadharani

• **Wajanja** watumia mbinu kinyonga kujipatia fedha za viingilio, kila mdau atajwa kuhusika na mchezo huo, TFF yajitetea...*Endelea ukurasa 2*





Moja ya nyumba za kifahari anazomiliki mtuhumiwa wa kosa la utakatishaji wa fedha haramu na kujipaitia mali, Magreth Kobelo Gonzaga (Picha ndogo), iliyopo Tegeta, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOHN BADI**

## Takukuru yamsaka mmiliki 'mahekalu'

UKURASA 2

## Zitto amjibu msajili vyama

UKURASA 3




HABARI KITAIFA

# Hujuma nzito za mapato U/Taifa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli juzi, alihoji maswali magumu kuhusu uhalisia wa ukusanyaji na matumizi ya mapato ya Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam.

Kiongozi huyo mkuu wa nchi, pia alihoji kuhusu ukarabati wa uwanja huo, usalama wa mashabiki na mfumo wa ukataji tiketi, akitolea mfano mechi ya Jumapili iliyopita ambayo Tanzania ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Uganda, idadi kubwa ya mashabiki wenye tiketi wakizuiwa kuingia uwanjani kutokana na uwanja kufurika.

"Ingawa mimi sijauliza wala sikutaka kuuliza kwamba jana (Jumapili) mlikata tiketi nyingi na uwezo wa uwanja ni watu 63,000 na zaidi ya nusu ya watu walikuwa nje, zimekusanywa kiasi gani? Sijauliza na wala siulizi. Na hizo zingine zimeenda kwenye akaunti gani?

"Ukarabati hauko vizuri, asilimia zinazokatwa kwa ajili ya uwanja zinatumika kufanya nini? Je, wizara inafanya nini? Je, viongozi wa wizara huwa hawaendi uwanjani kuona? Kama uwezo wa uwanja ni kuchukua watazamaji 63,000 na kama watu wengi walikata tiketi, je, tiketi za Tanzania hazina 'limit' (ukomo)?

"Je, suala la ulinzi limeangaliwaje na wizara? Je, kama watu 200,000 wangeingia ndani, je, kama wangedondoka, watu wangapi wangefariki (dunia)? Je, wizara, vyombo vya ulinzi wanalionaje suala hili?" Rais Magufuli alihoji alipokutana Ikulu jijini Dar es Salaam na wanamichezo walioipatia sifa Tanzania katika mashindano ya kimataifa.

**RUSHWA MAGETINI**

Ripoti za TFF na Bunge za mwaka 2011 na 2014 kwa mfuatano huo, zinabainisha mbinu mbalimbali zinazotumika kuhujumu mapato ya milangoni kwenye viwanja vya soka nchini, ukiwamo Uwanja wa Taifa.

Juni 4, 2014, Bunge lilieleza serikali inavyopoteza mabilioni kutokana na hujuma dhidi ya mapato yatokanayo na viingilio kwenye viwanja vya soka nchini.

Akiwasilisha bungeni mjini Dodoma siku hiyo taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2014/15, aliyekuwa mwenyekiti wa kamati hiyo, Luhaga Mpina, alisema:

"Serikali haipati mapato ya kutosha kutokana na mpira wa miguu kwa sababu ya tiketi bandia kuendelea kutumika, kukosekana kwa uwazi katika mapato halisi, uwezo mdogo wa kusambaza tiketi nchi nzima na rushwa kwenye mageti ya viwanja."

Mpina ambaye kwa sasa ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, aliliambia Bunge kuwa kwa muda mrefu serikali imekuwa haipati mapato ya kutosha kutoka katika sekta ya michezo, hususani mpira wa miguu ulio chini ya TFF, kutokana na mfumo dhaifu wa ukusanyaji fedha wakati wa kuuza tiketi.

**MFUMO DHAIFU**

Wakati Bunge likibainisha hayo, Ripoti ya Kamati Maalum ya Kudhibiti na Kuboresha Mapato ya TFF iliyotolewa Mei 2011, inaeleza kuwa baadhi ya watendaji wa TFF wamekuwa wakihujumu mapato ya milangoni kutokana na mfumo dhaifu wa uandaaji na uuzaji tiketi.

Ripoti hiyo yenye jumla ya

INAENDELEA UK. 8



Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu barua waliyoipokea kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. Kulia ni Mwenyekiti wa chama hicho, Yeremia Maganja. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## Magufuli amtumbua Mkurugenzi TAA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli amemteua Mhandisi Julius Ndyamukama kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Taarifa iliyotolewa na Ikulu jana, ilisema Mhandisi Ndyamukama anachukua nafasi ya Richard Mayongela, ambaye uteuzi wake umetenguliwa na anatakiwa kuripoti Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambako atapangiwa kazi nyingine.

Kabla ya uteuzi huo Mhandisi Ndyamukama alikuwa Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Dar es Salaam, na ndiye alikuwa msimamizi mkuu wa ujenzi wa majengo namba 3 (Terminal 3) ya uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam ambayo yapo katika hatua za mwisho kukamilika.

Uteuzi wa Mhandisi Ndyamukama ulianza jana.

# Takukuru yamsaka mmiliki 'mahekalu'

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inamsaka Magreth Gonzaga, mkazi wa Kinondoni jijini Dar es Salaam kwa tuhuma za utakatishaji wa fedha haramu.

Magreth anayedaiwa kumiliki nyumba tatu za kifahari jijini, anatuhumiwa kutakatisha fedha haramu kinyume cha Kifungu Na. 12(d) na 13(a) cha Sheria ya Utakatishaji Fedha Haramu Na. 12 ya Mwaka 2006.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Diwani Athumani, alisema wanamsaka Magreth kupitia tangazo lililotolewa kwa amri ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu inayosikiliza shauri la jinai namba 28 la mwaka 2019.

Alidai Gonzaga ambaye kwa sasa anadaiwa kukimbilia nje ya nchi, anatafutwa na Takukuru kwa tuhuma za kutakatisha fedha haramu na kujipatia mali kupitia Kampuni ya Superior Financing Solution Limited (SFS) inayodaiwa kufanya biashara bila kulipa kodi ya serikali.

"Wakati uchunguzi unaendelea, mtuhumiwa alitoroka nchini," Athumani alisema.

"Kisheria mtuhumiwa huyo anahesabiwa kama ni mtuhumiwa aliyetoroka. Kutokana na sababu hiyo, Takukuru inapaswa kutangaza kutafutwa kwake kabla ya kutaifisha mali alizojipatia kwa njia ya rushwa," aliongeza.

Alisema uchunguzi umebaini mtuhumiwa huyo katika nyakati tofauti, kwa kutumia fedha ambazo ni zao la ukwepaji kodi, alinunua viwanja vilivyoko ufukweni mwa Bahari ya Hindi pamoja na nyumba tatu.

Athumani alidai kuwa mbali na nyumba tatu za Kinondoni, mtuhumiwa pia anamiliki viwanja vitatu vilivyoko wilayani Temeke jijini.

"Hii ni moja ya nyumba ambayo inamilikiwa na Gonzaga ambazo tunategemea kuiomba mahakama iwe mali ya serikali, iwapo hatarudi nchini kujibu tuhuma zinazomkabili," Athumani alidai akiwa nje ya moja ya nyumba zinazodaiwa kumilikiwa na Magreth maeneo ya

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
26 - 03 - 2019

**TANGAZO**

1 . Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 03-04-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar -Es-Salaam kuelekea Tunduma,** gari hizo zenye namba za usajili:

**T 416 DFE / T 416 AYQ**
**T 628 DFA / T 139 CHN**
**T 780 DDU / T 723 AUW**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.80** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Tunduma Kupitia Iringa,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215141302



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 26/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa** tarehe **29/03/2019** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA** kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili:

**T679 CUL /T944 OPE.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | **21 METRES** |
| **Upana** | - | mita | **3.0 METRES** |
| **Kimo** | - | mita | **4.6 METRES** |

3. NJia itakayotumika **TUNDUMA hadi DAR ES SAALAM** kupitia **VIGWAZA** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

115140802

HABARI KITAIFA

# Shahidi kesi ya Malinzi aangua kilio kortini

**Na Hellen Mwango**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, shahidi wa 12 ambaye alikuwa dereva, Steven John, jana aliangua kilio kwa muda kabla ya kuanza kutoa ushahidi wa Jamhuri dhidi ya bosi wake, Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, na wenzake wanne wanaokabiliwa na kesi ya utakatishaji fedha.

Saa 10:34 asubuhi, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde ilianza shughuli zake.

Washtakiwa watano, akiwamo Malinzi, walipanda kizimbani kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa Jamhuri dhidi ya mashtaka ya kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, alimwongoza shahidi. Hata hivyo, shahidi alianza kujifuta machozi.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya hakimu na shahidi;

Hakimu: Shahidi mbona huongei?

Shahidi: Hakujibu kitu.

Hakimu: Shahidi una tatizo gani macho yamefanyaje?

Shahidi: Hayana tatizo.

Shahidi huyo aliyefika kutoa ushahidi dhidi ya bosi wake Malinzi alionekana kizimbani akijifuta machozi.

Baada ya dakika tano kupita, saa 4;42 alianza kutoa ushahidi wa Jamhuri.

Alidai kuwa aliajiriwa na TFF mwaka 2015 kama dereva wa Malinzi na kwamba alikuwa akiagizwa kwenda kwenye ofisi za shirikisho hilo kuchukua fedha kwa aliyekuwa mhasibu Hellen Ndaro na kumpelekea.

Alidai kuwa kabla ya ajira yake kukoma mwaka 2017, kabla ya kukabidhiwa fedha hizo na Ndaro alitia saini na Septemba 26, 2016 alimpelekea Dola 28,650, Dola 24,000 na Septemba 26, 2016 alimpelekea Sh. milioni nne.

"Niliwahi kuitwa Takukuru mara tatu na bosi wangu Malinzi aliniambia nikaeleze ukweli ninaoufahamu," alidai John.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna shahidi mwingine.

Hakimu alisema kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Aprili 9, mwaka huu.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Mwesigwa Selestine; Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga; Meneja wa Ofisi TFF, Miriam Zayumba; na Karani wa TFF, Flora Rauya, ambao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 30 katika kesi ya jinai namba 213 ya mwaka 2017.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walikula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Dola za Marekani 173,335.

Malinzi, Mwesigwa na Nsiande wanaendelea kukaa rumande kwa sababu wanakabiliwa na mashtaka ya utakatishaji fedha ambayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.

## Zitto amjibu Msajili wa Vyama vya Siasa

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amejibu hoja tatu zilizotolewa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kuhusu tishio la kukifutia usajili wa kudumu chama hicho endapo kitashindwa kutoa majibu ndani ya siku 14.

Juzi Ofisi ya Msajili kupitia kwa Naibu Msajili wa vyama hivyo, Sisty Nyahoza. ilikiandikia chama hicho ikitishia kukifutia usajili endapo hakitawasilisha ripoti ya hesabu za fedha za chama hicho kwa mwaka 2013/2014.

Hoja nyingine ambayo ofisi hiyo ilikitaka chama hicho kujibu ni kudaiwa kuchoma bendera za Chama cha Wananchi (CUF), tukio linalodaiwa kufanywa na wanachama wa ACT-Wazalendo lililoonekana kupitia ujumbe wa video katika mitandao ya kijamii.

Msajili alikituhumu chama hicho kutumia vibaya tamko takatifu la dini ya Kiislamu (Takbir) katika ujumbe wa video iliyowaonyesha watu wakipandisha bendera ya ACT-Wazalendo huku wakitamka neno hilo.

INAENDELEA UK. 8




//KUWA UNSTOPPABLE. Benki popote na SC Mobile Tanzania App. Benki ya kidigitali kiganjani

SC Mobile inamaanisha kubenki kirahisi na kwa usalama popote. Inachukua dakika 15 tu kufungua akaunti ya Standard Chartered na kuwa Unstoppable. Zaidi ya hayo, utafurahia huduma za kibenki zaidi ya 70, kiganjani.

Ipakue leo na ujionee njia mpya ya kubenki!

Download on the App Store

GET IT ON Google Play

215141002

sc.com/tz

Here for good

*Terms and conditions apply. Standard Chartered is regulated by the Bank of Tanzania.

# PM achukizwa wizi wa mitihani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa onyo kali kwa baadhi ya maofisa elimu wa mikoa na wilaya wanaoshirikiana na walimu kujihusisha na wizi, udanganyifu na uvunjaji wa mitihani na kuwataka waache mara moja tabia hiyo kwa sababu unalivunjia heshima na hadhi taifa.

"Kamati za mitihani za mikoa na wilaya ziendelee kusimamia sheria, kanuni na taratibu bila ya woga, uendeleo na tusiyumbishwe na hatua za kinidhamu na kiutumishi kwa mujibu wa sheria. Hatua ziendelee kuchukuliwa dhidi ya wote wanaobainika kukiuka sheria, taratibu na miongozo inayotolewa," aliagiza.

Alitoa onyo hilo jana wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa sita wa Umoja wa Maofisa Elimu Mikoa na Wilaya (REDEOA), uliofanyika jijini Dodoma.

Kaulimbiu ya mkutano huo inasema "Elimu bora itatufikisha katika uchumi wa kati ifikapo 2025".

Waziri Mkuu alisema, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) ni chombo ambacho kwa muda mrefu kimejijengea sifa nchini na barani Afrika, na serikali imewekeza kiasi kikubwa cha rasilimali ili kukifanya chombo hiko kuwa imara na cha kisasa. Alisema hali hiyo imezifanya nchi mbalimbali kuja nchini kujifunza masuala ya upimaji na uendeshaji wa mitihani. "Nimejulishwa pia hivi sasa hapa nchini wapo viongozi wa mabaraza ya mitihani kutoka nchi za Afrika Mashariki."

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema suala la tatizo la nidhamu mbaya ya wanafunzi ni jukumu la walimu wote, hivyo wanatakiwa watekeleze majukumu yao ya kufundisha, kulea, kuwaongoza na kuwaendeleza wanafunzi kimwili, kiakili na kiroho kwa uadilifu na kuzingatia sheria. Alisema serikali imesikitishwa na matukio ya hivi karibuni ya athari ya viboko kwa wanafunzi shuleni ikiwamo kuvunjwa mikono, kuachwa na makovu pamoja na tukio la kifo cha mwanafunzi Sperius Eradius wa Shule ya Msingi Kibeta mkoani Kagera.

"Ninatambua si kusudio la walimu kuwadhuru wanafunzi, lakini tukubaliane kuwa kuna udhaifu katika utaratibu wa utoaji na usimamizi wa adhabu ya viboko shuleni. Maofisa elimu kawakumbusheni walimu wote nchini wazingatie mwongozo wa kutoa adhabu shuleni chini ya kifungu cha 61 cha Sheria ya Elimu sura ya 353 pamoja na kanuni zake."

"Adhabu ya viboko itatolewa iwapo patatokea utovu mkubwa wa nidhamu au kosa kubwa litakalofanywa ndani au nje ya shule ambalo litaishushia shule heshima. Na adhabu hii itatolewa kwa kuzingatia umri, jinsia na afya ya mwanafunzi. Nina hakika tukisimamia utaratibu, matukio haya yaliyoanza kuonekana yatakoma," Waziri Mkuu alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Selemani Jafo, amewapongeza maofisa elimu hao kwa sababu wanafanya kazi kubwa ambayo imechangia kupandisha ufaulu wa kidato cha sita na cha nne nchini.

Naye Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, aliwataka maofisa hao wawe wanatoa taarifa sahihi kuhusu idadi ya wanafunzi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Mwenyekiti wa REDEOA, Germana Mung'aho, alisema umoja wao unatekeleza majukumu yao ya kusimamia elimu kikamilifu nchini, lengo likiwa ni kumuunga mkono Rais Dk. John Magufuli, ambaye anasisitiza watu wafanye kazi.

## NEC kuanza uandikishaji wapigakura kwa majaribio

**Na Margareth Chambiri**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kufanya zoezi la uandikishaji wa wapigakura kwa majaribio katika kata ya Kibuta iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani na Kihonda, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, mkoani Morogoro.

Taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Tume, Jaji (Rufani) Semistocles Kaijage, jijini Dar es Salaam jana, ilisema uandikishaji huo utakaoanza Machi 29 hadi Aprili 4, 2019, utafanyika katika vituo 20 vya kuandikisha wapigakura vituo 10 katika kila kata.

INAENDELEA UK.26



Mwonekano wa mzunguko wa makutano ya Barabara ya Morogoro na Sam Nujoma, katika eneo la Ubungo, unaendelea kujengwa jijini Dar es Salaam jana, ambao umepunguza foleni ya magari na kuwa mkombozi mkubwa kwa watumiaji wa barabara hizo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**




## Nauli yakwamisha mashahidi kesi ya Gugai

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi inayomkabili Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Godfrey Gugai na wenzake umedai kwamba umeshindwa kuita mashahidi kutoka nje ya Dar es Salaam kwa sababu hawana fedha za kuwalipia nauli.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Awamu Mbagwa, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba. Mbagwa alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa jana na leo ushahidi wa Jamhuri, lakini wameshindwa kuwaita mashahidi kwa sababu hawana fedha za kuwalipia nauli.

"Mheshimiwa hakimu mashahidi wamesema hawana uwezo wa kujisafirisha kuja kutoa ushahidi, tumeshindwa kupata mashahidi kwa sababu wote wanatoka nje ya Jiji la Dar es Salaam," alidai wakili wa serikali na kuongeza:

"Tunasikitika hatuwezi kuendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri kutokana na sababu ya kukosa fedha, utawala utakapokaa sawa tutafanikisha usikilizwaji," alidai Wakili Mbagwa.

Wakili wa utetezi Alex Mgongolwa, alidai kuwa anaomba suala la kuwaita mashahidi lifanyiwe kazi haraka.

Hakimu alisema malipo ya mashahidi yana utaratibu wake na kwamba mahakama yake italifanyia kazi.

"Tutalitatua hili suala linazungumzika halina shida," alisema Hakimu Simba.

Alisema kesi hiyo itasikilizwa Aprili 8, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu. Mbali na Gugai, washtakiwa wengine katika kesi hiyo, ni George Makaranga, Leonard Aloys na Yasin Katera.

Gugai na mwenzake watatu wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo, 19 ni ya kughushi, 23 ya utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Katika kesi ya msingi, Gugai na mwenzake, wanakabiliwa na makosa 43, kati ya hayo 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Gugai anakabiliwa na kosa la kumiliki mali kinyume na kipato chake, alidaiwa kutenda kosa hilo kati ya Januari 2005 na Desemba 2015.

Inadaiwa kuwa akiwa Takukuru Dar es Salaam, Gugai alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake huku akishindwa kuzitolea maelezo.

HABARI KITAIFA

# Polisi waipa ulinzi CUF kupachika bendera

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimefanikiwa kupachika bendera na kuzifungua ofisi zake katika makao makuu yake Mtendeni Mjini Unguja chini ya ulinzi mkali wa Jeshi la Polisi.

Awali, baada ya wafuasi wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, walizigeuza ofisi hizo kuwa za ACT-Wazalendo.

Maalim Seif, viongozi na wanachama kadhaa waliokuwa CUF walijiondoa katika chama hicho hivi karibuni na kujiunga na ACT-Wazalendo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa CUF, Mussa Haji Kombo, alisema lengo la kufanya hivyo ni kuona ofisi hiyo inatumika kwa ajili ya shughuli za kichama, na kwamba ni mali halali ya chama hicho na si za ACT-Wazalendo.

"Hizi ofisi ni mali ya chama cha CUF na sio mali ya mtu kama Maalim Seif... kaamua kwenda ACT-Wazalendo akatafute jengo lingine kwa shughuli zao na sio jengo hili la CUF," alisema Kombo.

Alisema mbali ya kuchukua hatua hiyo ya kuiweka sawa ofisi hiyo, pia tayari wameshafungua kesi mahakamani ya kuwashtaki wahusika wote wa vitendo vya uhujumu wa mali za CUF baada ya Maalim Seif kuhamia ACT-Wazalendo.

Alisema kitendo hicho hakikubaliki hata kidogo, ndio maana wakaona ni busara kuchukua maamuzi ya kufungua kesi, kwa kuwa lengo la vyama vya siasa si uhasama bali ni sehemu ya kuelekea katika maendeleo ya kweli.

Tangu Jumatatu ya wiki iliyoisha majengo yote ya CUF Unguja na Pemba yalipakwa rangi za ACT-Wazalendo na kupachikwa bendera za chama hicho, kitendo ambacho kinaonekana kufanywa na wafuasi wa Maalim Seif kumuunga mkono baada ya kutangaza kujiunga na ACT- Wazalendo.

## Mahakama kusikiliza maelezo awali kesi ya vigogo TPA

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepanga kusikiliza maelezo ya awali ya kesi inayowakabili vigogo wanne wa zamani wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), akiwamo Mkurugenzi Mkuu Ephraim Mgawe ya matumizi mabaya ya madaraka na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 984.8.

Mbali na Mgawe washtakiwa wengine ni, Wajumbe wa Bodi ya Manunuzi ya TPA, Happiness Senkoro, Apolonia Mosha na Theophil Kimaro. Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na waendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru), Maghela Ndimbo na Nickson Shayo. Ndimbo alidai kuwa maelezo ya awali yako tayari, lakini wanaomba kuwasilisha nakala kwa upande wa utetezi wayapitie.

"Mheshimiwa maelezo ya awali yako tayari tunawapa upande wa utetezi nakala kwa sababu ni marefu wakishayapitia tunaomba tarehe nyingine ya kuwasomea," alidai Ndimbo.

Hakimu Rwizile alisema washtakiwa watasomewa maelezo ya awali Aprili 25, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa nje kwa dhamana.

Katika kesi ya msingi ilidaiwa kuwa Septemba 28, 2010, katika ofisi za TPA zilizopo Ilala jijini Dar es Salaam, Mgawe akiwa mtumishi wa umma kama mkurugenzi mkuu na ofisa masulufu, alitumia madaraka yake vibaya kwa kushuhudia mikataba kati ya mamlaka hiyo na Kampuni ya Leighton Offshore Pte Ltd 19800397 na kupata faida ya Sh. 984,828,000 baada ya kuvunja sheria ya manunuzi kwa kuiwezesha kampuni hiyo kupata upendeleo.

Shtaka la pili la matumizi mabaya ya madaraka dhidi ya mshtakiwa wa pili, tatu na wa nne, Julai 13, 2010 katika ofisi ya TPA washtakiwa wakiwa watumishi wa umma na wajumbe wa bodi ya manunuzi, walitumia vibaya madaraka kwa kuidhinisha zabuni na kuvunja sheria ya manunuzi ya umma kwa kuiwezesha Kampuni ya Leighton Offshore Pte Ltd kupata faida ya Sh. 984,828,000.


TAARIFA KWA UMMA

Vodacom Tanzania yamteua Hisham Hendi kuwa Mkurugenzi Mtendaji

27 Machi 2019, Dar es Salaam

Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni ya Vodacom Tanzania, Ali A. Mufuruki anayo furaha kuutaarifu umma juu ya uteuzi wa Bw. Hisham Hendi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo kuanzia tarehe 19 Machi 2019. Bw. Hendi, aliteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo Septemba 1, 2018, chini ya uongozi wake Vodacom imepata mafanikio makubwa hasa katika utendaji ukizingatia ni soko lenye ushindani.

Bw. Hendi amekuwa na kampuni ya Vodacom Tanzania tangu mwaka 2016 kama Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara ambapo alipelekea mafanikio makubwa katika kitengo hicho. Hendi ana uzoefu wa miaka 15 katika sekta ya mawasiliano na amewahi kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika nchi za Ulaya, Misri na Afrika Kusini. Mwaka 2015 alifuzu mafunzo ya Uongozi "Vodafone's Global Leadership Program (Inspire)" kutoka chuo cha London Business School na mwaka 2013 alitunukiwa cheti cha Ubora wa Biashara "Commercial Excellence" kutoka chuo cha IMD Lausanne, Switzerland. Pia ana shahada ya Usimamizi wa Biashara kutoka chuo cha Kikuu cha Cairo.

Bw. Hendi anakuja na ujuzi huu kwenye kampuni, pamoja na uzoefu wake katika nyadhifa za kimataifa ambao utawezesha Vodacom kufikia malengo yake ya kuipeleka Tanzania kwenye zama za kidijitali na kuboresha maisha ya watu kwa kutumia teknolojia. Tuna imani kwamba chini ya uongozi wake Vodacom Tanzania itaendelea kutoa mchango katika jamii zinazoizunguka na kuisaidia Tanzania kufikia malengo yake ya maendeleo.

www.vodacom.co.tz



The future is exciting.

Ready?

vodacom

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vikwazo mabaraza ardhi sasa vitafutiwe ufumbuzi

**KUANZISHWA** kwa mabaraza ya ardhi nchini ulikuwa ni uamuzi wa serikali wenye lengo la kutafutia ufumbuzi migogoro ya ardhi iliyokuwa imeshamiri nchini.

Kimsingi, ilichosukuma kuanzishwa kwa mabaraza hayo ni kutokana na migogoro mingi ya ardhi kuchelewa kutolewa maamuzi, yakiwamo mashauri mengi yaliyokuwa yanafunguliwa katika mahakama.

Mbali na mashauri yaliyokuwa yakifunguliwa mahakamani kuchelewa kutolewa uamuzi kutokana na sababu kadhaa, ukiwamo uchache wa mahakimu, pia malalamiko yaliyokuwa yakipelekwa katika ngazi zingine, ikiwamo kwa viongozi wa mitaa, vitongoji na vijiji yalikuwa yanatolewa na kuacha shaka.

Walalamikaji wengi walikuwa wanakosa imani na viongozi wa ngazi hizo wakiwahisi kuwa walikuwa wanapindisha maamuzi kutokana na kupewa rushwa na watu wenye nguvu ya fedha. Wengi ni mashahidi kuhusiana na suala zima la migogoro ya ardhi iliyokuwapo pamoja na maamuzi yenye utata yaliyokuwa yanatolewa katika ngazi kadhaa za serikali hususan serikali za mitaa.

Itakumbukwa pia jinsi wananchi wengi wanyonge walivyokosa haki katika migogoro ya ardhi, kiasi cha kupoteza viwanja na mashamba yao kwa wachache walikuwa na ushawishi na nguvu ya fedha.

Uamuzi wa kuanzishwa kwa mabaraza ya ardhi hakika ulipokelewa na wengi kama ukombozi kwao kwa kuwa mashauri yamekuwa yakianza na kutolewa uamuzi ndani muda mfupi sambamba na kupunguza malalamiko dhidi ya maamuzi hayo.

Ni jambo ambalo serikali inastahili pongezi kutokana na migogoro ya ardhi kupungua sana kwa sasa kulinganisha na hali ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa mabaraza ya ardhi.

Hata hivyo, zimesikika taarifa kadhaa kuhusiana na baadhi ya changamoto ambazo zinakwaza mabaraza hayo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Imeelezwa kuwa kukosekana elimu kwa wajumbe wengi waliopo kwenye mabaraza ya ardhi na nyumba ngazi ya kata kunachangia kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa na kusababisha migogoro kwa wananchi pamoja na manung'uniko.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga, Doris Wilson, wakati wa warsha ya kuwajengea uelewa viongozi wa ngazi mbalimbali kuhusu ufahamu wa sheria na kufuata taratibu na kutoa maamuzi sahihi ili kutatua migogoro.

Alieleza kuwa changamoto kubwa ya mabaraza ya kata ni elimu kwa kuwa wajumbe wengi hawajapata elimu kuhusu mabaraza hayo, muundo, namna ya utendaji, akidi katika kuendesha na utaratibu wa kuendesha mashauri.


Alisema elimu hiyo itakuwa chachu kwa wajumbe hao kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwenye mabaraza hayo, lengo kubwa likiwa ni kuhakikisha wanatenda haki kwa wananchi ambao wanakabiliwa na migogoro mbalimbali kwenye maeneo yao.

Suala la elimu kwa wajumbe wa mabaraza hayo ni muhimu sana kwa sababu wanabeba jukumu kubwa na zito la kupokea, kusikiliza na kufanya maamuzi ya migogoro ya ardhi.

Ili kuendelea kuaminika kwa mabaraza hayo kwa wananchi na wadau kwa ujumla, kuna kila sababu ya kuwekwa utaratibu wa kuwapatia elimu wajumbe wa mabaraza hayo nchi nzima ili kuwaongezea uelewa, hivyo kutekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Hili lisiwe jukumu la serikali pekee, bali lifanyike kwa kushirikiana na wadau kwa kutilia maanani kuwa suala la ardhi ni mtambuka. Kwa maneno mengine linahusisha sekta nyingi. Bila shaka wadau wengine watajitokeza kutoa elimu hiyo kama Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (Tawla) Mkoa wa Tanga ilivyofanya kwa kutoa elimu kwa wajumbe hao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Acheni hujuma hizi mnapohama vyama

**BAADHI** ya wafuasi wa vyama vya siasa wamekuwa hodari kuharibu mali za vyama wanavyovikimbia, mchezo huo ukihusisha kuchoma kadi, bendera na sare na wakati mwingine hata kuharibu samani ofisini.

Imeshuhudiwa wapo wabunge waliposhindwa uchaguzi waliharibu ofisi walizokuwa wanazitumia kuwahudumia wananchi.

Mwanachama anaweza kuhama chama hiki na kwenda kingine na kuamua au chama kinaweza kupokea wanachama wapya na kuwatambulisha wageni huku kikichoma kadi za chama cha zamani tena kwa kushangiliwa.

Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, baadhi ya vyombo vya habari vilionyesha kadi zikiteketezwa baada ya wanachama hao kuhama kwenda upande mwingine.

Wakati huo karibu kila kona ya nchi kulikuwa na wanachama wanaotoka chama hiki na kujiunga na kingine hatua hiyo ikiambatana na ukusanyaji kadi na kuzitia kibiriti hadharani.

Wapo wanaofanya hivyo kwa kutukana, kukejeli na kulaani chama walichokikimbia. Baada ya kumalizika kwa uchaguzi huo kasi ya kuchoma kadi na bendera ilipungua, lakini tukio la hivi karibuni la aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad kuhamia ACT- Wazalendo, limerudisha upya uchomaji wa mali za vyama.

Hayo yanathibitishwa na video zilizorushwa kwenye mitandao ya kijamii zikiwaonyesha watu wanaodaiwa kuwa ni wanachama wa CUF, ambao wamehamia ACT- Wazalendo, wakichoma bendera.

Kutokana na kitendo hicho, Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, amekikemea kusema huo ni uvunjifu wa sheria na kuwaonya wahusika kuacha kufanya hivyo.

"Kifungu cha 11c cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 kinakataza mwanachama au kiongozi yeyote wa chama cha siasa kufanya kitendo chochote kinachodhihaki bendera ya chama kingine na adhabu ya kosa hilo ni faini isiyozidi Sh. 1,000,000 au kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote," anasema Jaji Mutungi.

**Kifungu cha 11c cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 kinakataza mwanachama au kiongozi yeyote wa chama cha siasa kufanya kitendo chochote kinachodhihaki bendera ya chama kingine na adhabu ya kosa hilo ni faini isiyozidi Sh. 1,000,000 au kifungo kisichozidi miezi sita au adhabu zote.**

Msajili anawaasa wanachama na mashabiki wote wa vyama vya siasa kuepuka na kujishusha na vitendo vyote vya uvunjifu wa sheria, kwa vile wakifanya hivyo watachukuliwa hatua za kisheria na chama kinachohujumiwa.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk Bashiru Ally, anawataka wanachama wa CCM kuheshimu alama za vyama vyote vya siasa nchini kwa sababu vimesajiliwa kisheria.

Anawataka kutochoma wala kubeza alama za vyama hivyo.

"CCM tusifanye mambo holela na uhuni huo katika siasa. Ni kosa kuparamia na kupaka rangi ofisi za vyama hivyo. ni kosa kisheria,' anasema.

Anawaambia wana-CCM hao kuwa wana wajibu wa kulinda uhuru wa vyama vingine vilivyosajiliwa kisheria, na kwamba kama CCM inafurahi na kuimba nyimbo zake, basi iache na wengine wafurahi na kuimba nyimbo zao, na pia kama wanaCCM wanapendeza kwa mavazi yao, waache wapinzani nao wapendeze kwenye sare zao.

Inavyoonekana si lazima kuchoma kadi, sare au bendera pale mwanasiasa anapohama kutoka chama kimoja kwenda kingine. Uchomaji huo hauna manufaa kwa mwanachama au kwa chama kilichochukua hatua hizo kwani kwa ujumla ni uharibifu.

Ufike wakati wanasiasa wabadilike na kuendesha siasa za kistaarabu kwa kutojenga na chuki. Wapo baadhi ya wanasiasa wamewahi hata kuwavisha mbwa bendera za vyama vya siasa wakati wakijua wazi kuwa kuheshimu alama za vyama vyote vya siasa ni jambo la muhimu ili kuepusha uhasama wa kisiasa.

Baadhi ya Watanzania wanahama vyama kila kukicha, sasa kwa mtindo huu watachoma kadi ngapi, sare ngapi na bendera ngapi? Kuna ubaya gani mtu kuhama chama kwenda kingine na kukabidhiwa kadi ya chama alichohamia bila kuharibu kile alichotoka.

Ni jambo jema Jaji Mutungi kukemea mtindo huu, ambao ni kama ulishazoeleka miongoni mwa wanasiasa na vyama.

# BARUA & MJADALA

## Kulikoni miongo bila umeme Msumi?

*Mhariri*

*NAPENDA kutumia nafasi hii kutoa masikitiko ya wakazi wa Mbezi Msumi jijini Dar es Salaam, tunaoishi maeneo ya Mchikichini.*

*Kabla ya yote napenda kupongeza Wizara ya Nishati, Wakala wa Umeme Vijijini na Tanesco kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini tunasikitika kwa watendaji wasiopenda kubadilika kuendana na kasi ya John Mgufuli ya kuwapatia wananchi wake maendeleo hasa kuwasha umeme Tanzania nzima.*

*Nizungumzie suala la umeme yapata miaka miwili baadhi ya wakazi wa Msumi walijaza fomu za kupatiwa umeme lakini hadi leo wanaambiwa nguzo hamna.*

*Ni jambo la aibu kwa Tanzania ya leo kusema nguzo hamna, majirani wa maeneo ya Mchikichini waliojenga hivi karibuni tayari umeme umeshawekwa. Tunapenda kujua ni nini ambacho hatujatimiza ili tupate umeme?*

*Waziri wa Nishati, ebu fuatilia watumishi wa eneo husika wasichafue wizara yako tunaimani serikali yako na imekiri kuwa umeme si jambo la kusubiri kwa miaka miwili*

***Joho Samwel***
***Mbezi Msumi, Dar es Salaam.***

## Tunahitaji wataalamu wa kukagua nyama

*Mhariri*

*NITOE kilio changu kuwa mimi ni mteja mkubwa wa nyama zinazouzwa kwenye maduka makubwa hivyo najihisi kuwa ni mwathirika wa tani nane za kitoweo cha nyama zilizoharibiwa, kama ilivyoelezwa kwenye gazeti lako la Jumatatu wiki hii.*

*Ni wazi kuwa nyama au vyakula vyenye sumu ni hatari kuliko tunavyoweza kufikiri. Hapa tupo kwenye hatari ya kupata magonjwa ya moyo, ini, saratani na figo. Kinachoniuma ni hiki wakaguzi wetu walikuwa wapi mpaka tukaachwa kula vyakula vyenye sumu?*

*Ni nani atatusaidia iwapo tumeathirika? Ninaomba serikali ichukue hatua maana vyakula vyenye sumu si kwamba tu vinatuathiri bali pia vinahatarisha hatma ya maisha yetu na watoto wetu wadogo ambao kwa tukio hilo tumewalisha sumu wakiwa wadogo. Tunashauri uagizaji nyama nje upigwe marufuku ikitokea kuna wenye vibali vya kuingiza nyama hizo zikaguliwe kikamilifu ili kunusuru maisha ya Watanzania.*

*Hata hivyo, serikali iweke mazingira wezeshi ili wanaotaka kuuza nyama za nguruwe na ng'ombe waweze kuuza zilizoandaliwa hapa nchini.*

***Galliard Mosses***
***Box 1575, Dar es Salaam.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Ni Afrika pekee vikongwe wanapogombea uongozi

**Na Salome Kitomari**

**UKIZISOMA** au kuzisikiliza hotuba za Mwenyekiti wa MO Foundation, MO Ibrahimu, ambaye amekuwa akitoa Tuzo ya Rais Bora wa Afrika baada ya kumaliza muda wa uongozi, ni ukweli usiofichika kuwa zina maudhui yanayoishi.

Zinaishi kama zilivyo hotuba za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ambazo kila ukizifuatilia zimejaa maudhui na mafundisho yanayotikisa kwenye uongozi wa si wa Tanzania pekee bali na Afrika kwa ujumla na hata mataifa mengi yanayoendelea.

Katika hotuba zake MO Ibrahim anasema Afrika ni bara la vijana kwa kuwa zaidi ya nusu ya idadi ya raia wake ni vijana wenye umri wa miaka 23, lakini ukiangalia umri wa marais wa nchi nyingi ni wazee wenye zaidi ya miaka 64

Anasema ni Afrika pekee ambako kuna marais ambao katika umri wa miaka 90 wanagombea urais kwa mara ya kwanza, tena kubwa baadhi yao wakiwa kwenye viti mwendo na hawawezi hata kusimama kupiga kura au wagonjwa wa kiharusi, lakini wanagombea urais.

Anatoa mfano wa Marekani yenye uchumi wenye thamani ya dola trilioni 15 hadi 16 huku Afrika yote uchumi wake ni chini ya dola trilioni moja, lakini Rais Mstaafu, Barrack Obama, aliingia madarakani akiwa na miaka 47 na muda wake ulipokwisha aliondoka, na hakuwa rais mdogo kwa kuwa Bill Clinton, alishika madaraka akiwa na miaka 43.

**Ni Afrika pekee ambako mstaafu bila hofu anaanza safari ya maisha ya kisiasa katika umri wa miaka 60 anaamka kugombea nafasi na kwa kutumia mbinu chafu kama fedha huingia madarakani hata Ikulu.**

MO anajiuliza kwanini nchi tajiri zenye misuli ya uchumi mkubwa, mitambo na nyukilia na ambazo sasa zinapanga kuishi angaza za juu zinakuwa na viongozi vijana, lakini kwa Afrika mtu anagombea uongozi akiwa na miaka 90? Anatuongoza kwenda wapi? Pengine kuelekea kaburini?

Anasema ni vyema vijana wakapewa nafasi kwenye uongozi na siyo wazee kuendelea kung'angania madaraka kwani zaidi wanapaswa kubaki kuwa washauri.

Kuna chanagmoto nyingi zinawakabili vijana na lazima zitatuliwe kwa kuwajumuisha kwenye madaraka, ni lazima kuwapa nafasi na kuwaamini kwa kuwa bado wana nguvu na ubongo unaofanyakazi kwa haraka zaidi badala ya kuendelea kujaza wazee.

Kwangu kauli hii ni madhubuti na inaishi na itaendelea kuwa hai kwa nchi zote za Afrika, Tanzania ikiwamo kutokana na mifano halisi tunayoiona kwamba watu wamefikia umri wa kustaafu au wanatakiwa kukubali kuwa washauri, lakini ndiyo kwanza wanakimbilia kushika madaraka.

Ni Afrika pekee ambako mstaafu bila hofu ananza safari ya maisha ya kisiasa katika umri wa miaka 60 anaamka kugombea nafasi na kwa kutumia mbinu chafu kama fedha huingia madarakani hata Ikulu

Ifikie wakati wazee hao wabaki kuwa washauri na wawe nyuma ya vijana walio na akili ambazo zimechangamka na zinazotaka mabadiliko ya kweli kuliko kuendelea kuongoza kwa mazoea.

Kwa kawaida ili kiongozi yoyote ashike madaraka fulani ni lazima jina lake lipitishwe na chama chake, na kwa kuwa siasa ndilo eneo la watu kukimbilia kwa kuwa kuna pumziko basi wengi hukimbilia huko na mwishowe ndiyo wale huishia kucheza na katiba ili waendelee kusalia madarakani.

Kwa Afrika Masharikí ina mifano ya viongozi ambao wamebadilisha katiba au kuchelewesha uchaguzi mkuu ili waendelee kuchota utajiri na kujilimbikizia mali huku wananchi wakiendelea kutaabika, kwa kuamini kuwa bila zao nchi zao haziwezi kuendelea jambo ambalo siyo kweli.

Mathalani, huko Rwanda, Burundi na Uganda, hatua hiyo iliyochukuliwa baada ya viongozi kumaliza muda wao. Wakuu hao walijenga mazingira ya kufanya mabadiliko ya katiba ili waendelee kusalia madarakani. Ipo mifano hai kama Congo ambako rais aliyemaliza muda wake Joseph Kabila, alitakiwa kuondoka Ikulu tangu mwaka 2016, lakini alichelewesha uchaguzi na kuanzisha mizengwe mingi hadi uchaguzi mkuu ulipofanyika Desemba mwaka jana tena ukichangiwa na shinikizo kubwa la jumuiya ya kimataifa.

Kwingine ni Zimbabwe ambako Robert Mugabe, licha ya kuheshimiwa na dunia na hasa Afrika kutokana na misimamo yake, lakini aliondolewa madarakani kwa aibu kwa kuwa alitaka kuugeuza urais kama mali ya familia yake.

Kwingine ni Togo ambako urais umegeuzwa kuwa mali ya familia kwamba anatoka baba anaingia mtoto, na ndicho kinachokaribia kufanyika Uganda kwamba atatoka baba ataingia mtoto ambaye ana nafasi kubwa ndani ya Jeshi la Uganda.Ifike mahali viongozi hawa waone aibu kwamba hawakuzaliwa peke yao kuongoza Afrika.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Hujuma nzito za mapato U/Taifa

INATOKA UK. 2

kurasa 95 na viambatanisho tisa, inaeleza katika ukurasa wa 29 na 30 kuhusu baadhi ya watendaji wakuu wa shirikisho wanavyohujumu mapato ya milangoni wakishirikiana na wadau wengine wa soka nchini.

Inaelezwa katika ukurasa wa 29 wa ripoti ya kamati hiyo kuwa: "Baadhi ya watendaji wakuu ndani ya TFF wanajihusisha na kuhujumu mapato kwa kuchapisha tiketi za ziada na kuziuza kwanza (zinauzwa kabla ya mauzo ya tiketi halali kufanyika)".

### POLISI, MABAUNSA

Ripoti ya kamati hiyo pia inabainisha kuwa baadhi ya askari polisi na mabaunsa wanaosimama kwenye mageti ya viwanja vya soka nchini wamekuwa wakijihusisha na hujuma za mapato kwa kuingiza kinyemela watu baada ya kupewa "kitu kidogo".

Ukurasa wa 34 wa ripoti hiyo unasomeka: "Licha ya kushirikiana na wahakiki tiketi, polisi huhujumu mapato kwa kuingiza bure watu uwanjani kwa kutumia magari yao na wakati mwingine kwa kutumia wadhifa wao baada ya kuchukua kitu kidogo.

"Mabaunsa nao hushiriki katika vitendo vya kuhujumu mapato kwa kuruhusu watu kuingia bure baada ya kuchukua kitu kidogo (rushwa)."

### MAKOMANDOO WA KLABU

Ripoti ya kamati hiyo pia inabainisha kuwa baadhi ya klabu zimekuwa na tabia ya ovyo ya kuweka milangoni wanachama wake maarufu makomandoo, ambao pia hujihusisha na hujuma dhidi ya mapato.

"Klabu hulazimisha kuwapo kwa watu wao wanaoitwa makomandoo milangoni kusimamia mapato, lakini watu hao hujihusisha na hujuma za mapato," inaelezwa katika ukurasa wa 35 wa ripoti ya kamati hiyo.

### WAPENDA BURE

Ripoti ya kamati hiyo pia inabainisha kuwapo kwa changamoto ya baadhi ya watu kuingia viwanjani bila kulipia tiketi wakitumia umaarufu au vyeo vyao.

Ukurasa wa 35 wa ripoti hiyo unasomeka: "Watu wengi hupenda kuingia bure uwanjani, hasa polisi, askari magereza, viongozi wa zamani wa mpira wa miguu, viongozi wa siasa, viongozi wa serikali, makocha wa sasa na wa zamani, wachezaji wa zamani na wanamuziki maarufu. Hufanya hivyo kwa kutumia umaarufu au vyeo vyao."

### UDANGANYIFU VITABU

Kamati hiyo pia inaeleza kuwa kutokana na udhaifu katika mfumo wa uandaaji na uuzaji wa tiketi, baadhi ya wawakilishi wa klabu, TFF, serikali na wamiliki wa viwanja, wamekuwa wakishiriki katika kuhujumu mapato kwa kutangaza mapato kidogo hata kama mechi imeingiza kiasi kikubwa cha fedha, baada ya kuwa wamegawana sehemu ya mapato ya mlangoni ya mechi husika.

Aliyekuwa Rais wa TFF kipindi hicho, Leodegar Tenga, aliunda kamati hiyo iliyokuwa na wajumbe 'wazito' akiwamo aliyekuwa Kamishna Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Suleimani Kova na mwenyekiti wa zamani wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Kanali (mstaafu) Iddi Kipingu, ili kuchunguza mwenendo wa shirikisho hilo kimapato na matumizi.

### MHASIBU WA UWANJA

Mwaka 2014, Nipashe ilitoa ripoti iliyofichua wizara yenye dhamana ya michezo ilivyokuwa inachukua na kusafirisha fedha kwenye viroba kutoka Ofisi za TFF zilizoko Karume jijini.

Fedha hizo ni zile zitokanazo na mgao wa asilimia 15 ya mapato ya kila mechi ya soka inayochezwa kwenye Uwanja Taifa.

Nipashe ilibaini wizara hiyo ilajiri mhasibu maalum kwa ajili ya kukusanya mapato ya uwanja huo, huku kukiwa na shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana na usafirishaji wa mamilioni hayo ya shilingi kufanyika kienyeji bila mhasibu mwenyewe kuwa na ulinzi wa vyombo vya dola.

Baada ya Nipashe kuchapisha ripoti hiyo ya kiuchunguzi, wabunge waliitaka wizara kulieleza Bunge sababu za kuwa na utaratibu huo mbovu wa malipo ya fedha serikali na kubainisha mapato yote ya matumizi ya Uwanja wa Taifa tangu ulipojengwa 2007.

Hata hivyo, aliyekuwa Naibu Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Amos Makala, alipopewa nafasi ya kujibu hoja za wabunge, alisema hawezi kutoa maelezo kwa kuwa hafanyi kazi kupitia taarifa zinazoandikwa na magazeti.

### KAULI YA TFF

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Cliford Ndimbo, Ofisa Habari wa TFF, kuhusu uuzaji wa tiketi katika viwanja vya mikoani na Dar es Salaam, ilieleza kuwa jukumu hilo sasa linasimamiwa na wamiliki wa viwanja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Taarifa hiyo ya Ndimbo ilibainisha kuwa tiketi zote ambazo zinakatwa kwa michezo ya mikoani, zinasimamiwa na Ofisi ya Rais - Tamisemi na kwa viwanja vya Dar es Salaam, usimamizi wake unafanywa na wamiliki wa viwanja.

"TFF katika zoezi hilo imekuwa ikitaja bei ya tiketi na madaraja yake na kuacha kazi kwa mamlaka husika za Tamisemi na uwanja kupanga namna ya ukusanyaji wa mapato kupitia tiketi," Ndimbo alieleza katika taarifa yake hiyo.

### MAPATO MIL. 700/-

Taarifa za TFF kuhusu mapato yaliyokusanywa msimu wa 2013/14 wa Ligi Kuu Tanzania Bara zinaonyesha serikali ilipata mgao wa Sh. milioni 755.9 kutokana na mapato ya milangoni kwenye viwanja vyote 10 vilivyotumika.

Kati yake, Mamlaka ya Mapato (TRA) ilipata Sh. milioni 422.25 (asilimia 18 ya mapato ya jumla ya mechi zote) wakati wizara inayosimamia michezo ilipata Sh. milioni 333.65 (asilimia 15 baada ya TRA kukata kiwango chake kwenye makusanyo ya jumla).

Viwanja vilivyotumika kwenye ligi msimu huo ni Uwanja wa Taifa, Manungu Complex, Azam Complex, Mabatini, Jamhuri Morogoro, Mkwakwani, Sokoine, Ali Hassan Mwinyi, Kaitaba na Sheikh Amri Abeid. Katika msimu huo, Uwanja wa Taifa ambao ulitumika kwa mechi zilizozihusu timu za Simba na Yanga, TRA ilikusanya Sh. milioni 422.25.

Mgao wa jumla kwa wamiliki wa viwanja vinavyotumika Ligi Kuu msimu huo ulikuwa Sh. milioni 474.77. Wamiliki wa Uwanja wa Taifa (serikali kupitia wizara yenye dhamana ya michezo) walipata mgao wa Sh. milioni 333.65, ikiwa ni takribani theluthi ya bajeti ya maendeleo ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/15.

### USALAMA VIWANJANI

Katika hotuba yake ya juzi, Rais Magufuli pia alihoji kuhusu usalama wa mashabiki wanaokwenda kutazama mechi za soka nchini.

Ripoti iliyotolewa na Nipashe mwaka 2017 kuhusu usalama wa viwanja vya soka nchini, ilibainisha kuwa hakuna hata uwanja mmoja nchini ambao unakidhi masharti yote 89 ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) kuhusu usalama wa viwanja vya soka.

Mathalani, Uwanja wa Taifa licha ya kuwa uwanja mkubwa zaidi nchini na ujenzi wake kugharimu Sh. bilioni 56, nao haukidhi masharti ya usalama ya FIFA kutokana na kutokuwa na eneo na njia maalum kwa ajili ya waandishi wa habari.

Aliyekuwa Ofisa Usalama wa Fifa nchini, Jonas Mahanga, alisema uwanja huo pia hauna alama zinazoongoza watu kwenda kwenye majukwaa na tahadhari ya vyumba na maeneo hatarishi, ikiwamo mitambo ya umeme.

Mahanga alisema viwanja vyote nchini vinapaswa kuwa na vituo vya maofisa usalama kuhifadhi silaha kwa vile Kanuni za Usalama za FIFA zinazuia polisi na maofisa usalama kuingia na silaha uwanjani.

"Hapa Tanzania tunakiuka kanuni hii. Askari wanatakiwa kuingia na silaha pale tu patakapokuwa na dharura, ndiyo maana zinapaswa kuhifadhiwa kwenye kituo cha usalama cha uwanja au kituo cha polisi au jeshi kilicho karibu na uwanja husika," alisema.

Akizungumzia changamoto zinazoukabili Uwanja wa Taifa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), Boniface Wambura, alisema serikali inapaswa kutupiwa lawama kutokana na kupuuza ushauri wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (Taswa).

"Wakati mchakato wa ujenzi wa Uwanja wa Taifa unaanza, nilikuwa Rais wa Taswa na niliikabili Wizara ya Michezo kuhusu sehemu ya waandishi wa habari, wakanihakikishia kuwa kila kitu kiko sawa, kwani uwanja unaojengwa ni wa kiwango cha Olimpiki. Lakini ulipofunguliwa, hali ilikuwa tofauti.

"Kumbuka, tatizo hili halikuwa kwa Taswa tu, kwani TFF walilazimika kutoa watu wao kurekebisha vipimo vya uwanja pamoja na magoli. Pia AT (Chama cha Riadha Tanzania) na TOC (Kamati ya Olimpiki Tanzania) waliikataa 'tartan' ya kukimbilia iliyokuwa imewekwa awali, ikabidi ing'olewe iwekwe nyingine," Wambura alisema.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Uwanja wa Taifa unashika nafasi ya 12 kwenye orodha ya viwanja vikubwa zaidi barani Afrika, ukiwa na uwezo wa kuketisha mashabiki 57,558, kabla ya kujengwa kwa Uwanja wa Soccer City, Afrika Kusini mwaka 2010, Uwanja wa Taifa ndio uliokuwa uwanja mkubwa zaidi barani Afrika.

Ushawishi wa marais wastaafu Benjamin Mkapa na Dk. Jakaya Kikwete kwa mataifa ya nje, ndio ulioifanya serikali ya China ikubali kushirikiana na serikali ya Tanzania kujenga Uwanja wa Taifa. Uwanja huo ulijengwa 2007 kwa gharama ya Sh. bilioni 56 (serikali ya Tanzania ilichangia Sh. bilioni 25).

# Takukuru yamsaka mmiliki

INATOKA UK. 2

Tegeta jijini.

Alidai mtu huyo si mtuhumiwa wa kwanza mali zake kutolewa uamuzi wa kutaifishwa, akikumbusha kesi namba CC.92/2016 ambayo mshtakiwa alikutwa na hatia na mali zake -- magari manne na nyumba saba zenye thamani ya Sh. milioni 486 zote zilirejeshwa serikalini.

Aliwataka watumishi wote wa umma na wananchi kwa ujumla kutojihusisha na vitendo vya rushwa kwa namna yoyote ile.

"Nina uhakika ukijihusisha na vitendo vya rushwa, hautakuwa umepata, bali utakuwa umepatikana. Na yeyote atakayejihusisha na vitendo vya rushwa, atakumbana na mkono wa Takukuru ikiwamo kufungwa jela na kufilisiwa mali zote alizopata kwa njia ya rushwa," Athumani alionya.

### BILIONI 14 ZAOKOLEWA

Katika hatua nyingine, bosi huyo wa Takukuru alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi sasa, taasisi hiyo imefanikiwa kurejesha Sh. bilioni 14.7, kutaifisha nyumba saba na magari manne kutoka kwa mafisadi.

Vilevile, alisema wameweka zuio la mali zikiwamo akaunti za kifedha za zaidi ya Sh. bilioni 20, nyumba 26, viwanja 47, magari 61 na mashamba 13.

Aliongeza kuwa Takukuru ina mamlaka hiyo kupitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007, Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu Sura ya 256 ya Mwaka 2002 na Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984.

### HALI YA 'MAHEKALU'

Waandishi wa habari walipata fursa ya kushuhudia nyumba ya kisasa iliyoko Tegeta jijini inayodaiwa kumilikiwa na Magreth ambayo kwa sasa hakuna mtu anayeishi.

Nyumba hiyo ina uwanja wa mpira wa mikono uliojengwa na kuwekwa wigo wa wavu pamoja na bwawa la kuogelea.

Mfanyakazi wa bustani katika nyumba hiyo aliyejitambulisha kuwa ni Hamis Kilindo, alidai amekuwa akifanya kazi katika nyumba hiyo kwa mwaka mmoja na nusu na hajawahi kuona mtu anayeishi katika nyumba hiyo zaidi ya mlinzi anayelinda getini.

# Zitto amjibu Msajili Vyama

INATOKA UK. 3

Akijibu hoja ya kutowasilisha ripoti ya ukaguzi wa hesabu za chama hicho za mwaka wa fedha 2013/2014, Zitto alisema wajibu wa chama cha siasa ni kuwasilisha hesabu zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kwamba katika kipindi hicho chama chake kilishaziwasilisha.

"Tuhuma hizi hazina ukweli wowote kwa sababu wajibu wa chama cha siasa chochote ni kuwasilisha hesabu zake kwa CAG. Hesabu za mwaka 2013/2014 ziliwasilishwa kwa CAG isipokuwa kilichotokea ni kwamba chama kilianzishwa kwa kupata usajili wa kudumu Mei 5, 2014 miezi miwili kabla ya mwaka fedha kuisha Juni 30,2014," alisema Zitto na kuongeza

"Kwa kutumia kanuni za kimataifa za kihasibu na kwa ushauri wa CAG, chama chetu kilielezwa kwamba kinaweza kuunganisha hesabu za mwaka 2013/2014 na za 2014/2015 katika ripoti moja. Na hili ni jambo la kawaida katika kanuni za uhasibu kwa kuwa inaruhusu kuunganisha hadi miezi 18 na kwa kuunganisha huko, ACT-Wazalendo ilikuwa na miezi 14 tu," alisema Zitto.

Alisema kabla ya kuamua kuunganisha hesabu hizo, chama hicho kilimwandikia barua Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye alijibu na kuridhia hesabu

INAENDELEA UK. 26

HABARI KITAIFA

# Ongezeko la mazao ya nyuki

Na George Tarimo, DODOMA

UZALISHAJI wa mazao ya nyuki katika mashamba ya serikali ya ufugaji nyuki yaliyopo mikoa ya Dodoma na Singida unatarajia kuongezeka hadi kufikia zaidi ya tani tisa za asali ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Ni shughuli ya uvunaji wa mazao ya nyuki katika mashamba ya serikali yaliyopo wilayani Manyoni mkoani Singida, na Kondoa mkoani Dodoma, ambapo Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kati, Methew Kiondo, alisema miaka iliyopita mavuno ya mazao ya nyuki yalikuwa ndoo 10 hadi 20, lakini mwaka huu uzalishaji umeongezeka maradufu.

Kiondo alisema ufanisi huo umetokana na mapinduzi yaliyofanywa katika sekta ya ufugaji nyuki kwenye mashamba hayo yaliyopo katika wilaya hizo, ambapo jitihada zaidi zimeimarishwa kwenye usimamizi wa karibu wa makundi ya nyuki.

"Mwaka huu hasa kituo cha Manyoni tunatarajia kupata tani sita hadi saba na kituo cha Kondoa tunaweza kupata tani mbili," alisema Kiondo.

Uwapo wa mashamba hayo ya serikali unawanufaisha wananchi kwa kuwapatia ajira na elimu ya utengenezaji wa mizinga ya kisasa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki.

Abdala Ali Bali, mkazi wa Kijiji cha Mialo Dodoma, alisema miradi hiyo itawasaidia sana kupata maendeleo kwa mfano wananchi wameanza kutengeneza barabara, kijiji kupata asilimia ya fedha zake na kutunza mazingira.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wafugaji Nyuki Tanzania (TAPEDO), Rodia Issa, ambaye pia ni mnufaika wa shughuli za ufugaji na uzalishaji wa mazao ya nyuki wilayani Kondoa, alieleza changamoto ya upatikanaji wa vifungashio na gharama kubwa ya mitambo ya kuchakata mazao ya nyuki.

**Mwaka huu hasa kituo cha Manyoni tunatarajia kupata tani sita hadi saba na kituo cha Kondoa tunaweza kupata tani mbili.**

# Uamuzi mgumu wa DC kufuta kijiji

Na Magreth Magosso, KIGOMA

MKUU wa Wilaya ya Kasulu mkoani hapo, Kanali Simon Anange, amefanya uamuzi mgumu wa kuvunja kijiji cha Nyakafyeke na kukirudisha katika kijiji mama cha Rungwe mpya kutokana na kijiji hicho kukosa uongozi kwa miaka sita.

Hali hiyo imetokana na mgogoro sugu wa mpaka kati ya vijiji hivyo vilivyomo katika Kata ya Rungwe mpya, ambapo tangu kianzishwe Kijiji cha Nyakafyeke mwaka 2014 hakijapata viongozi kutokana na kushindwa kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014.

**Wananchi msilazimishe kuanzisha vijiji bila ridhaa ya mkurugenzi ambaye ana mamlaka ya rasilimali watu wa kuendesha shughuli za kuimarisha kijiji.**

Uchaguzi huo ulishindikana kutokana na ugomvi wa mpaka, ambapo Kanali Anange alisema hawezi kuishi na raia wasio na kiongozi katika wilaya hiyo.

Alisema katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa mwaka huu, uchaguzi utafanyika kwa kijiji kimoja cha Rungwe mpya, na kwamba Nyakafyeke kikibaki kama kitongoji, hivyo na kuwataka kukaa upya na kuweka makubaliano, ili watume maombi ya kuanzishwa kwa kijiji hicho kwa kufuata utaratibu.

"Wananchi msilazimishe kuanzisha vijiji bila ridhaa ya mkurugenzi ambaye ana mamlaka ya rasilimali watu wa kuendesha shughuli za kuimarisha kijiji kuanzia uchaguzi na mengine," alisisitiza Kanali Anange.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Godfrey Kasekenya, alisema kijiji cha Nyakafyeke kilianzishwa pasipo makubaliano mazuri ya wananchi, jambo ambalo lilisababisha wananchi kugomea uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014, hivyo kijiji hicho kutokuwa na uongozi hadi kilipovunjwa.



Vijana wakivua samaki kwenye mitambo ya kuzalisha maji Ruvu Chini mkoani Pwani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tume ya Nguvu za Atomiki kuboresha uchimbaji urani

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), inafanya warsha na wadau mbalimbali kwa lengo la kujadiliana namna ya kuboresha sheria na kanuni mbalimbali kwenye uchimbaji wa madini ya urani hapa nchini.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Tume ya Nguvu ya Atomiki, Peter Ngamilo, ilieleza kuwa wadau kutoka Wizara ya Madini, Tume ya Madini, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Maliasili na Utalii na Baraza la Mazingira nchini (NEMC), kwa pamoja wanajadiliana namna ya kuboresha sheria na taratibu za uchimbaji wa madini yenye mionzi.

Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Teknolojia na Huduma za Ufundi wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Dennis Mwalongo, amesema kuwa wadau kwa pamoja wataweza kusaidia kuboresha kanuni za uchimbaji wa madini yenye mionzi kwa lengo la kuondoa mwingiliano wa sheria hizo katika sekta ya madini.

"Majadiliano haya yatatuwezesha kutoka na kanuni ambazo zitasaidia kwa namna moja ama nyingine katika kuweka mfumo mzuri utakaowezesha uchimbaji madini yenye mionzi kuwa katika utaratibu mzuri na usio na mwingiliano kwenye sekta ya madini na mazingira kwa ujumla," alisema Mwalongo.

Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Migodi na Mazingira wa Tume ya Madini, Dk. Abdul Rahaman Mwanga, ameeleza kuwa wanatarajia kupata utaratibu na mfumo mzuri wa usimamiaji wa madini yatokanayo na mionzi nchini.

Alisema kuwa sheria zipo, lakini kumekuwa na mwingiliano wa sheria, kwa kukaa pamoja wadau watawezesha kuimarisha taratibu za madini na ambazo zimeboreshwa zitasaidia katika usalama wa mazingira na afya kwa viumbe mbalimbali vinavyozunguka maeneo ya uchimbaji wa madini ya urani.

"Tuna imani kuwa taratibu tutaziweka sawa ili kuwezesha uchimbaji wa madini ya urani hapa nchini na matarajio yetu kuwa madini hayo yatakapoanza kuchimbwa hakutakuwa tena na mwingiliano wowote," Mwanga alisema.

Pia ameeleza kuwa sheria na kanuni hizo na uboreshaji wake utakapokamilika kurekebishwa kutawezesha utoaji bora wa huduma kwa wawekezaji ambao wataamua kuwekeza katika uchimbaji wa madini ya urani hapa nchini.

Naye mshiriki mwingine kwenye warsha hiyo, Dk. Justin Ngaile, alisema mfumo mzuri wa usimamizi wa madini ya urani utawekwa jambo ambalo litasaidia kurahisisha uwekezaji mkubwa nchini.

Umoja wa Ulaya ndio mdhamini katika warsha hiyo na kupitia wataalamu wake wanasaidia uboreshaji wa sheria na kanuni mbalimbali za uchimbaji wa madini yenye mionzi ambazo zimeingiliana na uchimbaji wa madini na masuala ya mazingira.

Baadhi ya maeneo nchini yanayopatikana madini ya urani ni pamoja na Bahi mkoani Dodoma na Mkuju mkoani Ruvuma.

# Wataalamu waipa neno serikali dawa za kulevya

**Na Dege Masoli,** TANGA

WATAALAMU wa kutibu watumiaji dawa za kulevya mkoani hapo, wamesema njia zinazotumika kushughulikia tatizo la matumizi ya dawa hizo nchini ni dhaifu na kunahitajika nguvu za ziada kukabiliana na janga hilo.

Katibu wa nyumba za kutibu watumiaji wa dawa za kulevya ya Tanga Drugs Free Sober House iliyopo Duga jijini hapa, Bakari Abeid, aliiambia Nipashe kuwa nguvu zinazotumika katika kukabiliana na janga hilo ni ndogo na matumizi ya dawa hizo bado ni makubwa.

Abeid alieleza kuwa licha ya serikali kupiga vita matumizi ya dawa hizo, lakini hali imeendelea kuwa changamoto kutokana na njia zinazotumika za kutowabana waingiziaji na wauzaji wa dawa hizo na badala yake wanaobanwa ni watumiaji mitaani.

**licha ya serikali kupiga vita matumizi ya dawa hizo, lakini hali imeendelea kuwa changamoto kutokana na njia zinazotumika za kutowabana waingiziaji na wauzaji wa dawa hizo na badala yake wanaobanwa ni watumiaji**

Aliiomba serikali na jamii kutumia nguvu ya ziada kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Mratibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Gift Of Hope, Said Bandawe, alisema bado kuna changamoto kwa sababu watu wameacha kutumia dawa kali aina ya heroin na cocain na kuhamia kwenye matumizi ya bangi, mirungi na dawa halali zinazopatikana katika maduka ya dawa kama Tramadol na Valium.

Bandawe alieleza mkakati wao katika kupambana na janga hilo ni kuielimisha jamii hasa vijana kwa kuwajengea uwezo wa kutambua athari za matumizi ya dawa hizo na namna wanavyoweza kujiepusha nazo.

Hata hivyo Bandawe aliikumbusha serikali na jamii juu ya umuhimu wa kuzisaidia nyumba zinazojihusisha na malezi ya waathirika (Sober House) kupata mahitaji mbalimbali na kuhakikisha watumiaji hao wanaingia moja kwa moja kwenye tiba.

Aidha, aliiomba serikali iharakishe upatikanaji wa dawa ya Methorol katika nyumba za Sober House mkoani Tanga, ambayo inasaidia kupunguza hamu ya kutumia heroin na dawa nyingine ili watumiaji hao wakose hamu pamoja na kurejesha kwa haraka utimamu kwa waathirika na dawa hizo.

Naye Abdalah Issa aliyezungumza na gazeti hili kwa niaba ya waathirika wa dawa hizo kutoka kituo cha Caurage on Recover Foundation kilichopo Sahare jijini hapo, alisema kuwa wanaendelea kuhakikisha wanawasaidia vijana wenzao walioathirika na matumizi ya dawa hizo kwa kuwatoa katika utumwa na kuwarudisha katika utimamu.



Baadhi ya wauguzi na wakunga wabobezi wakiwa kwenye kongamano la siku moja juzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam, kuhusu sheria na kanuni za kazi kwa wauguzi na wakunga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wauguzi wafundwa kanuni za kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAUGUZI na wakunga Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wametakiwa kuzingatia sheria na kanuni za kazi wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa leo na Ofisa Muuguzi wa Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC), Gustav Moyo, kwenye kongamano la siku moja linalofanyika katika hospitali hiyo.

Moyo aliwataka wauguzi kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia taaluma ya uuguzi na ukunga inayoitwa "The Nursing and Midwifery Act. 2010" pamoja na kanuni zake.

Pia, aliwataka wauguzi na wakunga kutowatelekeza wagonjwa wanapohitaji huduma kwa kuwa kumtelekeza mgonjwa ni kosa kwa mujibu wa sheria, hivyo aliwataka kuzingatia sheria na kanuni za kazi ili kuboresha huduma mahali pa kazi.

"Wauguzi na wakunga mnapaswa kuzingatia upendo na huruma kwa wagonjwa, ndugu na jamaa wa wagonjwa. Jambo muhimu mnatakiwa kuboresha mawasiliano na kuzingatia maadili na kuwaona ndugu wa wagonjwa ni wadau," alisema Moyo.

Naye Happy Masenga katika kongamano hilo alisisitiza umuhimu wa wauguzi na wakunga kujiendeleza katika mafunzo mbalimbali ili kuendana na sayansi na teknolojia wakati wa kutoa huduma.

Katika mafunzo hayo pia walifundishwa jinsi ya kujaza kitabu maalamu (Log Book) ambacho kinasaidia upatikanaji wa leseni kwa wauguzi.

# Wakulima sasa waona fursa NHIF

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

JUMLA ya wakulima 339 wa tumbaku na pamba mkoani Shinyanga wamejiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) tangu kuzinduliwa mwaka jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama.

Meneja wa mfuko huo Mkoa wa Shinyanga, Iman Emmanuel, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

"Mfuko umetambua jitihada za wakulima katika kujipatia kipato kupitia kilimo na kuliletea taifa maendeleo ya kiuchumi kwa wakulima kupitia katika vyama vyao vya ushirika wa mazao kwa lengo la kuongeza tija katika shughuli zao za kilimo," alisema na kuongeza:

"Mfuko unatumia fursa hii ya kuwafikia wakulima katika vyama vyao vya msingi kwa kuwapatia bima ya afya kwa utaratibu wa ushirika."

Emmanuel alisema kuwa Chama cha Wakulima wa Tumbaku (KACU) wamepatiwa elimu kwa njia mbili tofauti na njia ya kwanza ni uhamasishaji ambao ulifanyika kwenye maghala ya kuhifadhia tumbaku kipindi cha mavuno wanapokuwa wakisubiri kuuza.

Alisema njia ya pili waliyotumia kufanya mikutano ya hadhara na kuonana na viongozi wa vyama vya msingi (AMCO's) na wakulima waliokwishajiunga waliendelea kuhamasishwa zaidi kupatiwa elimu.

Aliongeza kuwa kwa upande wa Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (Shirecu) walikutana nao kwenye mkutano mkuu wa chama hicho kutoa elimu na kuhamasisha.

Mwenyekiti wa chama kikuu cha ushirika wilayani Kahama, Emanuel Cherehani, alisema matibabu ni gharama sana, hivyo aliwataka wakulima wa tumbaku kushirikiana na serikali kutunza afya kwa kujiunga na NHIF kwa gharama ya 76,800, kwa mtu mzima na watoto kwa 54,000.

Mrajisi wa vyama vya ushirika nchini, Tito Haule, aliwasisitiza wakulima kujiunga na mfuko huo kutokana na wengi wao mkoani Shinyanga kutoona umuhimu wa kujiunga kwenye bima kwa madai kuwa gharama za kujiunga ni kubwa.

"Ninawaomba wakulima mjiunge msiogope gharama ya shilingi 76,800 kwani utakuwa na uhakika wakupata matibabu mwaka mzima na kuruhusiwa hospitali zote kupata matibabu," alisema Haule.

Mwenyekiti wa Shirecu, Richard Luhende, alisema wamekuwa wakihamasisha wakulima wa pamba waliopo kwenye vyama vya msingi vya ushirika zaidi ya 300 kujiunga na mfuko huo, na kwamba baadhi wameanza kuitikia wito.

## Tahadhari yatolewa mifugo kuliwa na wanyamapori

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

BODI ya Ushauri wa Masuala ya Maliasili wilayani Longido, imesema matukio mengi ya mifugo kuuawa na wanyamapori inatokea wakati ikichungwa na watoto wadogo.

Imewataka wachungaji wa mifugo wawe watu wazima ambao wataweza kumudu kuilinda mifugo hiyo wakati ikiwa malishoni.

Meneja wa Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii ya Enduiment, (WMA), Peter Millanga, alisema hayo katika kikao cha ushauri ambacho pamoja na mambo mengine kilizungumzia migongano baina ya shughuli za kibinadamu, wanyamapori na mifugo.

Alieleza malalamiko ni mengi juu ya mifugo inayoliwa na wanyama wakali, lakini tafiti zilizofanyiwa na bodi hii imebaini mifugo hiyo huliwa malishoni kutokana na wachungaji kutokidhi vigezo.

"Wanaochunga mifugo ni watoto wadogo, wakati mwingine wanashindwa kumudu mifugo hiyo na hupotea na kubaki malishoni, hivyo ni rahisi wanyama wakali kula mifugo hiyo inayosalia malishoni," alidai.

Aidha, aliwaomba viongozi mbalimbali wilayani hapa, kuhakikisha wanawafuatilia wazazi ambao hawajawaandikisha watoto hao shule na badala yake wamewapa kazi ya kuchunga mifugo.

"Lakini pia ni wakati wenu kama viongozi kuchukulia jambo hili la watoto kuchungishwa mifugo hatua kali za kisheria," alisema.

Alidai wanyama wakali kama simba, fisi, chui na mbwa mwitu ni ambao wapo katika hifadhi ya jumuiya hiyo yenye kata nne ambazo ni Kata ya Olmolog, Sinya, Tingatinga na Kamwanga zinazounda Tarafa ya Enduiment.

Lakini katika utafiti zilizofanywa zimebaini simba zaidi ya 11 wameuawa kuanzia mwaka 2007-2018 na wananchi wenye hasira kali wakiongozwa na Kijiji cha Olmolog, Lerang'wa, Ngereyani na Kitendeni.

Hali hii imesababisha wananchi ndani ya hifadhi kuonekana kujali mifugo yao kuliko nyara za serikali pasipo kufikiria kupitia wanyamapori hao, serikali inajipatia mapato ambayo ndio haya hufanya maendeleo ndani ya wilaya.

"Wananchi hawana uvumilivu, inatokea mfugo au binadamu ameliwa/kuuawa na mnyama mfano simba, wanatupa taarifa, lakini ukifika eneo hilo ushahidi unakuwa hakuna wakati mwingine wananchi hao humchukua ule mfugo aliyeliwa na wao wanamla, hii ni hatari lazima tukute ushahidi ili tuweze kulipa fidia," alidai.

Mwenyekiti wa WMA Enduiment, Parsanga Lendapa, alisema anasikitishwa na takwimu zilizotolewa ya kuwa asilimia 82 ya wakazi ndani ya jumuiya hiyo wanaosema hawanufaiki na wanyamapori wakali ndani ya jamii bali wanufaika ni serikali kuu.

# Kamati ya Bunge yamweka 'kitimoto' naibu waziri maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Kilimo Mifugo na Maji imeitaka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kutoa maelezo kwake kwa maandishi ni kwa nini baadhi ya vifaa vya kutekeleza mradi wa maji wa shilingi bilioni 520 vimekwama bandarini kwa miezi mitatu kwa kukosa msamaha wa kodi.

Aidha, kamati hiyo imeitaka Kampuni ya Sinohydro Corporation ya China, kuiandikia kamati hiyo iwapo itaweza kutekeleza kwa wakati zabuni tatu za mradi ambao imepewa kwa wakati mmoja.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya visima vya uzalishaji maji ambavyo vitachimbwa pamoja na bomba kubwa la kusafirisha maji na upanuzi wa matandao wa majisafi.

Kazi nyingine waliyopewa ni pamoja na ujenzi wa mitambo ya kusafisha maji eneo la Miadwe, Olgilai na Ngarendolu pamoja na upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya mifumo ya majisafi na maji taka katikati ya Jiji la Arusha.

Agizo hilo lilitolewa juzi na kamati hiyo wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara yao ya siku nne jijini hapa ya kukagua miradi ya kilimo, mifugo na maji.

> **Naibu Katibu Mkuu tunataka utuandikie kwa maandishi kwa nini mpaka sasa vifaa vimekaa bandarini kwa miezi mitatu wakati mnajua kabisa fedha hizi Sh. bilioni 520 ni za mkopo.**

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahamoud Mgimwa, alimwagiza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Emmanuel Kalobelo, kutoa maelezo kwa maandishi ni kwa nini hawashughulikii vifaa, hivyo kusamehewa kodi licha ya makandarasi kuandika barua ya kuomba msamaha huo.

"Naibu Katibu Mkuu tunataka utuandikie kwa maandishi kwa nini mpaka sasa vifaa vimekaa bandarini kwa miezi mitatu wakati mnajua kabisa fedha hizi Sh. bilioni 520 ni za mkopo na marejesho yake yanatakiwa kuanza kulipwa mwaka 2021, mnapokalia barua za makandarasi bila kuzifanyia kazi mnategemea nini? Je, mradi ukichelewa kukamilika kwa sababu ya kutokuwa na vifaa ni nani atalazimika kumlipa mkandarasi fidia," alihoji.

Licha ya wizara hiyo, kamati hiyo pia ilimtaka mkandarasi wa Kampuni ya Sinohydro Corporation ltd kueleza iwapo kweli itaweza kutekeleza miradi yote mitatu ndani ya muda wa mkataba kwa sababu kamati hiyo ilipata hofu kutokana na ukubwa wa miradi hiyo.

Akichangia hoja hiyo Justine Monko (Singida Kaskazini) alisema kuna hatari ya miradi hiyo mitatu kutotekelezeka kwa wakati kutokana na baadhi ya vifaa kukwama bandarini kwa muda mrefu.

Awali Meneja wa mradi wa uchimbaji wa mabwawa 18 ya kutibu majitaka kutoka kampuni ya China Civil Engineering Construction Cooperation (CCCECC), Ning Yun Fong, alisema mradi huo kwa mabwawa ya maji taka, umetekelezeka kwa asilimia 60, unasuasua kutokana na vifaa kukwama bandarini kutokana na kusubiri msamaha wa kodi.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Kalobelo, alisema baadhi ya barua za makandarasi za kuomba kupewa msamaha wa kodi zimeshaanza kufanyiwa kazi na kwamba nyingine zinakwama kutokana na kutokidhi vigezo vya msamaha wa kodi.

Mikataba ya ujenzi wa mradi huo wa Sh. bilioni 520 kwa makandarasi wote ilisainiwa mwaka jana na baadhi ya miradi itakabidhiwa kuanzia Mei, mwaka huu na mingine mwakani.



Mama Maria Nyerere (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na mgeni wake, mjane wa Waziri Mkuu wa zamani, Edward Sokoine, Mama Napono Sokoine na wasaidizi wao, alipomtembelea katika makazi yake Msasani jijini Dar es Salaam, jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waomba serikali kutatua mgogoro mpaka

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAKAZI wa Kata ya Engikaret, Tarafa ya Longido, wameiomba serikali kuingilia kati mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Longido, Monduli na Arumeru.

Diwani wa Kata hiyo, Sarun Kispan, alisema kata yake ipo mpakani na Wilaya ya Arumeru na Monduli na kwamba kuna mgogoro unaendelea kati ya wilaya hizo.

"Ndani ya kata yangu kuna kijiji kinaitwa Kiseriani kimepakana na kijiji cha Mfereji Wilaya ya Monduli pamoja na Donyosambu wilayani Arumeru, tunafahamu siku chache zilizopita kijiji cha Mfereji na Donyosambu walichomeana maboma, hatutaki hii hali ifike kwetu," alidai.


Alisema kumekuwa na tabia ya majirani zao wa wilaya hizo kujiongezea maeneo ndani ya wilaya, hali ambayo ni uchokozi kwa wakazi wa kata yake, hivyo wanaiomba serikali ya wilaya hii kuingilia kati.

"Sisi hatutaki mgogoro na hivi vijiji, tu naomba serikali ifike hapa kuweka wazi mipaka halali ya Engikaret na hizo wilaya kwa kufanya hivyo itasaidia kuepusha mikwaruzano," aliomba.

Lakini pia alisema hawana imani kabisa na vijiji hivyo, kwa kuwa kilichotokea baada ya hao kuchomeana maboma ni hatari kwa jamii, hivyo na wao wanaishi kwa wasiwasi wakihofia hali hiyo inaweza kuwatokea muda wowote.

"Watu wale walichomeana maboma, tunaomba isifike kwetu wasije tuchomea ndani au kuchoma taasisi mfano shule na hospitali, serikali tunahitaji tamko lenu juu ya hili jambo," alieleza.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema anafahamu tatizo hilo la mipaka kati ya wilaya hizo na Longido, lakini alishamweleza waziri mwenye dhamana na kumwomba afike kutoa tamko juu ya mgogoro huo.





# Makundi ya mifugo yafanya uharibifu mashamba mahindi

Na Godfrey Mushi, MOSHI

MAKUNDI ya mifugo kutoka wilaya za jirani za Simanjiro na Mwanga yamevamia mashamba ya wakulima katika kijiji cha Mikocheni kilichoko kata ya Arusha Chini, Moshi Vijijini na kuharibu mazao ya chakula.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mikocheni na Masaini, Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo (WEO), Emmanuel Mosha, alisema kuwa makundi hayo yamelalamikiwa na wakulima kuharibu mazao yao.

"Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji (Masaini), wewe unalalamikiwa kuwaita wafugaji na unawakingia kifua wewe kwa wakulima, nakuagiza mbele ya wananchi hawa kawaondoe mwenyewe haraka kabla sijachukua hatua, naanza na wewe na usipotekeleza, nitakusukuma ndani," alisema mtendaji huyo.

**Tunaziomba serikali za mikoa hii miwili zikutane na kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya mara kwa mara ambayo inatishia amani.**

Hiyo mifugo ambayo ni makundi ya ng'ombe tayari imesababisha hasara kubwa kwa wakulima.

Mtendaji huyo alikuwa akijibu taarifa ya malalamiko kuhusu mifugo hiyo iliyoibuliwa na Diwani wa Kata hiyo ya Arusha Chini, Rodgers Mmari.

Alisema kwa hali ilivyo, wanawaomba serikali kukaa meza moja na kutafuta suluhu ya kudumu ya suala hilo ili kuzuia kujitokeza kwa matukio ya uvunjifu wa amani.

Aidha, akizungumzia uharibifu huo wa mazao ya wakulima, Evarist Komba, alisema ingawa suala hilo limekuwa likitafutiwa ufumbuzi na viongozi wa wilaya za jirani pamoja na Wilaya ya Moshi kuna haja wafugaji wakatozwa faini kubwa kwa kosa hilo ili kuwakatisha tamaa ya kuhama na mifugo na kulisha mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima

Zaidi Komba ameeleza: "Kwa mara kadhaa niliwahi kuona Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeweka mabango ya kuzuia uingizaji wa mifugo kutoka Wilaya ya Simanjiro kuingia Wilaya ya Moshi, lakini wafugaji waliyaondoa.

"Tunaziomba serikali za mikoa hii miwili zikutane na kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya mara kwa mara ambayo inatishia amani."




Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Richard Kasesela, akikata utepe kuzindua duka jipya la Tigo, lililopo Mtaa wa Miomboni mjini humo jana. Wengine ni wafanyakazi wa Tigo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi wanyamapori yakutanisha wafugaji

Na Godfrey Mushi, SAME

TAASISI ya Wanyamapori Afrika (AWF), imewakutanisha wafugaji kutoka wilaya tano za mikoa ya Kilimanjaro na Tanga kujadili juu ya changamoto za mifugo kuvamia hifadhi, maendeleo yao na jinsi wanavyoweza kushirikiana na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kuboresha maisha yao.

Taarifa iliyothibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, inaeleza kuwa wafugaji hao walikuwa wakipewa maelekezo ya kwa nini wanapaswa kufanya ufugaji wa kisasa na wenye tija.

"Yako mambo mengi wamejadili likiwamo suala muhimu kuhusu sheria za hifadhi zaelezwa zinazozuia mifugo kuingizwa hifadhini na jinsi wanavyohusiana na jamii inayowazunguka," alisema.

Wilaya zilizokutana kujadili masuala ya ufugaji na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ni Same, Mwanga, Lushoto, Mkinga na Korogwe.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Wilaya, Taasisi hiyo ya AWF imekuja kueleza dhamira yao ya kuona wafugaji wanajua faida ya Hifadhi ya Mkomazi na kuona ni fursa kwao.

Alisema kusudio la taasisi hiyo ni kutaka kubadilisha maisha ya wafugaji kwa kufanya ufugaji wao kuwa na tija zaidi.

Senyamule amegiza kufanya vikao hivi walau mara moja kwa mwaka, pia kupeleka huduma zinazohusisha ufugaji.

"Nataka watu wajue kuwa kama mtu asipowahifadhi vizuri wanyamapori, na maliasili nyinginezo, zitapotea. Nataka wafugaji mshiriki ujenzi wa miundombinu yenu, undeni ushirika, zingatieni sheria na kusomesha watoto ili baadaye wajue kufuga kisasa badala ya kurithi ufugaji huu wa kuhama hama kufuata malisho," alieleza mkuu huyo.

Akizungumzia fursa iliyotolewa na Rais Dk. John Magufuli juu ya maeneo ya malisho katika hifadhi. Ameeleza mpango mkakati wa utalii wa wilaya hiyo na dhamira ya wilaya hiyo ni kuvutia utalii.

Aliwashukuru AWF kwa kuwezesha kikao kilichoonekana kuhitajika na kila upande.

Katika mkutano huo, jamii ya wafugaji kutoka wilaya hizo waliomba maeneo ya malisho yanayotengwa kuwa na hati, pia wakaomba kujengewa mabwawa ya maji na huduma nyingine zitakazowezesha mifugo kupata huduma bila kuingia hifadhini.

# Uhaba wa maji watesa wakazi wa Rombo

Na Mwandishi Wetu, ROMBO

HALI mbaya ya kiuchumi inayotishia kasi ya ukuaji wa vijiji vitatu vya Kibaoni, Nayeme na Nanjara vilivyopo katika Wilaya ya Rombo, imeelezwa kuwa inasababishwa na kukosekana kwa huduma ya maji kwa miongo kadhaa sasa.

Vijiji hivyo ambavyo vinakabiliwa na tatizo kubwa la kukosa maji, Wilaya ya Rombo pia huathiriwa zaidi na uhaba wa maji kutokana na kupungua kwa ujazo kutoka mita za ujazo 27,000 hadi kufikia 18,000.

Katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo, Meneja wa Kampuni ya Maji ya Kili Water ambayo inatoa huduma wilayani humo, Prosper Kessy, amesema tayari wamevitengea vijiji hivyo kiasi cha Sh. milioni 155 kuvipelekea huduma ya majisafi mwaka huu.

"Mradi huo utahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha maji kutoka msitu wa serikali wa shamba la Rongai, lenye urefu wa zaidi ya kilometa 12 na kuyasafirisha hadi tangi lililopo Kijiji cha Kibaoni, tayari kwa kusambaza katika vijiji vingine viwili vya Nayeme na Nanjara," alisema.

Januari 31, mwaka huu, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 ambao pamoja na mambo mengine utaruhusu kuundwa kwa Wakala wa Maji Vijiji.


Alisema mahitaji ya maji wilayani humo ni mita za ujazo zaidi ya 40,000, lakini upatikanaji wa maji ni mita za ujazo 27,000.

Akitetea hoja yake kuhusu tatizo la maji kutofika maeneo yote ya wilaya hiyo, Kessy ameeleza kwamba tatizo linalochangia kukua kwa hali hiyo ni kuwapo kwa vyanzo vichache vya maji na ambavyo vingi kati yake, hukauka mara kwa mara.

Alisema zaidi ya wakazi 20,700 wanapata huduma ya maji wilayani humo baada ya kuboresha huduma za upatikanaji wa maji. Awali kampuni hiyo wakati inaingia Wilaya ya Rombo kuanza kutoa huduma mwaka 1995, walikuta wananchi 5,200 wa majumbani, ndio walikuwa wameunganishiwa huduma ya maji.

Kili Water ilikuta mtandao wa usambazaji maji, ulikuwa kilometa 700, lakini sasa umeongezeka hadi kufikia 1,200, huku vyanzo vya maji vikiongezeka kutoka vyanzo 24 hadi 30.

Ukurasa 18



## NYERERE ALIVYOIKOMALIA HOJA KUHUSU TANGANYIKA

**MAKALA:**

## Bulaya awaachia wapiga kura kuamua hatima 2020



Ukurasa 15

**KIMATAIFA:**



## Saudia yawekeza vitega uchumi kimkakati Pakistan na China


Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO MACHI 27, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

## Kupuuza sera na mipango ya maendeleo kumeiua Afrika

Ukurasa 14

# NI KIMBUNGA HAMAD Z'BAR

## Mahasimu wabeza, msako wahujumu, wachoma bendera na kadi wapangwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



KITENDO cha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF, Seif Sharif Hamad (pichani), maarufu Maalim Seif, kukihama chama hicho na kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo, kinaelezwa kuwa ni kupoteza nguvu za kisiasa na kurudi nyuma kwenye harakati za mapambano ya siasa za kipinzani.

Ni maoni ya Hamad Rashid Mohamed, mwanasiasa mkongwe na aliyekuwa mshirika wa karibu wa Maalim Seif, lakini aliyefukuzwa CUF, na kuunda chama chake.

Hamad Rashid, anasema hayo mjini Zanzibar wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maamuzi ya Maalim Seif kuikimbia CUF.

**AIITA HADAA**

Hamad Rashid, anadai alichokifanya Maalim Seif ni kutaka kuwadanganya wafuasi wake kwa kuficha hoja zake za kutaka kuapishwa na kuingia madarakani ambazo zimegonga mwamba na sasa kuwafanya wafikirie suala la kuingia katika chama kipya.

Analiona kuwa ni jambo la kushangaza kwa mwanasiasa kama yeye kukiacha chama alichokiasisi na 'kuchupia' jahazi ambalo hafahamu vizuri safari zake baharini huku, akiwaacha wafuasi wake ambao aliwapa ahadi za matumaini ya kufaidi matunda ya uongozi wa juu wa serikali.

Anakielezea kitendo hicho alichokifanya

ENDELEA UK 16

UCHAMBUZI

# Kupuuza sera na mipango ya maendeleo kumeiua Afrika

**Na Salome Kitomari**



Rais mstaafu Obasanjo katika mihula tofauti ya uongozi wa Nigeria, awali aliongoza kama Jenerali wa jeshi na mwishoni kama kiongozi aliyechaguliwa na raia. **PICHA: MTANDAO**

RAIS wa zamani wa Nigeria, Olusegun Obasanjo, ni miongoni mwa viongozi wa Afrika wanaoibua maono kuhusu kile kinachohitajika kufanyika ili kuwa na Afrika yenye maendeleo.

Katika moja ya nukuu zake zinazochambua umaskini wa Afrika anasema maendeleo duni ya Afrika ni matokeo ya viongozi wa bara hili kushindwa kutekeleza sera na mipango mingi ya maendeleo.

Anayasema hayo akizundua kitabu cha 'Making Africa Work', ambacho kiliandikwa kwa ubia baina ya Obasanjo na waandishi wengine.

"Serikali za Afrika hazijataka kutekeleza sera mwafaka za maendeleo lakini athari ndizo hizo wengi wametembea kwenye changamoto kubwa zilizotokana na kupuuzia ama kuacha sera na mipango ya kuleta maendeleo," anakumbusha Obasanjo.

Mara nyingi wakuu wa Afrika wanaitisha mijadala ya kuchambua mwelekeo wa bara hili katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii wakiliangalia kwenye vipindi mbalimbali mathalani, wakati wa uhuru, baada ya uhuru na sasa miaka 60 baada ya ukombozi.

Viongozi hao katika mikutano hiyo ukiwamo Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU), unaofanyika makao makuu ya AU, Addis Ababa Ethiopia kila baada ya miezi sita, mijadala mikubwa inalenga kupata majibu ya mbinu za kuliendeleza Bara la Afrika.

Matatizo ya nchi hizo ni yale yale na wakati mwingine hubadili mwelekeo kutokana na mazingira, kwa mfano umaskini umekuwepo Afrika na kila mara zinatajwa sababu za ufukara kuwa kikwazo cha maendeleo na mikakati ya kuumaliza.

Changamoto nyingine ni migogoro ya kisiasa, kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa viongozi wanaoshika madaraka, kuongoza kwa muda mrefu baada ya kubadili katiba ili iwape uhalali wa kuendelea kuwapo madarakani, unyanyasaji na uonevu wa raia.

Ndiyo maana Obasanjo, anasema ni lazima Waafrika wajiulize ni Afrika gani wanayoitaka?

Na kama watakubaliana wanataka Afrika gani ambayo haina atakayekandamizwa, kila mtu atakuwa na fursa sawa, bara lenye demokrasia na inaruhusu kila mmoja kushiriki, kupewa fursa ya kuonyesha uwezo wake na iwe rafiki kwa wote.

Anasema uongozi wowote ni lazima ubebe mwelekeo bora siku zote, tena uongozi ambao hauna mwelekeo hauwezi kuleta mabadiliko au mafanikio.

"Kiongozi anapaswa kuongoza muda wote katika mazingira yoyote. Je tunapataje viongozi kwa Afrika tunayoitamani? Wapo wanaofanya vizuri lakini hatuna wengi? Je, tunahitaji kuwa nao wengi ili tuweze kuifikisha Afrika mahali ambako tunaona inastahili kufika," anahoji Obasanjo.

**VIJANA**

Obasanjo anaziona changamoto nyingi zinazowakabili vijana na lazima zitatuliwe kwa kuwajumuisha kwenye madaraka, ni lazima kuwapa nafasi na kuwaamini kwani wana nguvu na akili zinazofanyakazi kwa haraka zaidi badala ya kuendelea kujaza wazee kwenye uongozi.

> Bado kuna safari ndefu kuifikia Afrika tunayoitamani kwa kuwa tunaogopa kuzungumza kwa uwazi, kusema mabaya yanayotendwa na wenzetu. Ni lazima tujifanyie tathimini, ukweli na uwazi ndiyo mwongozo mzuri kwa viongozi wa Afrika,"

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika mwaka 2015, Nkosazana Dlamini-Zuma, anasema wanahitajika viongozi wanaoifikiria Afrika kwa ujumla wake.

Wanahitajika viongozi wa bara hili siyo nchi moja moja kwa kutambua kuwa, kuwa na ukubwa na umoja ulio na nguvu ndiyo nguzo ya maendeleo, anasema.

"Vijana ndiyo taifa la sasa, kuwa na viongozi wanaowekeza kwenye vijana iwe dira, hatuwezi kufikia malengo ya kuwa na Afrika tunayoitaka kama hatutawapa vijana usukani," anasema Zuma.

Anataka Afrika ijiwekee malengo ya kuandaa vijana wenye ujuzi wa kila aina kushika na kuongoza sekta zote ili kufanyakazi kwenye maeneo yote ya kuleta maendeleo.

Anasema kama vijana watapewa ujuzi watajua nini chakufanya na ili kuwafikia wengi ni lazima kutumia teknolojia itakayowafikisha kwenye ubunifu na ugunduzi kwenye maeneo ya uwekezaji.

Rais wa Rwanda, Paul Kagame, anasema kujadili uongozi na Afrika tunayoitaka au kuitamani ni swali ambalo limekuwepo miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwake na mjadala wake umeendelea kujitokeza kila kwenye kikao cha AU.

"Tunaweza kuongelea uongozi kinadharia na kinachotarajiwa, tumetumia muda mwingi kueleza matatizo ya Afrika, kilichokosekana ni kutekelezaji ili kuifanya Afrika ifikie malengo inayotarajiwa," anasema Kagame.

"Ni lazima kuwa na viongozi ambao wako kwa ajili ya kuongoza kufikia malengo mahususi kwenye maendeleo, watakaoleta mabadiliko na matokeo chanya." Anasisitiza kiongozi huyo.

**KUAMBIANA UKWELI**

Aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Thabo Mbeki, anasema ili kufikia maono ya Afrika tunayoitamani' isiyokuwa na umaskini, vita na migogoro ya ardhi na rushwa kipaumbele ni uongozi bora. Anasema ni vyema viongozi wakaambiana ukweli, wakiwamo wanaoiba mali ya umma, kukandamiza demokrasia na kuwaeleza wazi kuwa uongozi katika taifa fulani haukuwa na tija.

Anasema yote hayafanyiki kwa kuwa kuna woga katika kuelezena ukweli pale kiongozi anapokosea.

"Bado kuna safari ndefu kuifikia Afrika tunayoitamani kwa kuwa tunaogopa kuzungumza kwa uwazi, kusema mabaya yanayotendwa na wenzetu. Ni lazima tujifanyie tathimini, ukweli na uwazi ndiyo mwongozo mzuri kwa viongozi wa Afrika," anasema Mbeki, aliyeiongoza Afrika Kusini baada ya kuondoka Nelson Mandela.

Aliyekuwa Rais wa awamu ya nne, Benjamin, Mkapa, anasema Afrika inatakiwa iwe na usawa wa kijinsia, fursa, uhakika huduma bora za afya, elimu na uongozi unaofikiria kutumikia zaidi kuliko kutumikiwa pamoja na kuondoa vikwazo kwenye mipaka.

"Kwanini yote hayo? Jibu langu liko wazi kabisa kwamba Afrika ina viongozi wabinafsi, tunafikiria tatizo la uongozi limekuwa ni tatizo la viongozi wenyewe, ni lazima mabadiliko yawapo kuanzia kwenye vyama na jamii kwa ujumla," anasema.

Anasema haiingii akilini kwamba Afrika yenye rasilimali muhimu lakini zinanyonywa na watu ambao waliitawala badala ya kuzitumia kwa maendeleo ya raia wa Waafrika.

Mkapa anasema ili kuendelea ni lazima kuweka msisitizo kwenye utoaji wa huduma bora za afya na kwamba nchi kama Rwanda imeendelea kwa kuwa kuna uhakika wa huduma bora za afya na elimu.

"Ni lazima tufikiri upya wapi tulipo, kwanini tupo hapo na nini kitafanyika kutoka hapo tuliko kuyaendea maendeleo," anasema Mkapa.

Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika mwaka 2005 hadi 2015, Dk. Donald Kaberuka, anasema uongozi wa Afrika katika ngazi zote kuanzia kibiashara, siasa na uchumi umeshindwa kupata mafanikio, hivyo ni lazima kujadili nini cha kufanya ili kuwa na Afrika tunayoitaka.

Anasema changamoto anazoziona ni kukosekana kwa imani baina ya wananchi na viongozi. Kipo kiasi kidogo cha imani na sera za maendeleo za nchi mbalimbali na wananchi hawana imani kwamba sera hizo zipo kwa ajili ya maendeleo yao.

Anashauri kuwe na fikira zenye mabadiliko akisema viongozi wajiambie: "Wajibu wangu kama kiongozi ni kufanya maendeleo wakati nipo madarakani kwa kuwa tunachokifanya siyo kuhesabu mafanikio kwa kipindi tulichopo madarakani kwa kuwa tunachoongoza siyo mafanikio bali ni maisha ya wananchi," anasema Dk. Kaberuka.

Kwa ujumla viongozi hao wanaziona sababu zinazozididimiza Afrika, lakini licha ya mijadala mizuri kila wakati shida za Afrika zipo pale kwa kuwa bado hakuna utashi wa kisiasa wa kuondoa au kumaliza matatizo yaliyopo, ndani ya bara lenye rasilimali zote muhimu kwa maendeleo.



Mbunge wa Jimbo Bunda Mjini, Esther Bulaya, akihutubia katika moja ya mikutano yake. **PICHA: MTANDAO**

# Bulaya awaachia wapiga kura kuamua hatima 2020

**Na Sabato Kasika**

ESTER Bulaya ni miongoni mwa wanasiasa vijana aliyeanza kuvuma katika siasa za Tanzania tangu akiwa Mbunge wa Viti Maalumu kundi la Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mara.

Nyota yake iling'aa kutokana na umachachari na kuonyesha umahiri mkubwa bungeni kuhoji na kusimamia hoja za maendeleo ya vijana, wanawake pamoja na mustakabali mzima wa kutumia bunge kwa manufaa ya Watanzania kwa kuishauri, kuikosoa na kuihoji serikali bila hofu au kukiogopa chama chake.

Licha ya kwamba mila potofu na ukandamizaji wa kijinsia ni suala lisilokwepeka na ndilo linalowaangusha wanawake kwenye masuala mengi yanayohusu uongozi wa jamii, Bulaya alivuka kizingiti hicho na kuonekana kama nyota ya asubuhi na kuchaguliwa kwa kura za kutosha kuwa mbunge wa Bunda Mjini jimbo lenye historia ya kukaliliwa na vigogo wakiwamo viongozi na mawaziri waandamizi wa serikali za awamu zilizopita.

Hivi karibuni Bulaya ambaye ni Waziri Kivuli (Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), anaibua hoja ya kupingana na sheria ya mafao ya wafanyakazi ambayo ililekeza watumishi kulipwa kiasi kiduchu cha fedha .

Mwanasiasa huyo kwa sasa ni mbunge wa Bunda Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), nafasi aliyoipata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ikiwa ni miezi michache tangu ahame kutoka CCM.

Bulaya ni mwanasiasa anayepigania haki za vijana bila kuangalia itikadi zao za vyama, dini wala kabila zao, ndivyo amekuwa akijipambanua na kujipatia umaarufu ndani na nje ya bunge.

Anaamini kwamba vijana wakiweka pembeni itikadi za vyama vyao na kuunganisha nguvu wanaweza kufanya kazi na kujiletea maendeleo kwa vile wao ndio nguvukazi ya taifa.

> "Ninapenda kuwa karibu na wananchi wangu, lakini mwanzoni wakati ninaanza kazi hii nilikumbana na changamoto hizo, lakini niliwaambia wananchi wasiwe na hofu, mimi bado ni mbunge wao,"

Wakati akiwa CCM, aliwahi kusema kuwa ameingia bungeni kuwakilisha vijana na yupo tayari kupoteza uhai kwa kulitetea taifa lake, hata kama ataonekana msaliti katika chama chake kwa kukemea uovu."

Pamoja na kuwa mbunge wa viti maalum, Bulaya alikuwa anatamani kupata jimbo na ndipo miezi michache kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 alihamia upinzani na kufanikiwa kuchaguliwa kuwa mbunge wa jimbo.

Anasema anaamini kwamba msimamo wake wa kuunganisha vijana bila kujali itikadi, dini na kabla ambao uliwahi kumwingiza matatani wakati akiwa CCM ni mzuri kwa vile Tanzania haina ubaguzi wa aina yoyote.

**UCHAGUZI 2020**

Bulaya anasema jambo la msingi kwake ni maendeleo ya Bunda Mjini na kwamba suala la kuwania ubunge mwaka 2020 siyo kipaumbele chake wakati huu ambao anaendelea kutekeleza ahadi zake kwa wananchi.

"Baadhi ya watu wamekuwa wakimuuliza kuhusu uchaguzi huo wa mwaka 2020 kama nitawania ubunge. Jibu langu ni kwamba kipaumbele changu ni kuwatumikia wananchi siyo uchaguzi huo," anasema.

Anasema utendaji wake na utekelezaji wa ahadi kwa wananchi wa Bunda Mjini ni wa muhimu zaidi, na wao ndiyo watampima kulingana na jinsi ninavyowatumikia kwa kuamua kumrudisha bungeni.

Anasema amekuwa akitumia muda mwingi jimboni ili kushirikiana na wananchi kwa ajili kutekeleza majukumu yake ya kibunge, kwa vile alishaahidi kutokuwa mbali na jimbo kwa muda mrefu.

"Kwa ujumla ni kwamba nimeshatekeleza ahadi nyingi kwa asilimia kubwa nikishirikiana na wananchi, kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo na zangu binafsi, ndiyo maana ninasema mwaka 2020 wao ndiyo wataamua," anasema.

Mbunge huyo anasema awali wananchi walikuwa hawana uelewa kuhusu fedha za mfuko wa jimbo, lakini wameshaelimishwa na sasa wanafahamu jinsi ambavyo zimekuwa zikitumika ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

"Baadhi ya fedha hizo zimetumika kukarabati vyoo na kujenga madarasa ya shule za msingi, kununua madawati, kununua mabomba ya maji na ujenzi wa zahanati za vijiji ili kusogeza huduma za jamii zikiwamo za afya karibu na wananchi," anasema.

Anasema jimbo lake hupokea Fedha za Mfuko wa Jimbo Sh. milioni 34. 6 kila mwaka na huzitumia kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na kwamba wana imani na matumizi ya fedha hizo kwa vile wanashirikishwa.

"Ninatambua na kuheshimu dhana ya ushirikishwaji kwani ninafanya kila kitu kwa uwazi nikishirikiana na wajumbe wa mfuko huo, hivyo kila senti inajulikana inavyotumika," anasema.

**CHANGAMOTO**

Hakuna kisichokuwa na mabonde na mito anasema mbunge huyo, anayetaja baadhi ya changamoto alizowahi kukumbana nazo kuwa ni kukamatwa mara kwa mara na vyombo vya dola na pia kufunguliwa kesi ya kupinga ushindi wake na kusababisha atumie muda mwingi nje ya jimbo.

"Ninapenda kuwa karibu na wananchi wangu, lakini mwanzoni wakati ninaanza kazi hii nilikumbana na changamoto hizo, lakini niliwaambia wananchi wasiwe na hofu, mimi bado ni mbunge wao," anasema.

Anasema pamoja na changamoto hizo, hakukata tamaa kwa vile anajua anachokifanya na pia wananchi walikuwa nyuma yake wakimtia moyo.

"Siasa siyo lelemama, lazima mtu ukomae, mimi ni jasiri, wananchi wa Bunda walijua hilo na hawana shaka nami, kwani wanaelewa kuwa changamoto za siasa zinanikomaza na ninaendelea kutimiza ahadi zangu nilizoahidi wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015," anasema.

Bulaya anasema hata Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ulishauona ujasiri wake huo na kumpa tuzo ya 'Kiongozi Mwanamke Jasiri Mtetezi wa Haki', hivyo anaendelea kujivunia ujasiri huo.

Anasema changamoto kubwa anayoendelea kuikumbuka ni ile ya kupotezewa muda katika kesi ya kupinga ushindi wake na kwamba pamoja na hayo, alishamsamehe mpinzani wake Stephen Wasira.

"Hizo ni sehemu ya changamoto na kama unakumbuka, baada ya mahakama kuhalalisha ushindi wangu nilitangaza kumsamehe na kumtaka tuungane kwa ajili ya maendeleo ya Bunda Mjini," anasema.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Mahasimu wabeza, msako wahujumu, wachoma bendera na kadi wapangwa

Maalim Seif kuwa ni kosa sawa na kiongozi wa jeshi vitani aliyekuwa mstari wa mbele kukimbia mapambano na kuwaacha wapiganaji wake mikononi mwa vikosi vya adui

''Maalim Seif amepoteza mvuto wa kisiasa ambapo anatakiwa kustaafu siasa kwa sababu hana nguvu tena za ushawishi kama anavyowadanganya wafuasi wake.''anadai Hamad Rashid.

Aidha, Mohamed anaongeza: "Kilichofanyika kwa Maalim Seif ni sawa na mtu aliyepewa adhabu baada ya kuwaadhibu wenzake wengi kwa muda mrefu bila ya sababu za msingi kwa kujiona mwanasiasa bora."

Anamkosoa Maalim Seif kwa kupenda uadui, akisema amejenga uadui mkubwa kwa baadhi ya wanachama na viongozi wa kisiasa kwa tabia yake ya'fukuzafukuza', huku akijifanya mwenye mamlaka ya juu ndani ya CUF.

''Umeona wapi muhusika mkuu katika igizo au filamu akafariki kabla ya igizo hilo kumalizika ....Huyu Maalim kwa muda mrefu kazi yake ilikuwa kuwaadhibu wenzake na leo hii zamu yake imefika, tena ndani ya chama alichokiasisi mwenyewe','anasema Hamad Rashid.

Anaeleza kuwa tathmini yake katika siasa ina wasiwasi kuwa kiongozi huyo hatadumu katika harakati za kisiasa kwa sababu tofauti za kisera na kiitikadi.

Anaongeza kuwa Maalim Seif hakutakiwa kujiunga na chama badala yake alipaswa kuunda chama chake cha siasa ili kutekeleza ahadi zake pamoja na usimamizi wa sera.

''Bado mimi sijaona kwamba maalim Seif yupo salama kisiasa kwa sababu naona kuna mitizamo pamoja na sera zinazotofautiana kwa kiasi kikubwa,''andai Hamad Rshid.

**HISTORIA YAO**

Hamad Rashid pamoja na Maalim Seif walikuwa ni watu marafiki sana ambapo kwa pamoja walifukuzwa kutoka Chama Cha Mapinduzi mwaka 1988 kwa madai ya kwenda kinyume na maadili ya chama hicho.

Kwa wakati huo Hamad Rashid, alikuwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi katika kipindi cha uongozi wa mstaafu Ali Hassan Mwinyi, na kwa upande wa Maalim Seif alikuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Julai mwaka 2015, Hamad Rashid alihama CUF na kuunda chama cha Alliance for Democratic Change -ADC. Aidha, ni Waziri wa Kilimo wa Serikali ya Zanzibar, inayoongozwa kwa utaratibu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

**WAPINZANI WAPONGEZA**

Kwa upande wake Mwenyekiti wa chama cha AFP Wakulima Said Soud, alisema ni jambo la kawaida kwa mwanasiasa kubadilisha chama baada ya kuona kilichopo kimepoteza mwelekeo.

''Kilichofanywa na Maalim Seif Sharif Hamad ni maamuzi ya kawaida ambayo yanatakiwa kufanywa na mwanasiasa mkongwe katika kuimarisha demokrasia ya mfumo wa vyama vingi nchini''anasema Soud na kupongeza.

Aidha Makamu Mwenyekiti wa chama cha Ada, Tadea Juma Ali Khatib, anasema ni uamuzi sahihi lakini ingelipendeza zaidi kama Maalim Seif angelianzisha chama chake mwenyewe.

Anasema anachofahamu vyama hivyo viwili vinatofautiana katika sera na itikadi ambapo kwa upande wa mlengo wa kisiasa wa Maalim Seif ni kuwa na Serikali ya Muungano ya mkataba.

''Sina tatizo la uamuzi wa Maalim Seif kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo ingawa tatizo naona linakuja katika sera na itikadi na muelekeo wa viongozi wa vyama hivyo naona kama wanatofautiana,''anaeleza wasiwasi.

> "Tumetoa maelekezo kwa viongozi wote waliokuwa wa chama cha CUF kushusha bendera za chama cha CUF na kuweka za chama cha ACT- Wazalendo kazi ambayo imefanyika Unguja na Pemba,"



Seif Sharif Hamad (kushoto) akimsikiliza Hamad Rashid. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mbunge wa Kigoma Mjini na kiongozi wa Chama Cha ACT – Wazalendo, Zitto Kabwe

**WAFUASI WA MAALIM**

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa Chama cha CUF, Salim Bimani, anasema wamepokea taarifa za kiongozi wao kujiunga na chama cha ACT-Wazalendo kwa mikono miwili na wanaungana naye kwenye maamuzi yote.

Anasema mambo muhimu waliyoyafanya mara baada ya kutangazwa kwa uamuzi huo ni yaliyokuwa matawi ya CUF kubadilishwa rangi na kupakwa za chama cha ACT- Wazalendo.

''Tumetoa maelekezo kwa viongozi wote waliokuwa wa chama cha CUF kushusha bendera za chama cha CUF na kuweka za chama cha ACT- Wazalendo kazi ambayo imefanyika Unguja na Pemba," anaongeza Bimani.

Anamfananisha Maalim Seif na nahodha katika usafiri wa baharini hivyo kitendo cha kutoka CUF ni sawa na kuwaokoa abiria wake ambao jahazi alilokuwa akiliendesha lilikuwa hatarini kuzama baharini.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili umegundua kwamba ofisi kuu za chama cha CUF Mtendeni zimefungwa pamoja na ofisi nyingine Unguja na Pemba huku zikiwa zimepakwa rangi na kupachikwa bendeza za ACT- Wazalendo.

**MSIMAMO MBADALA**

Makamu Mwenyekiti wa CUF, Abasi Muhunzi, kwa upande wake anawataka wanachama wa chama hicho kufuata sera, katiba na malengo ya chama chao na kuacha siasa za kumfuata kiongozi au kufuata upepo.

Anasema chama hicho kwa miaka mingi kimeshindwa kufikia malengo ya kushika dola kwa sababu ya kuongozwa na fikra ambazo hazikukamilisha malengo hayo.

Anasema wakati umefika sasa chama cha CUF kuachana na siasa zisizokuwa na tija za kufuata mawazo ya kiongozi au mtu mmoja ambayo pengine hayana muelekeo wa kujenga mshikamano katika chama hicho.Anaeleza fukuzana katika chama ni mambo ambayo yamekifikicha chama hicho katika wakati mgumu na kuonekana kama taasisi ya mtu binafsi, hatua ambayo ilijenga chuki kwa wanachama na viongozi.

Anawataka wanachama na wafuasi wa CUF kujipanga na sasa chama hicho kinapita katika harakati za mikakati ya kuzaliwa upya kwa ajili ya kuelekea kushika dola katika uchaguzi mkuu mwaka 2020.

**HUJUMA YA MALI**

Muhunzi anasema CUF haitomvumilia yeyote aliyeshiriki kuhujumu mali za chama hicho ikiwamo kuchoma moto bendera, kadi pamoja na matawi ya chama hicho kuyageuza kuwa ya ACT- Wazalendo.

Anaonya kuwa mali zote za chama hicho zinatambulika kisheria hivyo hakuna haja ya kuona zinaendelea kuharibiwa na watu wenye dhamira mbaya.

"Tupo katika hatua ya kuandaa mpango wa kutembelea matawi yote ya chama ambayo kwasasa yamefanyiwa hujuma na mengine kugeuzwa kuwa ofisi za chama cha ACT Wazalendo,"anasema Muhunzi.

Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa CUF, Mussa Kombo anawataka wanachama wa CUF kuimarisha umoja na mshikamano kwa lengo la kukifanya chama kuwa imara katika kuelekea kwenye mapambano ya kushika dola.

Anawahimiza wafuasi wa chama hicho wasitetereke kutokana na kitendo cha baadhi ya wanachama kumuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif na kuihama CUF, kwani bado wapo wanachama wenye uwezo wa kupima ukweli na kufanya uchambuzi wa kina katika mambo ya siasa.

"Chama chetu kinazingatia ubora na si kufuata matakwa ya mtu binafsi....Sisi tupo imara wala hatujayumba na wale wanaokihama chama hicho na kujiunga na ACT- Wazalendo kwa kumfuata Maalim Seif ni hiari yao,"anasema Komba.



Rais Abdelaziz Bouteflika. **PICHA: MTANDAO**

# Bouteflika apingwa ndani ya chama

CHAMA cha rais mkongwe wa Algeria Abdelaziz Bouteflika, kimekataa mpango wake wa kuitisha mkutano wa kitaifa kutafuta suluhu ya vuguvugu la maandamano ya upinzani nchini humo.

Mpango wa mkongwe huyu wa Algeria kuitisha mkutano wa kitaifa kutafuta suluhu ya vuguvugu la maandamano ya upinzani, umekataliwa na chama chake mwenyewe, kwa mujibu wa Msemaji wa chama cha FLN.

Alisema jana kupitia kituo cha televisheni cha Dzair News kinachomilikiwa na watu binafsi, kwamba mkutano huo hauna maana tena, kwa sababu ungewahusisha viongozi ambao hawakuchaguliwa, na tayari umekataliwa na waandamanaji.

Msemaji huyo, Hocine Khaldoun, anasema suluhisho kwa matatizo ya kisiasa ya Algeria itamalizwa na uchaguzi, utakaomweka madarakani rais mwingine anayeweza kuzungumza na wananchi.

Hatua hiyo ni pigo kubwa kwa Bouteflika mwenye umri wa miaka 82, ambaye anaonekana hadharani kwa nadra sana tangu, alipopata ugonjwa wa kiharusi mwaka 2013.

Mapema mwezi huu, Bouteflika, alitangaza kutogombea urais kwa muhula wa tano kwa lengo la kumaliza maandamano ya wiki kadhaa kuipinga hatua yake ya kutaka kuendelea kuwa Rais wa Algeria.

Katika barua yake iliyosomwa kupitia Televisheni ya Taifa, APS, Rais Bouteflika, aliapa kwamba hatogombea tena katika uchaguzi wa urais, baada ya kuitawala nchi hiyo kwa miaka 20. Aidha, Bouteflika aliahirisha uchaguzi mkuu wa nchi hiyo uliokuwa ufanyike Aprili 18 2018, na anakusudia kufanya mageuzi kadhaa katika mfumo wa kisiasa na katiba nchini Algeria.

Bouteflika alisema aliufikia uamuzi huo ili kufanya marekebisho katika serikali yake haraka iwezekanavyo na kwamba mabadiliko hayo yanatokana na madai ya wananchi wa Algeria. Alibainisha kuwa ataunda jopo ambalo litapanga tarehe mpya ya uchaguzi wa urais.

Maelfu ya wananchi wa Algeria walijitokeza mitaani kushangilia uamuzi huo wa Bouteflika.

Honi za magari zilikuwa zikisikika barabarani kwenye maeneo ya katikati ya miji nchini humo, huku baadhi ya Waalgeria wakipepereusha bendera za taifa hilo. Taarifa zilieleza kuwa polisi hawakuonekana mitaani wakati wa shamrashamra hizo.

**BBC**

# Nyerere alivyoikomalia hoja kuhusu Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya vuta nikuvute na vikao kadhaa kati ya viongozi wa serikali na CCM pamoja na wabunge waliokuwa wakiunga mkono kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika, maarufu kama G-55, hatimaye hoja hiyo iliwasilishwa Bungeni.

Kuwasilishwa kwa hoja hiyo Agosti 23, 1993 kulisababisha kuandikwa kwa historia mpya ya siasa za Tanzania. Licha ya serikali hiyo iliyofutwa rasmi mwaka 1964 kutokana na Muungano wa mataifa mawili- Tanganyika na Zanzibar na kupatikana serikali mbili, haujaundwa takriban miaka 26 sasa, mpaka sasa kuna mabadiliko makubwa.

Hoja hiyo imezaa mambo mengi ambayo yamesababisha Muungano kuendelea. Miongoni mwa mambo hayo ni watu kutoka Tanzania bara kwenda upande wa pili wa Muungano bila pasi za kusafiria kama ilivyokuwa awali. Pia kero mbalimbali za Muungano zimefanyiwa kazi na kuondoa manung'uniko yaliyokuwapo.

Baada ya serikali kupitia aliyekuwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Samuel Sitta na Waziri Mkuu na makamu wa Kwanza wa Rais wakati huo), John Malecela, kuunga mkono, mtoa hoja hiyo kwa niaba ya G-55, Njelu Kasaka, aliyekuwa Mbunge wa Chunya, aliwasilisha iliyosomeka:

"Serikali iandae na kusimamia utaratibu utakaoshirikisha wananchi na taasisi nyingine, kwa madhumini ya kufikisha Bungeni kabla ya Aprili 1995, mapendekezo ya muundo muafaka wa Muungano ambao utahusisha, pamoja na mambo mengine, kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano."

**QARESI AGEUKA**

Pamoja na hoja hiyo kuungwa mkono, baadhi ya wabunge wakati wa kuchangia waliipinga akiwamo aliyekuwa mwenyekiti wa kamati ya G55, Mateo Qaresi, aliyekuwa Mbunge wa Babati.

Qaresi katika kuchangia hoja hiyo baada ya kuwasilishwa, alisema hotuba iliyowasilishwa si sehemu ya azimio hivyo kuwataka wabunge watambue azimio lilivyotokea kwenye orodha ya shughuli za kila siku za Bunge (Order Paper).

Akielezea katika kitabu chake cha Njelu Kasaka; Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika-G55, Kasaka anasema baada ya Qaresi kutaka hotuba hiyo iwe yake (Kasaka) alishangaa hotuba hiyo kutoonekana kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

"Watu wengi walilalamika kwamba hotuba hiyo haipatikani kwenye kumbukumbu za Bunge. Nakumbuka viongozi wa CCM na seriakli walivyonitaka niwasilishe hoja bila hotuba kwa madai kwamba serikali ilikwishaunga mkono hoja, hivyo hotuba isiwepo," anasema Kasaka.

**YALIYOTOKEA BAADAYE**

Kasaka anasema baada ya kuwasilisha na Bunge kupitisha azimio, malecela na wabunge wenzake walimpongeza na wakati huo nje ya ukumbi wa Bunge kundi kubwa la watu lilikuwa likimsubiri.

"Nilichelewa kidogo kutoka kutokana na kupokea pongezi kutoka kwa wabunge. Nilipotoka kupitia mlango wa mbele, wananchi walianza kushangilia kwa nguvu, wananchi walinizunguka na kunibeba huku wakiimba 'Tanganyika, Tanganyika, Tanganyika'," anabainisha.



Julius Nyerere

> Kutokana na upinzani mkali kutoka kwa Nyerere, viongozi wa CCM walilazimika kurekebisha katiba ya chama chao (CCM) Ibara ya 8 na ya 12 ambazo zilimruhusu Mwenyekiti wa CCM kuitisha mkutano Novemba, 1993... Lengo la mkutano huo lilikuwa kutafuta njia ya kuua Azimio la Bunge ingawa ilitangazwa kuwa ni mkutano wa kutafuta njia bora ya kutekeleza Azimio,"

Hatimaye picha ya ukumbusho ya kundi la wabunge waliounga mkono mwanzo hadi mwisho kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ilipigwa huku Naibu Spika, Pius Msekwa, akiungana nao kwa ajili ya tendo hilo.

Hafla ya kupitishwa kwa azimio hilo ilifanyika Ikulu jijini Dar es Salaam ambayo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa ngazi za juu serikalini akiwamo Rais wa wakati huo, Ali Hassan Mwinyi na Waziri Mkuu Malecela. Kasaka na wabunge wengine walihudhuria hafla hiyo.

Baada ya hoja hiyo kupita na kupitishwa kwa azimio ambalo lingewezesha kuundwa kwa serikali ya Tanganyika, serikali ilitangaza kwamba ilikuwa inashughulikia taratibu za utekelezaji wa azimio hilo.

Sitta, akiwa mjini Tabora, aliwaambia waandishi wa habari kwamba serikali ilikuwa inatafuta njia ya namna ya kushirikisha wananchi kutoa maoni ya jinsi ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika na namna ya kuimarisha Muungano.

Msekwa pia alitilia mkazo kwamba uamuzi wa bunge ulikuwa wa mwisho na serikali ya Tanganyika itaundwa kabla ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 1995 huku akisisitiza kwamba wananchi watashirikishwa katika utekelezaji wa Azimio la Bunge, kwa kutoa maoni kuhusu serikali itakavyokuwa na uhusiano wake na serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar.

**MSIMAMO WA NYERERE**

Pamoja na bunge kupitisha azimio juu ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika, baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, hakukata tamaa katika harakati zake za kuhakikisha serikali hiyo haiundwi.

Muda mfupi baada ya mchakato huo wa Bunge, kilifanyika kikao cha siku tatu cha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kuanzia Oktoba 14 hadi 16, 1993 Kilimani Club mjini Dodoma.

Kasaka anasema kikao hicho kilichokuwa mahsusi kujadili azimio la Bunge, ilielezwa kuwa Nyerere aliwakoromea viongozi wa CCM kwa kuruhusu Bunge lipitishe azimio la kuundwa kwa serikali ya Tanganyika.



Njelu Kasaka

"Katika mkutano huo, inaaminika kuwa Nyerere alipinga azimio hilo kwa nguvu zake zote na kulazimisha viongozi wa CCM na serikali kutafuta mwanya wa kuacha kutekeleza azimio.

"Kutokana na upinzani mkali kutoka kwa Nyerere, viongozi wa CCM walilazimika kurekebisha katiba ya chama chao (CCM) Ibara ya 8 na ya 12 ambazo zilimruhusu Mwenyekiti wa CCM kuitisha mkutano Novemba, 1993... Lengo la mkutano huo lilikuwa kutafuta njia ya kuua Azimio la Bunge ingawa ilitangazwa kuwa ni mkutano wa kutafuta njia bora ya kutekeleza Azimio," anasisisita Kasaka.

Kutokana na madaraka aliyopewa kwa mujibu wa mabadiliko ya katiba ya CCM, Mwinyi aliitisha mkutano Kilimani Club Novemba 12 hadi 14, 1993 uliohudhuriwa na wabunge wote wa Bunge la Tanzania, Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa NEC.

Licha ya kwamba mwenyekiti wa mkutano alikuwa Mwinyi, Kasaka anasema Nyerere ndiye alikuwa msemaji mkuu na katika hotuba yake alionyesha ameudhika huku akiweka bayana kwamba azimio la bunge kuhusu kuundwa kwa Tanganyika lilitokana na mambo mawili.

Kwa mujibu wa Kasaka, mambo hayo ni msukumo wa chuki kwa Wazanzibari na kichinichini chuki kwa Uislamu huku akisisitiza kuwa Tanganyika ikiundwa kwa msukumo wa mambo hayo Tanzania haitabaki.

Pia Nyerere, kwa mujibu wa Kasaka, alizungumza kwa kirefu kwamba hoja ya Tanganyika ilipingana na sera ya CCM ya serikali mbili na kwamba sera ni suala la CCM na si bunge, hivyo ubadilishaji wa sera hufanywa na chama na bunge hupelekewa ili litunge sheria kwa ajili ya utekelezaji.

Sambamba na hilo, Nyerere aliwalaumu viongozi wa CCM na serikali kwa kushindwa kuzuia hoja hiyo kupitishwa na bunge huku akimshutumu Malecela kwa kile alichodai kuwa kukosa msimamo na kwamba kwa hilo, kwa mujibu wake (Nyerere) lilikuwa kosa kubwa.

**• Nini kilitokea baada ya hotuba ya Nyerere? Fuatilia kwa undani kwenye kitabu hicho na makala itakayofuata.**

# Ya Profesa Lipumba CUF yana mafunzo mengi

Na Mwandishi Wetu

TANGU mwaka 2015 mpaka sasa, Profesa Ibrahim Lipumba, amehusika na hatua kadhaa zinazohusu Chama Cha Wananchi (CUF) na kupelekea kufikiwa maamuzi mengi mojawapo ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Seif Sharif Hamad, kuhamia ACT-Wazalendo, wiki iliyopita.

Hatua hiyo imetoa mafunzo kadhaa kwa yale wanayofanya wanasiasa iwe Tanzania na duniani. Miongoni mwa mafunzo hayo ni haya yafuatayo:-

Mosi ni ukiwa na hasira usifanye maamuzi mazito.

Profesa Lipumba alipoamua kuacha uenyekiti wa CUF, alikuwa na hasira kali dhidi ya kilichomfanya achukue uamuzi huo, ndiyo maana katika mkutano wa hivi karibuni uliomchagua kuwa Mwenyekiti wa CUF mapema mwezi huu, alisema alipata hasira na kutamani kurusha ngumi.

Anaeleza kuwa kilichomfanya atamani kupigana ni kwa sababu Hammad, alisema CUF haijajipanga kuwa na mgombea wa urais wa mwaka 2015, hivyo jukumu hilo lichukuliwe na Chadema.

Aidha, anadai kilichomuudhi zaidi ni kutokuridhishwa na ujio wa Edward Lowassa, ndani ya Umoja ya Katiba ya Wananchi (Ukawa) na kupewa nafasi ya kuwa mgombea urais.


Pengine, angeiruhusu kwanza hasira ipite kisha kutafakari hatua ya kuchukua, angeweza kufanya uamuzi ambao usingeleta mkanganyiko wa leo. Angeweza kuomba mapumziko ya siku kadhaa kufanya utafiti wa kiuchumi. Angekuwa anarudi kwenye kazi zake napengine CUF isingesambaratika.

Hili ni funzo kwa wanasiasa kwa mambo yote, kwa mfano hata unapopokea ujumbe wa simu au wa barua pepe wa kukukera usiujibu mara moja. Tuliza hasira na ikitulia utashughulikia suala hilo kikamilifu. Kujibu haraka haraka katikati ya hasira kunaweza kukufanya ukaandika lugha kali inayoweza kukugeuka baadaye.

Pili, si vyema kusema mambo mapema. Usiliweke jambo hadharani kabla ya kufanya tafakari na hatua unayokusudia kuichukua

Baada ya kufanya uamuzi kwa hasira, mara moja Profesa Lipumba aliutangaza uamuzi huo kuwa anaondoka kwenye wadhifa wa uenyekiti na akieleza sababu mahsusi ya uamuzi huo.

Ingekuwa jambo jema kama angejipa muda wa kutafakari kabla ya kutangaza. Asingeweka kila hisia yake hadharani. Angetumia hoja ya kwenda kutumia taaluma yake kutafakari kwa kina mambo ya kisiasa yaliyokuwa yamemkabili.



Profesa Ibrahim Lipumba. **PICHA:MTANDAO**

Hili liwafundishe wanasiasa kuwa ukiwa na jambo lako zito dhidi ya wanasiasa wa karibu usiweke kila kitu wazi. Kama kuna matatizo ndani ya chama ni vizuri wahusika wakatoa muda ili hasira itulie, hakuna sababu ya kutangaza mlivyoumizana. Ukifanya hivyo unaweza kumdhalilisha mwenzio na siku mkipatana na kupendana upya zaidi ya pale mwanzo, utakuwa umemdhalilisha vibaya kwa watu uliowaeleza mabaya yake kipindi cha mgogoro wenu.

Kumbuka, kwenye siasa hakuna adui wa kudumu wala rafiki wa siku zote. Pia ni vizuri kukumbuka kuwa Ukishaamua jambo baada ya kuridhika na usahihi wake usibadili msimamo hata kama ukigundua ulikosea kufanya uamuzi.

Ukifanya kosa la kufanya mamas katikati ya hasira uamuzi wa kukosewa kisha ukautangaza uamuzi huo, basi kubaliana na matokeo. Chukua mkondo mwingine wa maisha badala ya kurudi nyuma kutakakokushushia hadhi.

Suala jingine la kujifunza ni kutekeleza jambo kwa kufuata mlolongo uliopitia kulifanya jambo hilo ama kuchukua hatua.

Mathalani, ukifanya jambo la kiofisi kupitia ofisi fulani, endelea kufanya mawasiliano na ofisi hiyo hiyo kwa kila jambo linalohusu suala husika.

Hii huondoa mkanganyiko na kulinda usahihi wa kumbukumbu. Profesa Lipumba aliandika kwa Katibu Mkuu wa CUF barua ya kujiuzulu uenyekiti. Alipaswa aandike barua ya kubadili mawazo hayo kwa huyo huyo Katibu Mkuu wa CUF.

Kumwandikia Msajili wa Vyama barua kueleza kuhusu kubadili msimamo kama alivyofanya pengine haikuwa sahihi. Ikumbukwe kuwa awali alieleza kuwa alimuandikia barua Msajili wa Vyama kutengua uamuzi wake wa kujiuzulu. Japo kulikuwa na maelezo mengine kwamba aliandika barua ya utenguzi kwa Katibu Mkuu. Hata hivyo, yamepita la msingi ni kujifunza kutokana na yaliyopita.

Jambo jingine ni kulinda hadhi ya mamlaka rasmi kwa kutoonyesha kujua ilichoamua kabla ya uamuzi kutolewa.

Tarehe 28, Agosti 2016, Profesa Lipumba alieleza kuwa yeye ni Mwenyekiti halali wa CUF kwa sababu aliandika barua kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kufuta uamuzi wa kujiuzulu. Kama aliandika barua ya kuomba jambo, hakupaswa kusema amepata wadhifa wa kuwa Mwenyekiti halali, hata kabla ya kujibiwa barua yake. Kufanya hivyo kunawafanya watu wafikirie zaidi dhidi ya taratibu zilizofanyika.

Barua ya Profesa Lipumba ilijibiwa na Msajili Septemba 23, 2016, ikihalalisha uenyekiti wake, siku 26 baada ya yeye kuonyesha kwamba jibu alikuwa nalo kuwa yeye ni Mwenyekiti halali.

Hii iliwafanya wanasiasa na wana CUF kufahamu kuwa Profesa alijua matokeo ya ombi lake hata kabla halijajibiwa. Katika maisha yoyote, usianze kusema ya moyoni ambayo pengine hayakutakiwa yatoke hadharani. Hii itafanya mamlaka uliyoonyesha imekupendelea isiaminike tena kwa maamuzi yoyote mengine kwa kuonekana kuwa mamlaka yake inaweza kufanya ndivyo sivyo. Maamuzi rasmi ya kisheria hayatekelezwi kwa nguvu na mabavu. Hili ni jambo la kujifunza pia.

Ikizingatiwa kuwa Profesa Lipumba alirudishiwa uenyekiti wake rasmi kisheria kwa nguvu ya mamlaka rasmi kisheria, kuingia kwake ofisini kulipaswa kufanywa kisheria kwa nguvu ya sheria na wala si kwa nguvu ya polisi, kunyang'anya mlinzi silaha na kuruka ukuta. Hii haikuwa sahihi. Kwa sababu kama Profesa angezuiliwa kuingia ofisini, angetumia sheria kuingia na kutekeleza majukumu yake.

Hapa wanasiasa wanapaswa kujifunza kwamba wakiwa na uhalali wote kimadai wanaoupata kupitia maamuzi halali ya vyombo vya kisheria kama mahakama, upande wa pili ukiacha kutekeleza maamuzi hayo hawapaswi kutumia nguvu kuwalazimisha wayatekeleze.

Hapo kuna hatari ya kutenda kosa la jinai linaloweza kusababishia kesi na mwisho adhabu za mahakama. Wanasiasa watumie hatua za kisheria kufanikisha utekelezaji wa maamuzi ya kisheria.

Ni vyema wanasiasa wakajifunza kupitia mambo ya Profesa Lipumba tangu kujiuzulu mpaka kurudishiwa mamlaka rasmi kwenye nafasi aliyojiuzulu kwa hiari yake na waone athari ya mambo hayo kwa mkanganyiko uliotokea sasa. Watumie mafunzo hayo kuweka sawa mambo yao ndani ya siasa na nyanja tofauti za maisha.

MAKALA

# Saudia yawekeza vitega uchumi kimkakati Pakistan na China

**Na Nimi Mweta**

MABADILIKO ya kina yanaanza kuonekana katika mwelekeo wa Saudi Arabia kutokana na uhasama unaoendelea na nchi za Magharibi licha ya juhudi za Rais Donald Trump wa Marekani kulinda uhusiano na Saudia ili usizorote, bunge la nchi hiyo limepania kupata ukweli wa mauaji ya kinyama ya mhariri na mwanasafu maarufu wa gazeti la Washington Post la Marekani, Jamal Khashoggi ubalozini Istanbul nchini Uturuki.

Mwanamfalme Mohammed bin Salman ambaye nafasi yake ni kama Waziri Mkuu wa Saudia alitembelea China mapema mwezi uliopita na kufikia mikataba kadhaa ya kibiashara ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kusafisha mafuta na kutengeneza dawa chenye thamani ya dola bilioni 10. Ni habari njema kwa China wakati uchumi unafifia.

Mwanamfalme huyo alikuwa katika ziara muhimu ya nchi za mashariki ambako alianza kwa kutembelea nchi rafiki ya Pakistan, ambako alifikia mikataba ya biashara yenye thamani ya dola bilioni 20, bila kujali kuwa taifa hilo lilikuwa katika malumbano na mashambilizi ya ndege za kivita baada ya tukio kubwa la ugaidi.

Wachunguzi wa habari walisema kuwa haikuwa inatazamiwa kuwa Mohamed bin Salman angekuwa na fedha nyingi kiasi hicho kwa ajili ya miradi na Pakistan, nchi ambayo kama ilivyo Saudia inaongozwa na itikadi mahsusi ya Uislamu. Makundi ya kijeshi na kigaidi nchini Pakistan kwa sehemu kubwa yana vianzo katika itikadi za Saudia.

Pakistan ilionyesha juhudi ambazo si za kawaida katika kumpa heshima kubwa mwanamfalme Mohammed bin Salman, ikiwa ni pamoja na kupeleka ndege za kivita kuiongoza ndege yake hadi kutua kuanzia wakati ilipoingia anga ya Pakistan.

Hatua hiyo ni pamoja na kuwa hakuna kikundi chochote cha kigaidi kinachohofiwa kuwa na mipango ya kufanya shambulio dhidi ya Saudia, hata ingekwa ni vikundi vinavyoungwa mkono na Iran, au hata vya upinzani nchini Yemen.

Kwa upande mwingine, serikali ya Waziri Mkuu Imran Khan ilitazamia kwa kiasi fulani kuwa uhusiano mzuri na Saudia, au kuonyesha heshima kwa Mwanamfalme, kutapunguza uhasama na makundi ya kigaidi, hivyo kutoa nafasi kwa utawala huo kutafuta njia za kupunguza kiwango cha mafarakano.

Waziri Mkuu Imran Khan na Mkuu wa Majeshi Qamar Javed Bajwa, walisalimiana na Mohammed bin Salman katika uwanja wa ndege wa kijeshi wa Rawalpindi, halafu Waziri Mkuu Khan, mwenyewe akaendesha gari la mgeni wake kwenda mji mkuu wa Islamabad.

Alisifu uhusiano wa Pakistan na Saudia kuwa nchi hiyo wakati wote imekuwa ni rafiki wa kweli Pakistan inapokuwa katika matatizo na ndiyo maana nchi hiyo inaithamini sana Saudia. Wachunguzi wa habari wanasema kuwa hivi karibuni Saudia iliingiza kiasi cha dola bilioni sita kujazia akiba ya fedha za kigeni ya Pakistan kwa mkopo, kuipatia nafasi ya kupumua nchi hiyo ikitafuta mkopo Shirika la Fedha la Kimataifa, IMF.



Waziri Mkuu Imran Khan wa Pakistan (kushoto) na Mwanamfalme Bin Salman. **PICHA: MTANDAO**

> Ni hatua kubwa na sehemu ya kwanza tu na bila shaka itakua kila mwezi na kila mwaka, na itakuwa na manufaa kwa nchi zote mbili,"

Wachunguzi wanasema ziara ya Mohammed bin Salman nchini Pakistan ni ya pili kwa umuhimu wa kitaifa nchini humo tangu kutembelewa na Rais Xi Jinping wa China mwaka 2015, ambaye alitangaza mpango wa uwekezaji unaogharimu mabilioni ya dola. Ni sehemu ya mkakati mpana wa China unaoanzia Mashariki ya Mbali hadi kingo za Bahari ya Atlantiki kwa upande wa magharibi.

Saudia itajenga kiwanda cha kusafisha mafuta pamoja na kutengeneza dawa kutokana na mabaki ya petroli katika jiji la Gwadar nchini Pakistan, ambako tayari China inajenga bandari ya kisasa. Yako pia makubaliano ya uwekezaji katika sekta za madini na kilimo. Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Khan, akiainisha kuimarishwa zaidi kwa uhusiano huo wa jadi.

Wakati wachambuzi wa nchi za Magharibi wanaona ziara hiyo ni sehemu ya juhudi za mwanamfalme huyo kujenga haiba yake kutokana na dhoruba ya kuuawa mwandishi/mhariri huyo nguli Khashoggi, baadhi ya wadadisi wanaona ishara tofauti.

Kwa mfano ziara ya Mohammed bin Salman nchini Pakistan na China ilitazamiwa kuwa na safari nyinginezo ya kutembelea Malaysia na Indonesia, ambapo pia ni nchi kubwa za Kiislamu, lakini hatua hizo za ziara yake ziliahirishwa hadi baadaye. Ina maana kuna mwelekeo maalum wa mahusiano na uwekezaji kwa upande wa Saudia, kuanza kupunguza kimkakati uhusiano wake na nchi za Magharibi.

Akionyesha wazi kuwa hakuja tu kutoa misaada au kufikia ushirikiano wa hapa na pale bali kuanzisha mkakati wa muda mrefu na wa kina, Mohammed bin Salman alisema kuwa miradi hiyo ya dola bilioni 20 ni mwanzo tu wa ushirikiano wa kiuchumi ambao utazipeleka nchi hizo zinazoshirikiana kwa jadi kuwa karibu zaidi katika uchumi.

"Ni hatua kubwa na sehemu ya kwanza tu na bila shaka itakua kila mwezi na kila mwaka, na itakuwa na manufaa kwa nchi zote mbili," alisema mwanamfalme, kana kwamba hakuwa tayari kutoeleweka kina cha nia za Saudia katika suala hilo. Pia mwanamfalme alikuwa akijisikia vizuri akitaja kuwa nchi hizo zimeshirikiana katika wakati wa furaha na mgumu, kwani katika mazingira ya sasa Saudia inahitaji sauti tofauti na misakamo kadhaa.

Yako maeneo mengine katika mazungumzo kati ya viongozi wa Pakistan na Saudia ambayo wadadisi wa habari hapa na pale wangepata taabu kuelewa ni nini kinatafutwa, kwa mfano mstaalamu wa masuala ya kimataifa wa Pakistan, Mosharraf Zaidi, akisema kuwa kinachotokea ni kuthibitishwa upya kwa dhamira ya Pakistan ya kusaidia kuilinda familia ya kifalme ya Saudia na mpangilio mzima wa kijamii kama ulivyo nchini Saudia, hali au kauli inayomaanisha kupuuza sauti za nchi za Magharibi kutaka kuwajibishwa mwanamfalme Mohammed bin Salman kuhusiana na mauaji ya mhariri Khashoggi yaliyofanywa na maofisa usalama wa Saudia, anaowatuma.

Mtaalamu huyo anaonyesha pia kuridhika kwake na uwezekano mkubwa wa Saudia kushiriki kikamilifu katika kupanua uwekezaji nchini Pakistan, wakati ambapo mwanamfalme Mohammed bin Salman alikutana pia na viongozi wa kundi la Taliban nchini Afghanistan.

Lengo la majadiliano hayo lilikuwa ni kutafuta msingi wa kurudisha amani nchini humo baada ya vita viliyoanza kwa ulipuaji wa majengo marefu jijini New York kwa ulipuaji wa ndege uliosimamiwa na kundi la kigaidi la Al Qaeda likisimamiwa na Osama bin Laden, aliyefia Pakistan katika shambulio la kikomandoo la jeshi la baharini la Marekani mwaka 2011.

Baadhi ya wadadisi wanadhani kuwa Saudia na hasa mwanamfalme Mohammed bin Salman anaweza kupiga hatua kwa kiwango fulani katika jitihada hiyo, ambayo imeishinda Marekani tangu iuondoe utawala wa Taliban mwisho mwa mwaka 2001.

Rais Donald Trump alitangaza mkakati wa kuondolewa nusu ya askari wa Marekani huko Afghanistan tena kwa haraka.

# Wanafunzi waomba wadau kusaidia ujenzi wa bweni

**Na George Tarimo,** IRINGA

WANAFUNZI wa kiume katika Shule ya Sekondari Mlowa wilayani Iringa, wameiomba serikali na wadau kuwajengea bweni ili kuwasaidia kupata muda wa kusoma tofauti na sasa ambapo wanatumia muda mwingi kufanya kazi za nyumbani kutokana na kupanga mitaani wanakoishi kwa kujitegemea.

Wakizungumza na Nipashe shuleni hapo baada ya kumalizika kwa zoezi la kukabidhi bweni la wasichana lililokarabatiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Lyra in Afrika baada ya kuungua mwaka jana baadhi ya wanafunzi hao wamesema wamefurahi bweni hilo kukarabatiwa, lakini wakaomba wadau na serikali kufikiria kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wote kwa kuwa shule nyingi ziko mbali, hivyo wanafunzi hulazimika kuhama nyumbani na kupanga mitaani.

Wakizungumza baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo akiwamo, Victor Chatanda na Modestus Lwena, wamesema kuwa wakiwa nyumbani wanafanya kazi nyingi tofauti na wakiwa shuleni.

Mkurugenzi wa shirika hilo Roseline Marick amesema shirika hilo wameamua kukarabati bweni hilo la wasichana katika Shule ya Sekondari Mlowa ukiwa ni mwendelezo wa mpango wao wa kuhakikisha wasichana wanapata fursa ya kusoma kwa kuwaepusha na vishawishi wanapotembea umbali mrefu kwenda shuleni au kupanga mitaani.

"Tuna imani kubwa kwamba kila binadamu ana uwezo mkubwa, lakini tunapata fursa tofauti katika maisha yetu na pia tunapitia changamoto tofauti na kama shirika tulianzisha mfumo wa kujifunza kidijitali," alisema Mariki.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, amewaomba wazazi wakiwamo wazee wa mila ya Kimasai wanaoishi katika eneo hilo kuwakanya vijana wao wanaoendeleza mila za kutorosha wasichana hasa wanafunzi kwa kufanya hivyo ni kuharibu maisha ya wasichana hao.

# Polisi yanasa waganga kienyeji kutoka Malawi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu 21 wakiwamo wafanyabiashara kutoka nchini Malawi kwa tuhuma za kufanya matukio mbalimbali ya uhalifu ikiwamo shughuli za uganga wa kienyeji bila kibali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, aliyasema hayo jana ofisini kwake na kudai kuwa watuhumiwa walikamatwa kwa nyakati tofauti baada ya askari wa jeshi hilo kufanya msako katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Taarifa ya Kamanda Matei ilifafanua kuwa katika Kitongoji cha Mwambuluko, wilayani Kyela, Jeshi la Polisi walikamata gari moja lenye namba T. 268 BNH aina ya Mitsubishi Fuso Truck likiwa limebeba magunia 88 yenye mahindi makavu mali ya Dorin Kaongo (35) na Glory Kafwila (32) wafanyabiashara kutoka wilayani Karonga nchini Malawi.

**Gari hilo lilikuwa likielekea kivuko haramu cha Nyasa kilichopo Mto Songwe mpakani mwa nchi ya Tanzania na Malawi kwa ajili ya kuyavusha.**

Alisema gari hilo lilikuwa likielekea kivuko haramu cha Nyasa kilichopo Mto Songwe mpakani mwa nchi ya Tanzania na Malawi kwa ajili ya kuyavusha magunia hayo ya mahindi kwa mitumbwi kuelekea nchi hiyo jirani ya Malawi.

Aliongeza kuwa katika Kitongoji cha Mapinduzi B Kata ya Itewe wilayani Mbeya Jeshi la Polisi walimkamata Paschal Patrice (30) na wenzake 19 waki-



fanya shughuli ya uganga bila kibali.

Watuhumiwa wote wakiwamo wanawake watatu walikutwa wakiwa kwenye nyumba ya mtu aliyefahamika kwa jina moja la Mwarabu mkazi wa Dar es Salaam wakipatiwa matibabu.

"Jeshi la Polisi lilifanya upekuzi ndani ya nyumba hiyo ya Mwarabu na kufanikiwa kupata begi ambalo ndani yake likiwa na kibuyu kimoja, chupa mbili za plastiki zenye unga unaodhaniwa kuwa ni dawa za kienyeji, kikopo cha plastiki cha njano chenye unga unaodhaniwa kuwa dawa za kienyeji zinazotumiwa na waganga kutolea tiba pamoja na ngoma moja na upelelezi unaendelea," alisema Matei.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe akisalimiana na Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, alipotembelea banda la benki hiyo jana, kabla ya ufunguzi wa jukwaa la tisa la fursa za biashara na uwekezaji mkoani Lindi. Benki ya NMB ni mdhamini wa jukwaa hilo linalofanyika kwa siku tano mkoani Lindi. **PICHA: NMB**

# Wadau masuala ya ukatili kijinsia waweka mikakati

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WADAU wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Mbeya wameweka mpango mkakati katika mwaka huu 2019, kukabiliana na vitendo hivyo ili jamii iendelee kuwa salama.

Wakizungumza juzi kwenye kikao cha kujadili na kuweka mkakati wa kutokomeza vitendo hivyo ambacho kilihusisha Mahakama, Wizara wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi na Idara ya Maendeleo ya Jamii walisema ni wakati mwafaka wa kupaza sauti.

Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Janeth Masagano, alisema kuwa lengo la mpango huo ni kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni vya ubakaji, ulawiti na vipigo.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa wahanga wa matukio hayo kuna changamoto ya watu hao kutotoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

"Kuna changamoto kubwa ya vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto mbaya zaidi hawatoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi wanawakumbatia watuhumiwa kutokana na mahusiano waliyonayo kwenye familia zao naomba tubadilike," alisema Janeth.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Anna Gloria Gereta, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea watoto wengi ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili.

Alisema miongoni mwa vitendo vinavyoripotiwa ni ulawiti kwa watoto wakiume na wa kike na kwamba wanapohitaji ushirikiano kutoka kwa wazazi wanakosa.

Alisema licha ya hospitali hiyo kupokea watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo alidai mpango mkakati huo waliokubaliana katika kikao hicho utaleta tija kwa kuwa wataendelea kutoa elimu kwa kuwashirikisha wazazi na walezi.

Hata hivyo Annagloria alisema wananchi wanaendelea kupata elimu dhidi ya vitendo vya ukatili katika Mkoa wa Mbeya kwa kuwa vinaendelea kupungua.





# Mabilioni yatengwa kukarabati barabara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIKA mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Barabara (Tanroads), Mkoa wa Dodoma, umeomba Sh. bilioni 19.17 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 1,692.26.

Hayo yalielezwa jana na Meneja wa Tanroads mkoani humo Mhandisi Leonard Chimagu katika kikao cha Bodi ya Barabara, jijini hapo.

Alisema fedha hizo pia ni kwa ajili ya matengenezo ya madaraja 298 kwa barabara kuu na mkoa.

Akizungumzia hali ya barabara za Dodoma, Chimagu alisema kuwa sehemu kubwa ya mtandao wa barabara uko katika hali nzuri isipokuwa barabara ambazo zilipandishwa hadhi mwaka 2010 kutoka barabara za wilaya na kuwa za mkoa zenye jumla ya kilomita 438.53 ambazo ukarabati wake unaendelea ili ziweze kupitika.

**Mapendekezo ya mpango wa mwaka 2019/20 yanahusisha mipango kazi ya matengenezo inayogharamiwa na Mfuko wa Barabara.**

Aidha, alisema Desemba 201, hadi Novemba 2018, barabara nyingi ziliharibika na mvua hali iliyosababisha baadhi ya maeneo kutopitika au sehemu nyingine kupitika kwa shida.

“Hadi kufikia Februari 2019, matengenezo ya kurudisha mawasiliano yamekamilika isipokuwa barabara ya Mpwapwa-Makutano-Pwaga-Lumuma-daraja la Godegode lilivunjika na barabara ya Mbande-Kongwa-Suguta daraja la mfuto la Ibwaga lilisombwa na maji sehemu hizi bado hazipitiki,” alieleza.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini(Tarura), Mhandisi Lusako Kilembe, alisema wakala huo unahitaji Sh.bilioni 12.63 kugharamia kazi mbalimbali za matengenezo ya barabara zilizo chini ya wakala huo.

Alisema mapendekezo ya mpango wa mwaka 2019/20 yanahusisha mipango kazi ya matengenezo inayogharamiwa na Mfuko wa Barabara.

Hata hivyo alisema kutokana na ukomo wa bajeti ni finyu na kwa mujibu wa maelekezo elekezi, vipaumbele vilitumika katika kuainisha barabara zitakazoingia katika mpango ni masuala ya kijamii, kiuchumi na kiufundi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mundemu wilayani Bahi, mkoani Dodoma, wakitengeneza taulo za kike (pedi) za asili kwa kutumia vitambaa, inaelezwa kuwa upatikanaji wa pedi katika shule hiyo umechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mahudhurio shuleni. **PICHA: PAUL MABEJA**

## NBS yabaini upungufu takwimu mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imesema kumekuwa na upungufu wa takwimu za mazingira kwa asilimia 60 nchini.

Hayo yalielezwa jana na ofisa kutoka NBS, Benedict Mugambi, katika semina ya kitaifa ya wadau kuhusu uanzishwaji wa ushirikiano wa kitaifa na kimataifa wa uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa takwimu za mazingira, jijini hapa. Alisema lazima ukusanyaji wa takwimu za mazingira ufanyike kabla ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

“Kuna tofauti ya asilimia 60 ya takwimu za mazingira, tunafanya uchaguzi, lakini bado tuna ‘gap’ kwenye takwimu za mazingira, tunafanya sensa kuna ‘gap’, hili linabidi lifanyike kabla ya sensa 2022, ili kuwasaidia watunga sera kuwa na maamuzi sahihi,” alisema.

Akielezea umuhimu wa takwimu hizo, Mugambi alisema kuna baadhi ya maeneo wamefanya majaribio kwenye mikoa mbalimbali ikiwamo Ziwa Manyara, ambapo kwa takwimu walizokusanya inaonyesha maji hukauka katika eneo hilo.

“Katika Ziwa Manyara tunaona kwa mwaka 2017 lilipoteza maji kwa asilimia 57.8 na kuna hatari maji kukauka kabisa na kutokana na kuonyesha kuwa na madini kama vile urani, watu wataanza kuchokonoa eneo hilo,” alisema.

Hata hivyo, alisema kwa Jiji la Dar es Salaam walishazungumza na viongozi wa mkoa huo na kuonyesha athari zilizopo ikiwamo maeneo ya Mto Msimbazi yanayopakana na msitu wa Kazimzumbwi ni hatari mvua zikinyesha. Kwa upande wake, Mkurugenzi wa NBS Dk. Albina Chuwa, alisema tatizo la upatikanaji wa takwimu hizo si kwa Tanzania peke yake bali ni la kiulimwengu.

Alisema wanajipanga kukusanya takwimu za mazingira zitakazowezesha kutunga sera za uhifadhi na ulinzi wa mazingira nchini.

# Mradi wa kusoma, kuandika watu wazima waja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Biblia Tanzania, kimeanza utekelezaji wa mradi wa kujifunza kusoma na kuandika kwa watu wazima waliokosa fursa hiyo kutokana na sababu mbalimbali, katika vijiji 30 vya wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, ikiwa ni sehemu ya kuunga juhudi za serikali katika kupambana na adui ujinga.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mahafali ya kwanza yaliyojumuisha wahitimu 97 wa elimu ya watu wazima yaliyofanyika katika kijiji cha Berega wilayani humo, Mratibu wa Mradi huo, Frank Makala, alisema kuwa lengo ni kuwasaidia kujua kusoma na kuandika wote waliokosa fursa hiyo awali.

Alisema kuwa wahitimu hao 97, ni sehemu ya 120 ambao ndiyo walijiandikisha kujiunga na elimu ya watu wazima ya kusoma na kuanadika mwezi Septemba mwaka jana, ambao wachache kati yao walishindwa kufika mwisho kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo hali ya kiuchumi.

“Hawa wahitimu wanaomaliza leo ni kutoka katika vijiji 10, ambavyo ndivyo tulianza navyo katika mradi kama awamu ya kwanza na leo 97 wameanza kuhitimu na wote wanajua kusoma na kuandika wengine wachache wamekosa kufika siku ya leo kutokana na hali za kiuchumi kwa kuwa wengine walilazimika kwenda katika shughuli zao za kilimo ili kujitafutia riziki,” alisema Makala.

Makala aliongeza kuwa mradi huo wa kusoma na kuandika unatoa mafunzo kwa kutumia lugha mama ya Kikagulu ili kuweza kuwawezesha wanafunzi kuelewa kwa wepesi.

“Tunatumia lugha mama ya Kikagulu katika kufundisha na hii imetusaidia sana kuweza kuwafundisha wanafunzi hawa ambao ni watu wazima ambao wengi wao walikuja hawajui lolote, lakini kwa kipindi cha miezi sita kila mmoja anajua kusoma na kuandika kwa lugha yake ya kuzaliwa ambayo ni Kikagulu lakini pia wakati huohuo na Kiswahili,” alisema.

Alifafanua kuwa madarasa mengine katika awamu ya pili yanatarajia kuanza mwezi Aprili mwaka huu, ambapo vijiji vingine 10 vitahusishwa na baadaye mwezi Mei vijiji vingine 10 na wanatarajia hadi ifikapo Novemba 2019, kuwa na jumla ya vijiji 30, ambavyo vimefikiwa na mradi huo.

Mwakilishi wa Askofu wa Kanisa la Agrikana Tanzania Dayosisi ya Morogoro, Canon Isack Mgego, akizungumza katika mahafali hayo alisema wao kama kanisa wanajisikia faraja kuwa sehemu ya kuwawezesha Watanzania katika kupambana na adui ujinga.

“Adui ujinga ni moja kati ya maadui ambao taifa letu linapambana nao na sisi kama kanisa tunayofuraha leo kuwezesha watu kujua kusoma na kuandika ili waweze kuondokana na umaskini ambao umekuwa ukiwakabili,” alisema Mgego.



# Kangi Lugola avionya vyama vinavyopiga siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amesema kuna baadhi ya vyama vya siasa vimekuwa vikikiuka taratibu kwa kufanya mikutano ya hadhara jambo ambalo limeshapigwa marufuku na serikali.

Waziri huyo aliyasema hayo katika viwanja vya Komba mjini Zanzibar katika mkutano wa wazi kati ya watendaji wa serikali na wananchi katika kueleza changamoto zinazowakabili na kuweza kufanyiwa kazi.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo waziri huyo, aliliagiza Jeshi la Polisi kushughulikia chama chochote cha siasa ambacho kitakachokiuka taratibu ikiwamo kufanya mikutano ya hadhara.

"Naliagiza Jeshi la Polisi kupitia kwa kamshna kuwashika wale wote ambao wanakiuka taratibu kwa kufanya mikutano ya hadhara na kutishia amani na utulivu uliopo nchini," alisema.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona serikali imezuia mikutano ya kisiasa, lakini kuna kundi linaonekana kufanya mikutano hiyo bila ya kuwa na hofu.

Aliongeza kuwa haikubaliki hata kidogo kuona kauli ya serikali kupingwa kwa maslahi ya watu wachache, na kusema kuwa yuko tayari kuhakikisha anatumia gharama za kusambaratisha makundi hayo.

"Kuna wengine wanafanya mikutano ya wazi wazi Unguja na hivi sasa naskia kuna baadhi ya video zinaonyesha wakiwa kisiwani Pemba, nasema kwamba wanachofanya ni kinyume na sheria na nitahakikisha tunawashughulikia," alisema.

Aidha, alisema licha ya kufanya mikutano ya hadhara kinyume na sheria, lakini pia ni jambo la ajabu kuona wanaharibu baadhi ya vitu ikiwamo bendera za chama.

Alisema kufanya hivyo pia ni kosa, kwa kuwa kuhama au kufukuzwa chama si sababu ya kuharibu vitu vya chama ulichohama kwa sababu zisizo na msingi.

Waziri huyo alimwagiza Kamishna wa Polisi Zanzibar, Mohamed Haji Khamis, kuhakikisha anatumia nguvu zake zote za kiaskari katika kuhakikisha makundi hayo yanatokomezwa mara moja.

Alisema haiwezekani hata kidogo kuona Zanzibar kuna Jeshi la Polisi kisha wakatokea watu wakaona kama hakuna vyombo vya ulinzi, huku wakiendelea kufanya wanavyotaka wao.

Alisema Zanzibar ni nchi iliyo na amani na itaendelea kuwa na amani chini ya usimamizi wa Rais wake Dk. Ali Mohamed Shein.

Naye Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema mikakati imara iliyopangwa na Jeshi la Polisi Zanzibar ni moja ya mambo yaliyosababisha hali ya amani na utulivu kuendelea hadi wakati huu.

# Spika Ndugai azungumzia maandalizi uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Job Ndugai, amewataka wanachama na viongozi wa chama hicho visiwani Zanzibar kuendeleza harakati za kuandaa mazingira rafiki ya kukipatia ushindi mwaka 2020.

Aliyasema hayo mjini Zanzibar katika ziara ya kutembelea mikoa miwili ya kichama ambayo ni Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kusini Unguja.

Ndugai ambaye ni mlezi wa mikoa hiyo, alisema kila mwanachama anatakiwa kujipanga kuhakikisha CCM inaendelea kubaki madarakani kwa ridhaa ya wananchi.

Aidha, aliwashukuru viongozi na wanachama wa CCM wa mikoa hiyo kwa mapokezi makubwa jambo aliloeleza kuwa hali hiyo imemwongezea ari, hamasa na ujasiri wa kufanya ziara yake kwa ufanisi mkubwa.

**Kila mwanachama anatakiwa kujipanga kuhakikisha CCM inaendelea kubaki madarakani kwa ridhaa ya wananchi.**

Aliwataka wanachama wa mikoa hiyo kuendeleza sifa na heshima ya maeneo yao yanayosifika kwa kuwa ngome imara za Chama Cha Mapinduzi. Alieleza kuwa CCM inaendelea kuimarika kisiasa, kiuchumi, kidemokrasia na kimfumo, huku baadhi ya vyama vya siasa vikiendelea kudhoofika kisera na kisiasa.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, alimwakikishia mjumbe huyo wa kamati kuu ya CCM na pia ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa hali ya kisiasa katika mikoa anayoilea ipo shwari kutokana na historia nzuri ya maeneo hayo ambayo ndio yenye azma kubwa ya mtaji wa kisiasa wa CCM.

Alisema kuwa jukumu la ulezi wa mikoa ni kubwa, hivyo anaamini kuwa Job Ndugai atafanya ziara yake hiyo ya kujitambulisha kwa wanachama pamoja na kuwapatia nasaha mbalimbali za kuwaongezea hamasa ya kuendelea kuwa wazalendo wa CCM na taifa kwa ujumla.

Ziara hiyo ya Ndugai ni ya siku tatu atatembelea maeneo mbalimbali na kuzungumza na wanachama kupitia vikao vya ndani sambamba na kukagua miradi iliyotekelezwa kupitia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020.



Spika wa Bunge na Mlezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kusini Unguja na Kaskazini Unguja, Job Ndugai (wa pili kulia), Wajumbe wa Kamati Kuu Zanzibar, Wajumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, wenyeviti wa mikoa, wenyeviti wa wilaya na maofisa wa CCM wakisali kwa pamoja kwenye kaburi la aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume, jana katika ziara ya kikazi visiwani humo. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# RC ashauri mgawanyo fedha za bajeti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, ameishauri Kamati ya Kilimo, Biashara na Fedha ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuangalia mgawanyo wa bajeti kwa serikali za mitaa kwa kuzingatia idadi ya watu katika kila mkoa pamoja na mahitaji yao.

Alisema mkoa wake kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, una idadi ya watu 597,000, sawa na asilimia 49 ya watu wote wa Zanzibar, hivyo kuupatia bajeti sawa na mikoa mengine ambayo haina idadi kubwa ya wakaazi imekuwa ni changamoto kubwa katika suala la kiutendaji.

Mkuu wa Mkoa huyo aliyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo ya Baraza la Wawakilishi iliyofika ofisini na kukagua miradi ya maendeleo katika mkoa huo.

Alisema licha ya udogo wa ardhi katika mkoa huo, lakini una idadi kubwa ya watu, hivyo amependekeza bajeti ya maendeleo zinazokwenda katika Serikali za Mitaa, angalau asilimia 48 zingekwenda kwenye mkoa huo.

Aidha, aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kulipa kipaumbele suala la miundombinu zikiwamo barabara kwa vile nyingi ya barabara hizo ni chakavu.

Akizungumzia kuhusu kilimo na ufugaji, Ayoub alisema Serikali ya Mkoa imeanza kutilia mkazo ufugaji kwa kuunda vikundi vya ushirika vya ufugaji vya vijana na kunasibisha miradi hiyo na kukuza ajira kwa vijana.

"Hivi karibuni mimi mwenyewe nikiambatana na viongozi wa Mabaraza ya Manispaa tulifanya ziara maalum Tanzania Bara ili kujifunza namna watakavyoweza kuimarisha sekta ya ufugaji kwa Mkoa Mjini Magharibi ikiwa ni mikakati ya kuwasaidia vijana," alisema.

Aliwahakikishia viongozi hao kuwa Serikali ya Mkoa ipo tayari kufanya kazi kwa karibu na kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa kuwa wote lengo lao ni moja la kuwahudumia wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwinyihaji Makame, alisema madhumuni ya ziara yao ni kufuatilia utekelezaji wa mambo waliyoyaahidi mawaziri katika bajeti zao kama wameyatekeleza kama walivyoahidi.

Alisema pia wajumbe wa kamati hiyo watapata fursa ya kuangalia maendeleo ya miradi, mafanikio pamoja na changamoto ziliopo, ambapo maeneo watakayo yatembelea ni utafiti wa mifugo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 25 March**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 26 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 27 March**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 28 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 29 March**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 30 March**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 31 March**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 25 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 26 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 27 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 28 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 29 March**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 30 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 31 March**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


EATV
LEO ASUBUHI SAA 5:00
DADAZ.
JUMATANO
10:59 Jikoni Na Jane
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Mid Week Movie
DADAZ Kipindi kinachompatia mwanamke nafasi ya kuzungumza maswala ya kijamii, afya, siasa na uchumi ambayo yanayoizunguka jamii

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

**CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM**
**FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE**

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Ethiopian Airlines bado wanaimani na Boeing

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

MKUU wa Kampuni ya Shirika la Ndege la Ethiopia, Tewolde Gebremariam, amesema bado anaimani na ndege za Boeing, licha ya kutokea kwa ajali iliyohusisha ndege ya aina hiyo 737 Max, ambayo iliwaua watu 157.

Gebremariam alisema licha ya maafa yaliyolikumba shirika lao la ndege, Boeing na Ethiopian Airlines wataendelea kuwa na uhusiano mwema siku zijazo.

Vilevile, alisema kuwa mfumo wa usalama wa ndege ulikuwa unafanya kazi vizuri kabla ya mkasa wa kuanguka kwa ndege kutokea.

Katika sehemu ya taarifa aliyoitoa jana, Gebremariam alisema: "Tuwe wazi Ethiopian Airlines inaimani na Boeing wamekuwa washirika wetu kwa miaka mingi."

Pia alisema zaidi ya theluthi mbili ya safari za ndege za Ethiopia hufanywa na ndege zilizotengenezwa na Boeing.

Gebremariam alifafanua kuwa Ethiopian Airlines pia imeagiza ndege nyingine zaidi ya Boeing 25 Max 737, baada ya kununua ndege tano.

Ripoti kutolewa wiki hii

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Wizara ya Usafiri ya Ethiopia, Mese Yiheyis, alisema kuwa ripoti ya awali ya uchunguzi kuhusu ajali ya ndege aina ya Boeing 737 MaX 8 ya Shirika la Ndege la Ethiopia inaweza kutolewa wiki hii.

"Inawezekana kutolewa wiki hii, lakini mambo yasiyotabiriwa yanaweza kutokea, siwezi kusema kama itatolewa leo au kesho," alisema Yiheyis.

Wiki iliyopita, Kampuni ya Ndege ya Garuda Indonesia ilisema itafuta mpango wake wa kuagiza ndege za 49 Boeing 737 Max 8 aina ya jet kutokana na wateja wao kukosa imani na ndege za aina hiyo.

Timu ya wataalamu wakiwamo watu kutoka Wizara ya Uchukuzi ya Ethiopia, wanachunguza taarifa kutoka kwenye kisanduku (black box) kilichopatikana kwenye eneo la ajali iliyotokea Machi 10 karibu na Addis Ababa.

Ajali hiyo ni ya pili kutokea kwa ndege za Boeing 737 Max katika kipindi cha miezi mitano baada ya ndege ya Lion Air kuanguka Indonesi Oktoba mwaka jana na kuua watu 189.

Wakati huo huo, Gebremariam aliliambia jarida la Wall Street kwamba mfumo wa kuzuia ajali kwenye ndege ulionekana ukifanya kazi kabla ajali kutokea.

Alisema kuwa bado hajapata taarifa za kisanduku cha kurekodi sauti za ndani ya ndege na chumba cha rubani vilivyo patikana kutoka ndege namba 302 iliyoanguka.

"Ninasema hivyo kwa sababu nilikuwa nimesikiliza mawasiliano kati ya rubani na chumba cha kuongoza ndege kwenye uwanja wa ndege wa Addis Ababa," alisema Gebremariam.

Kwa sasa Boeing inaandaa programu ya kurekebisha mfumo ambao utatakiwa kuidhinishwa na shirika la safari za anga la Marekani ambao umetengenezwa kwa ajili ya kuzuwia ndege kuelekeza uso wake juu hali ambayo inaweza kupoteza uwiano. **BBC**



Familia ikiwa imekimbilia kwenye paa la nyumba yao katika Wilaya ya Buzi, Msumbiji, baada ya nchi hiyo kukumbwa na mafuriko. **PICHA: REUTERS**

# Wizara ya Ulinzi Marekani yaidhinisha fedha ujenzi wa ukuta

**WASHINGTON,** Marekani

WIZARA ya Ulinzi ya Marekani imeidhinisha fedha kiasi cha dola bilioni moja kwenye akaunti ya wahandisi wa jeshi kwa ajili ya ujenzi wa ukuta wa mpakani kati ya Marekani na Mexico.

Fedha hizo ni za kwanza kutolewa chini ya hali ya tahadhari ya kitaifa iliyotangazwa na Rais wa Marekani, Donald Trump ambazo hazikupitishwa na Baraza la Congress. Zitatumika kujenga ukuta wa maili 57.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilieleza kuwa Kaimu Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Patrick Shanahan, alimwagiza kamanda wa kikosi cha Marekani cha wahandisi kuanza kupanga na kutekeleza usaidizi wa dola bilioni moja kwa wizara ya usalama wa ndani na udhibiti wa mipaka na forodha.

Taarifa hiyo ilielezea kuwa sheria ya serikali kuu inaipatia Wizara ya Ulinzi mamlaka ya kujenga barabara na uzio, kuweka taa za barabarani kwa ajili ya kufunga njia baina ya mipaka ya kimataifa na Marekani.

Pamoja na ukuta huo wenye urefu wa futi 18, fedha hizo pia zitatumika katika ukarabati wa barabara na kuweka taa mpya.

Rais Trump alitangaza dharura Februari 15 baada ya Baraza la Congress kukataa ombi lake la kuidhinishwa fedha kiasi cha dola bilioni 5.7 kwa ajili ya ujenzi wa ukuta.

Kwa kutangaza hali ya tahadhari, Rais Trump alipata uwezo wa kutolihusisha Baraza la Congress na kujenga ukuta kwa pesa za jeshi.

Bunge la Wawakilishi linalodhibitiwa na chama cha Democratic lilipitisha azimio la kupinga dharura hiyo mwezi uliopita na wabunge 12 wa chama cha Republican baadaye walijiunga na maseneta wa Democratic kuipitisha katika seneti.

Hata hivyo, Rais Trump alitumia mamlaka aliyonayo kupiga kura ya veto dhidi ya maazimio hayo mapema mwezi huu.

Kwa sasa Baraza la Congress litahitaji kuwa na theluthi mbili ya walio wengi katika mabunge yote kumpiku, jambo ambalo wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema huenda lisiwezekane.

**BBC**



## Bouteflika apata pigo kutoka chama chake

**ALGIERS,** Algeria

CHAMA cha Rais wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika kimekataa mpango wa rais huyo wa kuitisha mkutano wa kitaifa kutafuta suluhu ya vuguvugu la maandamano ya upinzani nchini humo.

Akizungumza kupitia kituo cha televisheni cha Dzair News, Msemaji wa chama hicho (FLN), Hocine Khaldoun, alisema mkutano huo hauna maana tena kwa sababu ungewahusisha viongozi ambao hawakuchaguliwa, na tayari umekataliwa na waandamanaji.

Khaldoun alisema suluhisho la matatizo ya kisiasa ya Algeria yatamalizwa na uchaguzi utakaomweka madarakani rais anayeweza kuzungumza na wananchi.

Hatua hiyo ni pigo kubwa kwa Rais Bouteflika mwenye umri wa miaka 82, ambaye ameonekana hadharani kwa nadra sana tangu alipopata ugonjwa wa kiharusi mwaka 2013.

Kiongozi huyo ambaye alikabiliwa na maandamano ya mwezi mzima, alifuta uchaguzi uliotarajiwa kufanyika Aprili 18, na kuitisha mkutano wa kitaifa ambao ungewashirikisha wawakilishi wa makundi ya wananchi ili kuandaa uchaguzi mpya.

**DW**

## Wabunge Uingereza wapiga kura udhibiti kujitoa EU

**LONDON,** Uingereza

WABUNGE wa Uingereza wamepiga kura juzi usiku, kuchukua udhibiti wa hatua ya Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU) kutoka kwa Waziri Mkuu, Theresa May.

Hatua hiyo ni kujaribu kupata makubaliano yanayokubalika kwa pande zote mbili, Uingereza na EU.

Kura hiyo inamaanisha kuwa kuanzia kesho wabunge watafikiri juu ya kutoa nafasi kwa mapendekezo kadhaa ambayo wanatumai yatakubalika kwa pande zote.

Serikali ya May, imeita hatua hiyo ya bunge kuwa ya hatari na isiyotabirika kwa mfano wa siku zijazo, lakini ikatoa wito wa kutambua hali halisi.

Kura iliyopigwa juzi na wabunge hao inamaanisha kuwa kuanzia kesho wabunge watafikiri juu ya kutoa nafasi kwa mapendekezo kadhaa ambayo wanatumaini yatakubalika kwa pande zote ili kuwezesha Uingereza kujitoa EU, hatua ambayo Waziri Mkuu May ameshindwa kukifanikisha. **VOA**

# Kortini tuhuma wizi wa mabaki ya madini

**Na Hellen Mwango**

WATU saba wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo wizi wa mapipa 20 ya mabaki ya madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 900.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mbando.

Wakili wa Serikali Jenifer Masue, aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Jacob Kihombo, Yahya Masoud, Mbaraka Lipinda, Ramadhani Zombe, Waziri Kibua, Mustapha Mnyika na Richard Sangana. Masue alidai washtakiwa hao, siku na mahali pasipofahamika jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kutenda kosa la wizi.

Alidai kuwa kati ya Februari 6 na 7, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, walitenda kosa la wizi wa mali inayosafirishwa. Katika shtaka la pili, siku na tarehe za tukio la kwanza, washtakiwa wote walidaiwa kuiba mapipa 20 ya mabaki ya madini aina ya tantalite.

Ilidaiwa kuwa madini hayo yana thamani ya Sh. 938,339,907 mali ya kampuni ya Bollore Transport and Logistics.

Shtaka la tatu, linamkabili mlinzi Zombe kati ya tarehe hizo akiwa mwajiriwa wa kampuni ya Bollore, alishindwa kuzuia kutendeka kwa kosa la wizi wa mapipa hayo ya madini.

Washtakiwa wote walikana mashtaka yao na upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Washtakiwa wote walirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ambayo ni kuwa na wadhamini wawili kutoka katika taasisi zinazotambulika na serikali watatia saini bondi ya Sh. milioni 52 kila mmoja.

Pia mdhamini au mshtakiwa alitakiwa kuwasilisha mahakamani hapo hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 52.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Aprili 9, mwaka huu.

# Zitto amjibu Msajili wa Vyama vya Siasa

INATOKA UK 8

za miezi miwili za mwaka 2013/2014 kuunganishwa katika mwaka wa fedha wa 2014/2015.

"Taarifa zote hizo ziko wazi kwa CAG na kwa Msajili wa Vyama vya Siasa na kwa nia njema angeweza kuuliza na angepewa taarifa sahihi, tulitimiza wajibu wetu, CAG naye alitimiza wajibu wake wa kutukagua. Hivyo basi chama chetu hakuna mwaka ambao hakijawahi kuwasilisha hesabu zake na mwaka 2015/2016 na 2016/2017 kilipata hati safi za ukaguzi kutoka kwa CAG, na Msajili anajua kuwa ndicho chama pekee chenye hati safi," alisema Zitto.

Akijibu hoja ya pili kuhusu wanachama wa chama hicho kudaiwa kuchoma bendera za CUF, Zitto alisema anaamini kwamba wanachama waliochoma bendera hiyo siyo wa ACT-Wazalendo.

"Kuhusu hoja ya kuchoma bendera na kadi, barua yenyewe ya Msajili iliyotufikia inasema kwamba imeona picha zinazoonyesha wanaodaiwa kuwa wanachama wa ACT-Wazalendo wakichoma bendera na kadi za CUF. Katika hili Msajili mwenyewe anaonyesha kwamba hana uhakika kama kweli wahusika ni wanachama wetu," alisema.

Alisema inashangaza Msajili anaamua kuandika barua ya kutishia kufuta chama cha siasa kwa tuhuma ambazo hata yeye mwenyewe hana uhakika nazo.

Kuhusu hoja ya tatu ya kutumia neno 'Takbir', Zitto alisema jambo hilo limewashangaza kwa sababu chama hicho kina wanachama wa dini zote.

"Barua hiyo ya Msajili inaeleza kwamba chama chetu kimevunja sheria ya vyama kwa sababu wanaodaiwa kuwa wanachama wetu wametumia maneno 'Takbir' kwenye shughuli za kichama na kwamba maneno hayo yana udini. katika Katiba yetu tumeonyesha wazi hatufungamani na dini yoyote na ndiyo maana tumeruhusiwa kufanya shughuli za kisiasa," Zitto alisema.

Alisema anafahamu kuwa Watanzania wana dini zao na wana maneno ambayo ni ya kawaida kutumia bila kuleta athari yoyote hivyo haoni sababu ya chama chake kubanwa kuhusu kutumika kwa neno hilo.

Zitto aliomba nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADEC), kufuatilia tishio la chama hicho kufutiwa usajili na ameahidi kuwasiliana na viongozi wa Jumuiya hizo kuhuhu jambo hilo.

Kuhusu kutakiwa kujibu hoja hizo katika kipindi cha siku 14, Zitto alisema watajibu kwa wakati na kwa vielelezo.

Wakati huo huo, Zitto alimtangaza Juma Duni Haji kuwa Naibu Kiongozi wa chama hicho na kwamba uamuzi huo umefikiwa na kikao cha uongozi cha chama hicho.

Duni alikuwa mgombea mwenza wa Edward Lowassa waliopitishwa na Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Ukawa ni umoja ulioundwa na vyama vya NLD, NCCR Maguezi, Chadema na CUF






# Ofisa uvuvi mahakamani madai ya rushwa milioni 5.1/-

**Na Rose Jacob,** MWANZA

OFISA Uvuvi Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mkuu wa Operesheni ya Uvuvi Haramu Wilaya ya Ukerewe, Judith Mafunda (48), amekamatwa na Takukuru kwa madai ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 5.1.

Akizungumzia tukio hilo Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Stenga, alidai Judith alipokea rushwa hiyo kutoka kwa mfanyabiashara, Thobias Kaswahili, kinyume na kifungu cha 15(1) (a) cha Sheria ya Takukuru Na. 11/2007.

"Ofisa uvuvi huyo aliomba na kupokea rushwa kutoka kwa Kaswahili ili aweze kumrudishia injini zake tatu za boti ambazo zilikuwa zimezikamatwa katika operesheni ya uvuvi haramu, Februari 2, mwaka huu, " alidai.

Adha, Stenga alidai Machi 3, mwaka huu, Kaswahili alifika ofisini kwa Judith kwa lengo la kupatiwa injini zake kwa mujibu wa maelekezo na badala ya kupatiwa mali zake na maofisa uvuvi baada ya kulipa faini, Judith alimuamuru ampatie Sh. milioni 5.1 ndipo ampatie injini zake.

"Ilipofika Februari 7, mwaka huu, Kaswahili alifika tena ofisini kwa Judith na kumpatia Sh. milioni tano na laki moja, lakini

hakumpatia stakabadhi wala injini zake kama alivyomuahidi," alidai.

Uchunguzi wa tuhuma hizo umekamilika na amefikishwa Mahakama ya Wilaya ya Ukerewe juzi na kufunguliwa kesi.

Akisomewa mashtaka na mwanasheria ambaye ni Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Wakili Maximillian Kyabona, mbele ya Mheshimiwa Hakimu Veronika Selemani, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo, yuko nje kwa dhamana na kesi yake imepangwa Aprili 4, mwaka huu, itakapotajwa tena.

# NEC kuanza uandikishaji

INATOKA UK 4

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uandikishaji huo unalenga kuvifanyia majaribio vifaa na mfumo wa uandikishaji wapigakura ili kubaini changamoto kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi hilo.

Sifa za watu watakaoandikishwa katika uandikishaji huo zimetajwa kuwa ni raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 au atakayetimiza umri wa miaka 18 siku ya uchaguzi mkuu ujao.

Aidha, uandikishaji huo hautawahusu raia walio chini ya kiapo cha utii wa nchi nyingine, aliyebainika kuwa hana akili timamu au yuko kizuizini kama mhalifu mwenye ugonjwa wa akili au yuko kizuizini kwa ridhaa ya Rais.

Taarifa hiyo imeendelea kutaja watu ambao hawatahusika katika majaribio hayo ya uboreshaji kuwa ni mtu aliyehukumiwa adhabu ya kifo na mahakama au anatumikia kifungo kinachozidi miezi sita pamoja na mtu aliyepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura chini ya Sheria za Uchaguzi au sheria nyingine yoyote inayohusu makosa ya uchaguzi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi pia inawajulisha wakazi wa kata hizo zinazofanya uandikishaji wa majaribio na ambao walijiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura mwaka 2015 kuwa wanaweza kutumia fursa hiyo kuhakiki taarifa zao katika vituo walivyojiandikishia.

Wakati huo huo, tume inatoa fursa kwa vyama vya siasa kuweka wakala mmoja katika kila kituo cha kuandikishia wapigakura kwa lengo la kushuhudia na kujiridhisha kuhusu taratibu zitakazotumika pamoja na changamoto zitakazojitokeza ili ziweze kupatiwa ufumbuzi kabla ya zoezi rasmi la uandikishaji.

Tume imevitaka vyama vyenye nia ya kuweka mawakala katika uandikishaji huo wa majaribio kuwasilisha orodha ya majina ya mawakala na vituo walivyopangiwa kwa maofisa waandikishaji wa Halmashauri za Kisarawe na Manispaa ya Morogoro.

Tume kwa mujibu wa Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa Sura ya 292 inapaswa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na unaofuata.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
26/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili: **T571 DHR/T961 DHT**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu*(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115139202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
26/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.
Kutoka DAR ES SALAAM kuelekea **TUNDUMA kupitia VIGWAZA** gari hilo lenye namba za usajili: **T569 DHR/T973 DHT**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115139202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
26/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili: **T244 DFJ/T745 DFD**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115139202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
26/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.
Kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili: **T239 DCN/T998 DCM**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115139202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
26/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 27-03-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA kupitia VIGWAZA gari hilo lenye namba za usajili: **T249 DCS/T135 DCP**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.84** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115139202

## KUPOTEA KWA VYETI




**Latifa Said Rashid** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1181/0046** kilichotolewa na shule ya Sekondari Senge mwaka 2015. Na Result slip ya kidato cha nne yenye **index namba S.1181/0046** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 na Result slip ya kidato cha sita yenye **index namba S.0526-0640** iliyotolewa na shule ya Sekondari Mringa mwaka 2018.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: SI/RB/9908/2018.**

115140602

## KUPOTEA KWA VYETI



**Betty Mntambo** anatangaza kupotea kwa vyeti. Kidato cha nne chenye **index namba S0302-0016** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka **1994** katika shule ya Sekondari Arusha, Cheti cha kidato cha nne chenye **Index namba P110/0004** likichotolewa na Baraza la Mitihani la taifa mwaka **1995** katika shule ya Sekondari Ilboru Centre.

Yeyote atakaeviona vyeti atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: MOR/RB/1620/2019**

115139902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Zera Mtebene** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0413-059** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1989 katika shule ya Sekondari Kibiti.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

Polisi Taarifa:
**BUG/RB/2036/2019**

215139702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Happy E. Somboi** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.1187-0552** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari **St. Mary Goreti.**

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**KMR/RB/3281/2019**

115139802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **EDWIN JOSHUA THOBIAS mkaaji** wa KIRUMBA, S.L.P 6642 DSM kabila mjaluo Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T 663 AFT** Aina ya **TOYOTA HILUX**

Kwa atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa kumb. **MW/RB/225/2019.**

115140502

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**BENSON MAKURILE NDARO** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina FUSO yenye namba za usajili ***T 964 ASZ*** Chassis FK618K51028 Engine Namba **6D17750559.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/1518/2019.**

115140202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**APOLONIA JOSEPH MUSHI.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye namba za usajili **T 467 CCF.** Chassis namba **LPSPJB56C78981.** Engine namba. **SL57FM1KWO23443.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/202/2019.**

115139102

**IN THE DELIGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**FOR DODOMA**
**MISC. CIVIL APPLICATION NO. 15 OF 2019**
**(Arising from civil case No. 28/2015 in the District Court of Dodoma at Dodoma)**

**HASSAN MOHAMEDI MHOJI......APPLICANT**
**VERSUS**
**LELLO JOHN PAUL..........1ST RESPONDENT**
**JOHN TARIMO.............2ND RESPONDENT**
**PETER NYAKU ...............3RD RESPONDANT**

**CHEMBARS SUMMON**

**Made under section 14(1) of the law Act cap. 89 (R.E.2002)**

Let all the parties concerned appear before HON. A.J kirekiano. RESIDENT magistrate sitting in chambers on the 14/05/2019 at 8.30 am hours in the morning or soon after when the applicant will be heard on the Application for the following orders.

THIS application has been taken at the instant of **HASSAN MOHAMEDI MHOJI.** The applicant and shall be supported by the affidavit of **HASSAN MOHAMEDI MHOJI** the applicant together with further grounds and reasons as will be adduced during the hearing of this Application.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of this court this 21/03/2019
Presented for filling 21/03/2019

115140202

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.21 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late ALOYCE MATHIAS MCHIWA-DECEASED**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by ANTHONY MNYAMAZI-PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

**Objections to the grant should be filed on or before 10TH /04/2019.**

**Dated at Dododma this ....21 /03/2019**

115140402

**MARMO CIVIL & BUILDING ENGINEERING**
**IYUNGA INDUSTRIAL AREA,**
**TEL : + 255 25 2562017/18**
**MBEYA.**

INATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE KADI YA PIKIKPIKI YENYE USAJILI WA NAMBA **T 728 CFB** ILIYOTOLEWA NA TRA.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA KUTOA TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI:
**MB1/RB/297/2019.**

215141102


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DE LIGT:
## Tutaona nitakapotua

**AMSTERDAM,** Uholanzi

NAHODHA wa Ajax, Matthijs de Ligt (pichani chini), amesema mtazamo wake ni kuichezea miamba hiyo ya Uholanzi licha ya kuongezeka kwa tetesi za kumhusisha na klabu kubwa Ulaya.

De Ligt, 19, ni mmoja wa wanasoka wanaokuja juu kwa sasa, na macho yote yameelekezwa kwa beki huyo baada ya mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong kusajiliwa na Barcelona.

Mabingwa wa La Liga, Barca wamekuwa wakihusishwa na safari nyingine ya Ajax – na wakati huu ni kwa De Ligt, ambaye pia amezivutia Juventus, Manchester City, Paris Saint-Germain na Bayern Munich.

De Ligt, hata hivyo, hatoi mtazamo katika tetesi hizo wakati huu Ajax ikijiandaa na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Juve mwezi ujao.

"Ninacheza mchezo wangu, mtazamo wangu ni soka na tutaona wapi nitakapomalizia," De Ligt aliliambia Esporte Interativo.

"Si kitu kinachonipa hofu. Kwa sasa ninaichezea Ajax na timu ya taifa, hivyo huko ndipo mtazamo wangu ulipo. Ninaongeza uzoefu na ninalipenda hilo."

De Ligt, ambaye alifunga wakati Uholanzi ikichapwa mabao 3-2 kwenye mechi yao ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Ujerumani Jumapili – ameshatupia mabao mawili katika mechi 25 za Ligi Kuu alizocheza msimu huu.

Beki huyo wa kati wa Uholanzi amefunga mabao manne katika mechi 32 alizocheza Ajax kwenye mashindano yote msimu huu wa 2018-19.







# MANE,
## Hazard kumfuta Mbappe Madrid

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imesisitiza kwamba hawana mpango wa kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, badala yake wanataka kuwashawishi Eden Hazard na Sadio Mane.

Huku Real wakiwa wana mpango wa kutengeneza kikosi kipya msimu ujao Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa hapo kwenye kikosi hicho cha Santiago Barnabeu.

Habari kwamba Real Madrid hawana mpango na Mbappe zimebainishwa na Gazeti la Marca, ambalo limesema kwamba, si Real wala Zinedine Zidane ambao wanampango wa kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 280.

Hata hivyo, Mane amekuwa akitajwa kuwaniwa na Real Madrid baada ya kuwa na msimu mzuri pale Liverpool.

Imebainishwa kwamba, Zidane alitaka kumsajili wingi huyo kabla ya kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kilichopita, na sasa anataka kuhakikisha anamsajili.

Mane amefunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho nne kwenye mashindano yote msimu huu na ameonekana kuwa mwiba mkali zaidi kwa Wekundu hao.

Mchezaji mwingine ambaye anatakiwa na Real Madrid ni Hazard, ambaye yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kutua pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Hata hivyo, kwa kuwa Chelsea hivi sasa imepigwa marufuku kufanya usajili, iwapo watamruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kuondoka, maana yake kwamba hawataweza kusajili mrithi wake.




# Barca hawamtaki tena Griezmann

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeondoa uwezekano wowote wa kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann, kwa kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Griezmann amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua Barcelona kwa misimu iliyopita na mwaka jana alikaribia kujiunga na Blaugrana kabla ya kuikataa ofa hiyo.

Nyota huyo aliamua kuikataa ofa ya kutua kwa miamba hao wa Catalunya na kusaini mkataba mpya utakamweka hapo Atletico hadi mwaka 2023.

Uvumi ulizagaa tena wiki iliyopita kwamba Griezmann anahusishwa na mpango wa kutua Barcelona, lakini sasa klabu hiyo imeonyesha haina mpango wa kumsajili mchezaji huyo.

Kwa mujibu wa Gazeti la Marca, Barcelona imebainisha kwamba meli yake imemwacha Griezmann na hawana tena mpango wa kumrudia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

Wawakilishi wa Mfaransa huyo awali waliwasiliana na Barca na kutaja bei ya mchezaji huyo kuwa euro milioni 200 na baadaye kushushwa hadi euro milioni 120.

Aidha, taarifa nyingine zinaeleza kwamba, Barcelona kwa sasa wamejitosa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Serbia, Luka Jovic, ambaye mkataba wake wa mkopo wa miaka miwili na nusu unafikia mwisho pale Eintracht Frankfurt.



# POGBA
## atajwa kutaka kwenda Madrid

**LONDON,** England

PAUL Pogba amekamilisha kile alichokipanga kwenye mafanikio yake baada ya kurudi England kwa mara ya pili mwaka 2016 na anataka kuondoka Manchester United wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Ripoti ya Gazeti la Daily Mail imeeleza kuwa, Mfaransa huyo atakwenda kujiunga ama na Real Madrid, klabu aliyoitaja kuwa kila mchezaji ana ndoto ya kucheza pale au kurudi katika timu yake ya zamani ya Juventus.

Gazeti la AS la Hispania liliandika Jumatatu wiki hii kwamba, Pogba ameonyesha nia ya wazi ya kutaka kwenda kujiunga na Real Madrid chini ya kocha Zinedine Zidane.

Gazeti hilo limebainisha kwamba, wakala wake, Mino Raiola tayari ameanza kazi ya kumtafutia mteja wake klabu sahihi ya kujiunga nayo na amebainisha kwamba Pogba hatakubali kusaini mkataba mpya na United.

"Kwa sasa akili ya Pogba inaifikiria zaidi Real Madrid kama chaguo lake la kwanza na pia Juventus kama chaguo la pili," kimeeleza chanzo kimoja kikinukuliwa na Gazeti la AS.

Pogba hivi karibuni alinukuliwa akisema kwamba ni ndoto ya kila mchezaji kwenda kucheza Real Madrid ambayo kwa sasa ipo chini ya Zinedine Zidane.

"Kucheza Real Madrid ni ndoto ya kila mmoja. Ni moja ya klabu kubwa duniani. Pia pale kuna Zidane kama kocha na ni ndoto ya kila mmoja anayependa soka," alisema Pogba wiki iliyopita.



# SOLSKJAER
## kufungwa jumla Man United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ipo mbioni kumpa mkataba wa kudumu kocha wake wa muda, Ole Gunnar Solskjaer (pichani), baada ya kuhudumu nafasi hiyo kama mwalimu wa muda akirithi nafasi ya Jose Mourinho.

Mourinho alifukuzwa Desemba mwaka jana baada ya kukaa na klabu hiyo kwa kipindi cha miaka miwili na nusu.

Licha ya kukumbana na kichapo katika mchezo wake dhidi ya Arsenal ikiwa ndio kipigo chake cha kwanza kwenye Ligi Kuu, Solskjaer sasa atapewa mkataba wa kudumu.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 46, raia wa Norway mpaka sasa ameweka rekodi bora kabisa ya kushinda jumla ya michezo 14 kati ya 19 aliyosimamia klabu hiyo tangu kuchukua nafasi ya Mourinho.

United siku zote imekuwa ikisema kuwa itafanya maamuzi kabla ya kufika mwishoni mwa msimu, lakini huenda akatangazwa mapema mno.

Kwa sasa Solskjaer yupo na familia yake nchini Norway akipisha kipindi hiki cha wachezaji kutumikia timu zao za taifa.

# Neymar, PSG waanza kujadili mkataba mpya

**PARIS,** Ufaransa

BABA mzazi wa Neymar Jr, amebainisha kwamba Mbrazil huyo yupo kwenye mazungumzo na Paris Saint-Germain kwa ajili ya kuongeza mkataba mpya na klabu hiyo.

Mshambuliaji huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Ufaransa tangu alipotua hapo kwa ada iliyoweka rekodi akitokea Barcelona mwaka 2017, huku Real Madrid ikipewa nafasi kubwa kumnasa.

Hata hivyo, katika mahojiano na UOL Esporte, Neymar Sr amebainisha kwamba uvumi huo hauna maana, kwani mtoto wake huyo kwa sasa yupo kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba wake ambao wa sasa unamalizika Juni 2022.

Alidai: "Watu wanasema mara zote Neymar yupo kwenye soko la usajili na kuhusishwa na klabu kubwa. Hii ina maanisha kwamba yupo kweye uongozi bora kwa sababu ni moja ya majina makubwa.

"Jina lake limekuwa likihusishwa na usajili tangu akiwa na umri wa miaka 17. Alifanya usajili mara mbili tu katika maisha yake hadi sasa, lakini uvumi ulikuwa zaidi ya mara 10.

"Uwezekano wa yeye kuondoka sio mkubwa. Yupo kwenye mwaka wake wa pili, ana miaka mitatu zaidi na sasa tunazungumza kuhusu kuongeza mkataba mpya na PSG."

"Neymar ni Neymar. Kesho wachezaji wengi wataanza kulinganishwa naye. Kama ambavyo watu walikuwa wakivutiwa na Pele, Zico, Romario, Ronaldinho na Ronaldo, itakuwa hivyo hivyo kwa Neymar.

"Kazi yangu kama wakala ni kumtengenezea mipango. Neymar hana muda wa kusoma na kuwa daktari, mwanasheria au mwandishi wa habari. Yeye ni mwanasoka. Changamoto yetu ni kuhakikisha maisha ya kumfanya kuwa mchezaji mzuri wa hapo baadaye."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO: JUVE MSIJALI NITAWAHI KUIVAA AJAX

**LISBON,** Ureno

CRSTIANO Ronaldo hayafikirii majeraha aliyoyapata wakati Ureno ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Serbia juzi na anaamini atakuwa tayari ndani ya wiki mbili hivyo kuiwahi mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax.

Ronaldo alitoka dakika ya 31 katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu michuano ya Euro 2020 iliyopigwa juzi jijini Lisbon baada ya kuonekana kupata matatizo ya misuli wakati akikimbilia mpira.

Lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 34, alisisitiza kuwa hajaumia sana na anatumai kuwa fiti kwa wakati kuuwahi mchezo wa robo fainali wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Ajax Aprili 10, mwaka huu.

Ratiba inaonyesha Juve itasafiri kwenda kuivaa Cagliari kwenye mechi ya Serie A kati ya mbili za nyumbani dhidi ya Empoli na AC Milan kabla ya kwenda Amsterdam kuvaana na Ajax.

"Sina hofu kuhusu hili, ninaujua mwili wangu," Ronaldo aliwaambia wanahabari. "Ninajua ninaweza kurejea ndani ya wiki ama mbili."

Ureno ilianza kuchapwa mapema kupitia bao la mkwaju wa penalti iliyozamishwa kimyani na Dusan Tadic, lakini kwa juhudi za Danilo Pereira, aliweza kuisawazishia timu yao kabla ya mapumziko.

Mabingwa watetezi hao wa Ulaya, walionekana kama wangeweza kuibuka na ushindi katika kipindi cha pili wakati Antonio Rukavina alipounawa mpira ndani ya eneo la hatari, lakini alikuwa ni mwamuzi Szymon Marciniak, alipobadili maamuzi yake ya awali ya kutoa penalti baada ya kuwasiliana na mshika kibendera.

Ronaldo alimlaumu refa kwa kubadili uamuzi wake kwa kusema: "Ilikuwa hasira, kwa sababu timu ilifanya kila kitu. Tulitengeneza nafasi, tulicheza vizuri - Serbia haikuwa na fursa kubwa.

"Kwa maoni yangu, refa alipaswa kutupa penalti. Mwamuzi msaidizi alikuwa mbali mita 40 na kufanya uamuzi kwa refa? Inaonekana kuwa geni kwangu ."

Kocha Fernando Santos, kadhalika, aliweka wazi, Marciniak aliomba radhi kwa makosa yake.

"Alinikaribisha kwenye chumba chake ili kutazama tukio hilo. Tuliona na hatukuwa na hofu, ama yeye au mimi, na kisha akaomba radhi," Santos alisema.

"Lakini kuomba msamaha hakunisaidii mimi. Hakuna yeyote ambaye yupo umbali wa mita 40 anaweza kusema si [penalti], zaidi kama refa ameona. Nini tutafanya na kuomba kwake msamaha?

"Msaidizi alikuwapo pale na alisema lilikuwa kosa lake."

Ureno haitacheza mechi nyingi tena ya kufuzu hadi September na kwa sasa ipo katika nafasi ya tatu kwenye Kundi B ikiwa na alama mbili kutokana na mechi zao mbili za kwanza, ambazo zote imecheza uwanja wake wa nyumbani.

## KWA UFUPI

### POGBA ATANGAZA KUONDOKA UTD

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba, 26, ameamua kuwa anataka kuondoka Manchester United majira haya ya joto na anapenda zaidi kwenda Hispania ama Italia. **(AS - in Spanish)**

### UMTITI KUPELEKWA SOKONI BARCA

Barcelona itazingatia kumuuza beki Mfaransa Samuel Umtiti, 25, kwa Manchester United katika majira haya ya joto, licha ya mchezaji huyo kuhitaji kubaki kwa miamba hiyo ya La Liga. **(Mail)**

### NEYMAR KUJIFUNGA TENA PSG

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, 27, yupo katika mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu kuongeza mkataba, baba yake amesema. Straika huyo amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid. **(ESPN)**

### SOLSKJAER KUTHIBITISHWA UTD

MANCHESTER United huenda ikathibitisha wiki hii kuwa kocha wa muda, Ole Gunnar Solskjaer, atapema jukumu hilo kama kocha wa kudumu. **(Mail)**

### ZIDANE AMBANIA MBAPPE REAL

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amemuweka mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, 20, kama chaguo lake la kwanza katika mpango wake wa usajili majira ya joto na anaweza kutoa ofa ya takriban pauni milioni 240.1. **(France Football - in French)**

### MANE KATIKA RADA ZA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane, 26, pia ni miongoni mwa wachezaji wanaowindwa na Real Madrid kuelekea dirisha la majira ya joto. **(Marca - in Spanish)**

### JUVE NAYO YAMFUATA VARANE

JUVENTUS imejiunga katika mbio moja na Bayern Munich, Manchester United pamoja na PSG katika mpango wa kuisaka saini ya beki wa kati wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane, 25. **(Sport)**

### SPURS YAMGEUKIA PERISIC

TOTTENHAM inajiandaa kumfuata winga wa Inter Milan, Ivan Perisic, 30, wakati huu klabu hiyo ya Italia ikihitaji pauni milioni 30 kwa Mcroatia huyo. **(TuttoMercatoWeb, via Star)**

### ARSENAL KWA MTOTO WA THURAM

ARSENAL inamtaka straika wa Guingamp, Marcus Thuram, 21, ambaye ni mtoto wa beki wa zamani wa Ufaransa, Lillian Thuram. Mkataba wa mchezaji huyo na klabu hiyo iliyopo ukanda wa kushuka daraja kwenye Ligue 1, unamalizika majira ya joto na pia anaivutia Borussia Dortmund. **(Sun)**

### HERERRA AFURAHIA TAARIFA PSG

KIUNGO wa Manchester United, Mhispania Ander Hererra, 29, amesema ni "mantiki" amekuwa akihusishwa na kujiunga na Paris St-Germain wakati huu ikiwa imebaki miezi mitatu tu katika mkataba wake na miamba hiyo ya Old Trafford. **(El Periodico - in Spanish)**

### CHRISTENSEN AFUNGUKA ZUIO CHELSEA

BEKI wa Chelsea, Mdenmark Andreas Christensen, 22, amesema wachezaji wameambiwa hawataruhusiwa kuondoka majira haya ya joto katika klabu hiyo ikiwa klabu hiyo haitaruhusiwa kusajili. **(Times)**

### CARRASCO AIIFUNGULIA NJIA ARSENAL

KIUNGO Mbelgiji, Yannick Carrasco, 25, ambaye aliwindwa na Arsenal katika dirisha la Januari, amesema "angependa" kurudi Ulaya na kuachana na Ligi Kuu ya China wakati huu akiitumiakia Dalian Yifang. **(Sun)**

### BENFICA KUMZUIA FELIX UTD, JUVE

BENFICA inataka kuongeza dau linalomruhusu kuvunja mkataba kwa mshambuliaji Mreno Joao , ili kuzizuia klabu kibao zinazomhitaji. Manchester United na Juventus zimekuwa zikihusishwa na kinda huyo mwenye umri wa miaka 19. **(Tuttosport - in Italian)**

## HABARI MICHEZO

RAHA TU...




Wafanyakazi wa Kampuni ya Mawasiliano ya Zantel, wakishangilia ushindi wa mabao 3-0, Taifa Stars iliyoupata mwishoni mwa wiki dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda (Cranes) na kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, zitakazofanyika nchini Misri. **MPIGAPICHA WETU**

# KAPOMBE AFUNGUKA, AREJEA UWANJANI

**Na Faustine Feliciane**

BEKI wa pembeni wa Simba, Shomari Kapombe, amesema anaishukuru klabu yake na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kusimamia matibabu yake ya mguu baada ya kuumia akiwa kwenye kambi ya timu ya taifa 'Taifa Stars'.

Kapombe alivunjika mfupa mdogo wa mguu akiwa kwenye kambi ya timu hiyo nchini Afrika Kusini wakati Stars ikijiandaa na mchezo wa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 dhidi ya Lesotho.

Akizungumza jana, Kapombe alifunguka kuwa matibabu ya mguu wake yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na klabu yake ya Simba na sehemu nyingine TFF.

"Naishukuru klabu yangu na TFF wamenisaidia matibabu ingawa kwa sehemu kubwa ni klabu iliyonitibu, kwa sasa naendelea vizuri nawashukuru kila mmoja kwa kweli," alisema Kapombe.

Aidha, alisema mwisho wa mwezi huu atarejea uwanjani kwa kuwa amepona na tayari ameanza mazoezi mepesi.

"Mwisho wa mwezi nitarejea uwanjani, naendelea vizuri na tayari nimekaa vizuri," aliongeza kusema Kapombe.

Katika hatua nyingine beki huyo wa pembeni amewapongeza wachezaji wenzake kwa ushindi kwenye mchezo dhidi ya Uganda na kukata tiketi ya kushiriki fainali za Afrika zitakazofanyika Juni mwaka huu nchini Misri.

"Kazi kubwa wamefanya... binafsi kama mchezaji na kama Mtanzania, nimefurahi sana kuona baada ya miaka zaidi ya 38 hatimaye tumefuzu fainali hizi za Afrika, ni furaha kwa kila Mtanzania," alisema Kapombe.

Kuumia kwa Kapombe, uongozi wa klabu ya Simba uliingia sokoni kusaka mbadala wake ambapo ulimsajili Zana Coulibaly kuziba nafasi yake, wakati Simba ikijiandaa kuanza kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi ambapo kwa sasa wamefika hatua ya robo fainali.

UTAMBULISHO...



Bondia wa kimataifa wa Tanzania, Hassan Mwakinyo (aliyevaa kofia), akitambulishwa na mwandishi wa michezo wa gazeti hili, Faustine Feliciane kwa Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe, baada ya kufanya ziara fupi chini ya wadhamini wake, Kampuni ya Sportpesa, katika Kampuni ya The Guardian kujionea jinsi inavyoendesha shughuli zake za kila siku. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# Mwakinyo: SportPesa imeniinua sana

**Na Faustine Feliciane**

BONDIA wa kimataifa wa Tanzania, Hassan Mwakinyo, amesema udhamini wa Kampuni ya SportPesa umechangia kwa kiasi kikubwa kufikia mafanikio aliyonayo sasa.

Akizungumza kwenye ofisi za gazeti hili jana, Mwakinyo, alisema ndani ya udhamini wa SportPesa umemsaidia kukutana na makocha bora duniani ambao wamempa ujuzi zaidi.

Mwakinyo wiki iliyopita alifanikiwa kumtwanga kwa (KO), bondia Sergio Gonzalez wa Argentina kwenye pambano lisilo la ubingwa lililofanyika jijini Nairobi, Kenya.

"Nashukuru sana wadhamini wangu, wamechangia kunipa ujuzi zaidi kwa sababu wamenikutanisha na makocha wakubwa ambao waliniandaa vizuri kabla ya pambano langu la Kenya," alisema Mwakinyo.

**Alisema anaamini kwa uwezo wa Mungu baada ya miaka mitatu ya udhamini wa kampuni hiyo atakuwa kwenye kiwango cha juu na kuweka rekodi kwenye mapambano yake.**

"Mkataba wangu na SportPesa ni wa miaka mitatu, kwa muda mfupi nimepata mashabiki wengi na jina langu kupaa, ndani ya mkataba huu nitakuwa mbali sana," alisema Mwakinyo.

Aidha, alisema kila atakapokuwa na pambano, wadhamini wake watamtafutia kocha wa kiwango cha juu na sehemu nzuri ya mazoezi kujiandaa.

Mwakinyo alianza kupata umaarufu baada ya pambano lake dhidi ya bondia Sam Aggington wa England Septemba mwaka jana, ambapo alishinda (KO) katika pambano lililofanyika mjini Birmingham nchini humo.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA


| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Michezo

Jumatano Machi 27, 2019

Nipashe


## Ronaldo: Juve msijali nitawahi kuivaa Ajax



HABARI UK. 30



Kinda wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, akiwatoka mabeki wa Montenegro kabla ya kutoa pasi ya mwisho kwa Ross Barkley aliyeifungia England bao la kwanza wakati wakishinda 5-1 ugenini kwenye mechi hiyo ya kuwania kufuzu Euro 2020 juzi. **PICHA: MTANDAO**

# KUISHUHUDIA STARS AFCON MISRI RAHISIII

### ●●● Mashabiki kama wote, nauli za ndege kushushwa, hosteli ya bei chee yatafutwa, Kamati Taifa Stars yaingia mzigoni huku...

**Na Faustine Feliciane**

ILI kuhakikisha Taifa Stars inafanya vizuri kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) Juni mwaka huu nchini Misri, mkakati wa kuhakikisha mashabiki wengi 'kama wote' kutoka Tanzania wanakwenda kuishangilia umeanza rasmi kwa kumulika unafuu zaidi wa gharama.

Mwenyekiti wa Kamati ya kuhamasisha timu ya Taifa 'Taifa Stars', Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema mikakati ya kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri kwenye fainali za Afcon umeanza na kila kitu wanatarajia kitakwenda vizuri ili kuwawezesha mashabiki wengi kwenda Misri kuisapoti timu yao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Makonda alisema kamati hiyo haitavunjwa na Ijumaa itafanya hafla ya kuwapongeza wale wote waliohamasisha na kusapoti juhudi za kamati hiyo, ambapo wanategemea kukusanya fedha zitakazoingia kwenye akaunti maalum ya kuhakikisha Taifa Stars inafanya vizuri na Watanzania wengi wanaisapoti timu hiyo.

"Katika hafla hii tunategemea zaidi ya kampuni 50 zitashiriki, huku tukitarajia kuwa na idadi ya watu 1,000 na tutatenga meza maalum kwa kampuni ambazo zitanunua meza hizo kwa Sh. milioni 10 fedha ambazo zitaingia kwenye akaunti maalum kufanikisha maazimio yetu," alisema Makonda.

Aidha, alisema kuwa kamati hiyo ipo kwenye mazungumzo na baadhi ya kampuni za ndege kuangalia uwezekano wa kushusha bei ili kuwawezesha Watanzania wengi kwenda Misri kuishangilia Taifa Stars.

"Tutaongea na ubalozi wetu Misri tunataka kupata 'Apartment' ambazo Watanzania watakaa hapo ikiwezekana kuwe na mtaa wetu wa Watanzania..., nafahamu kuna Watanzania wengi Misri na wanafunzi wanaosoma huko," aliongeza kusema.

**SHABIKI WA MANYARA AZAWADIWA**

Katika hatua nyingine, Makonda kwa niaba ya kamati hiyo alimzawadia Sh. milioni moja shabiki aliyesafiri kutoka mkoani Manyara kuja Dar es Salaam kuishangilia Taifa Stars.

"Huyu ameonyesha uzalendo mkubwa, amesafiri kwa baiskeli, pikipiki na gari kwa kuungaunga mpaka kufika Dar es Salaam kuja kuishangilia Taifa Stars..., vijana wanapaswa kuiga mfano huu wa uzalendo ulionyeshwa na kijana huyu," alisema Makonda.

Katika hatua nyingine, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, aliishukuru serikali, taasisi mbalimbali, vyombo vya habari na Watanzania kwa ujumla kwa sapoti yao kwa timu ya taifa iliyosaidia kufuzu kwa fainali za Afrika.

"Hakika ilikuwa hamasa kubwa na uzalendo wa hali ya juu ambao unapaswa kupongezwa kwa namna ambavyo kila mmoja alijitoa kwa nafasi yake kwa ajili ya timu yake ya taifa" alisema Karia.

Aidha, Karia ametuma salamu za rambirambi kwa familia ya shabiki kijana Ibrahim Hassan (7), aliyefariki nje ya Uwanja wa Taifa siku ya mchezo wa Stars dhidi ya Uganda kwa kukanyagwa na mashabiki.

Karia, alisema amepokea kwa huzuni taarifa za kijana huyo ambaye alikuwa na kiu ya kushuhudia mchezo huo.

Amesema shirikisho limeumizwa na tukio lililotokea na kusababisha mauti ya kijana huyo na kwa niaba ya TFF, ametoa pole kwa familia, jamaa, marafiki na wapenzi wa soka kwa kifo hicho, huku pia TFF ikitoa ubani wa Sh. 500,000 kwa familia ya kijana huyo.

## Simba, Yanga kazi inaendelea

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya majukumu ya timu ya taifa kwenye mchezo wa kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga vinarejea kwenye mikikimikiki ya michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Wakati Yanga ikisafiri kuelekea Mwanza kuumana na Alliance Jumamosi kwenye mchezo wa robo fainali wa Kombe la FA, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba wenye Jumapili wanakibarua kigumu mbele ya Mbao FC kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, alisema kuwa tayari wameweka mikakati kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo muhimu.

"Malengo ni kuona tunacheza michuano ya kimataifa mwakani... nafasi ya kufanya hivyo tutaipata kwa kufanya vizuri kwenye ligi au Kombe la FA," alisema Mwandila.

Alisema wachezaji wake wote wapo kwenye morali na kila mmoja anafahamu umuhimu wa mchezo huo utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Wakati Yanga ikijipanga kuwakabili Alliance, Simba wenyewe wapo kwenye mikakati kuhakikisha wanazoa pointi tatu kwenye mchezo dhidi ya Mbao na kuendeleza kasi yao ya 'kula viporo'.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia Nipashe jana kuwa kocha wa timu hiyo ameweka nguvu kwenye mchezo huo ambao atakuwa na nyota wake waliokuwapo kwenye kikosi cha timu ya taifa.

"Mazoezi yanaendelea na tunategemea wachezaji waliokuwapo kwenye timu ya taifa wataungana na sisi kujiandaa na mchezo wetu wa Jumapili," alisema Rweyemamu.

Simba ipo nyuma kwa michezo saba dhidi ya vinara, Yanga na Azam FC wanaoshika nafasi ya pili ambao wote wamecheza mechi 28.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >